

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 16 Aprili, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatuh Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Wabunge tukae, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 77

### **Kituo cha Afya na Zahanati Zilizojengwa na Mbunge**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Kwa juhudi zake Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale ameanzisha ujenzi wa baadhi ya majengo ya zahanati kubwa na za kisasa katika Vijiji vya Nyamikonze na Inyenze.

(a) Je, Serikali ipo tayari kusaidia kukamilisha ujenzi huo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuifungua zahanati illyojengwa na Mbunge katika Kijiji cha Mwamakilinga ambayo imekamilika tangu Novemba, 2014?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Nyang'hwale kupitia mapato ya ndani ilitenga shilingi milioni 45 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati ya Kijiji cha Nyamikonze, lakini ukamilishaji haukufanyika kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Nyang'hwale kuwa kidogo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Nyang'hwale kupitia mapato ya ndani imetenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Nyamikonze. Mpaka sasa zahanati hajaanza kufanya kazi na wananchi wa kijiji hicho wanapata huduma za afya katika zahanati ya Mwingiro iliyo karibu na kijiji hicho.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Nyang'hwale katika mwaka wa fedha 2017/2018 imetenga shilingi milioni 90 kutokana na mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati katika Kijiji cha Inyenze iliyofikia hatua ya kuezekwa. Fedha hizo bado hazijapatikana kutokana na makusanyo kuwa kidogo. Mara fedha hizo zitakapopatikana utekelezaji utafanyika kama mpango unavyoelekeza. Zahanati ya Mwamakilinga ilijoengwa na Mbunge wa Jimbo hilo, ilifunguliwa na Mheshimiwa *Engineer* Robert Gabriel, Mkuu wa Mkoa wa Geita tarehe 29 Januari, 2018 na mpaka sasa inafanya kazi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale alianzisha ujenzi wa majengo matatu katika Kituo cha Afya Kharumwa ambayo yote yalikuwa hatua ya lenta. Majengo hayo ni wodi ya watoto, wadi ya wazazi ambayo ndani ina chumba cha upasuaji wa dharura kwa wajawazito na jengo la kuhifadhi maiti (*mortuary*). Shirika la AMREFlinnaendelea na ukamilishaji wa jengo la wodi ya wazazi ambayo ndani ina chumba cha upasuaji wa dharura kwa wajawazito. Ujenzi huo unategemea kukamilika ifikapo tarehe 15, Mei, 2018 kwa gharama ya shilingi milioni 164.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua jitihada kubwa zilizofanywa na Mbunge wa Nyang'hwale, mwishoni mwa mwezi Desemba, 2017 Serikali ilitoa shilingi milioni 400 kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya Kituo cha Afya Kharumwa. Halmashauri imetenga shilingi milioni 70 kwa ajili ya ukamilishaji wa wodi ya watoto na shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la kuhifadhi maiti katika Kituo cha Afya Kharumwa. Ujenzi huo unaaendelea na unatarajiwu kukamilika ifikapo tarehe 30 Mei, 2018. Kiasi cha shilingi milioni 280 kilichobaki kitatumika katika ujenzi wa chumba cha upasuaji (*theatre*), maabara ya kisasa, nyumba ya mtumishi na wodi ya upasuaji (*surgical ward*) kwa wanawake na wanaume.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, swalil ya nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza, lakini naomba nitumie nafasi hii kuwapa pole wananchi wangu wa Jimbo la Nyang'hwale kwa mauaji ya kikatili ambayo yamefanyika wiki iliyopita, akina mama wanne wamenyongwa kwa kutumia kanga zao na wawili wakiwa wajawazito na mauaji hayo yanaendelea kwa Wilaya za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali dogo la nyongeza ni kama ifuatavyo; je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha kuisaidia Halmashauri ya Nyang'hwale ili kukamilisha ujenzi wa zahanati iliyopo lyenze na Mwamakiliga? Serikali ina mpango gani kuisaidia Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naishukuru *AMREF* kwa kukamilisha majengo matatu yaliyopo pale Kituo cha Afya Kharumwa. Serikali ina mpango gani baada ya kukamilisha majengo hayo kuendeleza kwa kutusaidia kuongeza vifaatiba pamoja na wauguzi? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa jithada zake za kuhakikisha wananchi wanapata huduma ilio bora ya afya. Yeye hakika ni mfano bora wa kuigwa kwa Waheshimiwa Wabunge wengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza, anauliza Serikali kusaidia Halmashauri kumalizia zahanati, ni nia ya dhati kabisa ya Serikali kuhakikisha kwamba tunasaidia, lakini kinachogombaa ni uwezo. Kwa hiyo, kadri bajeti itakavyokuwa imeboreka, hakika hatuwezi tukawaacha wananchi ambao Mheshimiwa Mbunge ameonesha jithada tukaacha kumalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili baada ya kazi nzuri iliyofanywa na AMREF, suala la zima la kupeleka vifaa pamoja na wataalam, ili kazi iliyotarajiwa iweze kuwa nzuri, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vya afya na zahanati zetu zote zinafanya kazi. Muda siyo mrefu, wakati tunahitimisha, Mheshimiwa Waziri wa Utawala atakuja kusema neno kuhusiana na suala zima la kuajiri watumishi wa Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, swali la nyongeza.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Mtikila kilijenga zahanati ambayo ilikamilika mwaka 2015, lakini mpaka leo hajifunguliwa kwa sababu ya tatizo la vifaa na wataalam. Namuomba Naibu Waziri aniambie, ni lini watafungua zahanati hii ili kutokudhoofisha nguvu za wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tulipokea katika michango ya Mheshimiwa Bobali na nikayarudia katika moja ya maswali ambayo nilikuwa najibu hapa, kwamba ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba zahanati ambazo zimekamilika huduma itatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nime tangulia kusema muda siyo mrefu kwamba ni siku ya leo ambapo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utawala atakuja kuhitimisha na atasema neno kuhusiana na suala zima la kupatikana wahudumu wa afya na waganga, maana na sisi tunategemea kupata kibali cha ajira kutoka kwake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira yaliyopo Jimbo la Nyang'hwale yanafanana kabisa na mazingira yaliyopo kwenye Jimbo la Ndanda na hasa kwenye Kata ya Chiwata ambapo kuna Shule ya Sekondari ya Chidya. Wananchi wa Chidya waliamua wenyewe kutumia nguvu zao kujenga jengo pale kwa ajili ya kuweza kupata zahanati. Kwa bahati mbaya kabisa, maelekezo niliyokuwa nawaambia, watakapokuwa wamefanikiwa kukamilisha boma, wawe wameendelea juu wameweka mpaka bati, Serikali itakuja kumalizia kuwaletea vifaa pamoja na kufungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ya kututaka tusubiri, lakini napenda watu wale wasikie, Chidya ni sehemu ya mkakati wa hiyo mikakati yenu ya Wizara kukamilisha maboma hayo na lini hiyo kazi itafanyika? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali na pia ni azma ya CCM; ukisoma katika Ilani ya CCM ukurasa wa 81 Ibara ya 50 tumetaja kabisa kwamba kila sehemu ambayo ipo kijiji tutahakikisha kwamba inajengwa zahanati, kila Kata itakuwepo na Kituo cha Afya na kila Wilaya itakuwa na Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, ni azma thabiti na ndiyo maana imeandikwa. Naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge avute subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba wananchi wake kama ilivyo Nyang'hwale wamejitlea, lakini sina uhakika kama naye

Mheshimiwa Mbunge amefanya kazi nzuri kama Mbunge wa Nyang'hwale. Na ye ye tumtake ashirikiane na Serikali, kwani wanaotibiwa ni wananchi wetu. Kwa hiyo, ni vizuri wote tukashiriki katika suala zima la kuhakikisha kwamba afya inakuwa bora. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Ntimizi, swali la fupi.

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nipongeze kazi nzuri ya kuboresha mazingira ya kutolea afya katika maeneo yetu kwa nchi nzima. Kutokana na shida kubwa ya afya iliyopo katika maeneo yetu tuliyokuwa nayo, Serikali ije na mpango mahususi wa kuhakikisha kwamba zile nguvu za wananchi katika maeneo yote waliyojenga maboma ya zahanati na nyumba za wauguzi, inawasaidia kumaliza maboma hayo. Je, Serikali lini itafanya hilo illi kumaliza shida ya afya katika maeneo yetu? Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mahususi wa Serikali upo na ndiyo maana katika bajeti hii ambayo tunakwenda kumaliza, jumla ya vituo 208 vinaenda kujengwa, lakini pia katika bajeti ambayo ndiyo tunaomba Waheshimiwa Wabunge leo wapitishe, nina uhakika kwamba ikipitishwa jumla ya shilingi bilioni 100.5 inaenda kutumika kwa ajili ya kujenga Hospitali za Wilaya 67 katika Halmashauri zetu. Hiyo yote inaonesha dhamira ya Serikali kwamba ina nia ya kuhakikisha kwamba tatizo la afya linaondolewa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunapopata fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza, tuyafanye mafupi kwa sababu tunapoteza muda wenyewe halafu tunaanza kulalamika. Usichangie kwenye swali la nyongeza. Tunaendelea. Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, sasa aulize swali lake.

Na. 78

**Tathmini Juu ya Ubora Katika Shule za  
Sekondari za Kata**

**MHE. HAMIDU H. BOBALI** aliuliza:-

Je, Serikali imefanya tathmini juu ya ubora na changamoto zilizopo katika shule za sekondari za kata nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la kitafiti la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchlinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 1995 hadi 2005 ni kipindi ambacho tafiti, tathmini, mikakati na mipango mingi katika sekta ya elimu, ikiwemo Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (*ESDP*) inayotekelze wa kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi (MMEM) kuanzia mwaka 2000 na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) kuanzia mwaka 2004 ilianzishwa.

Mipango hiyo ndiyo chimbuko la maamuzi ya kuanzisha Shule ya Sekondari kila Kata ili kuhakikisha watoto wengi zaidi waliokuwa wanakosa nafasi za masomo ya sekondari, licha ya kufaulu mitihani ya darasa la saba kwa sababu tu ya uchache wa shule wanapata nafasi hizo. Hadi mwezi Oktoba, 2017 tulikuwa na shule za sekondari za kata 3,103 zilizokuwa na wanafunzi 197,663 ambapo kama zisingekuwepo wangeikosa elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini mbili za Serikali zilizochambua kwa kina sekta ya elimu kupitia Tume ya Profesa Mchome ya mwaka 2013 iliyochambua sababu za ufaulu hafifu wa wanafunzi kwenye mitihani ya mwaka 2012

ya kidato cha nne na Kamati kuhuisha na kuoanisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo mwaka 1996, Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Elimu ya Msingi mwaka 2007 iliyoongozwa na Mwalimu Abubakar Rajab mwaka 2013, ndizo zilizobaini na kuishauri Serikali kuanzisha sera mpya moja ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera mpya imetoa maelekezo mahususi kuhusu namna ya kuboresha elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, elimu ya ufundu na elimu ya juu. Mitaala imesharekebishwa, ikama, vifaa, samani na miundombinu vyote hivi vinaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa shule mpya, ujenzi wa madarasa, vyoo, maabara, mabweni, maktaba, nyumba za walimu, ofisi ya walimu, mabwalo na majengo ya utawala unaoendelea nchi nzima kwa kushirikiana na wananchi; kuboresha upatikanaji wa vitabu vyta kiada na ziada katika shule za sekondari pamoja na juhudzi za Serikali kuhakikisha walimu wa kutosha wanapatikana hasa wa masomo ya sayansi na hisabati, ni uthibitisho wa namna Serikali ilivyo na dhamira ya kuinua ubora wa elimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba sasa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za kata tangu zimeanzishwa sasa takribani ni muongo mmoja; na kwa bahati mimi nilikuwa ni miongoni mwa walimu walioanzisha shule za kata. Matatizo na changamoto yaliyokuwepo mwaka 2006/2007 wakati shule za kata zinaanzishwa kama vile madarasa, ukosefu wa maabara, ukosefu wa walimu wa sayansi na hisabati, bado mpaka leo changamoto zile zipo.

Naomba sasa kujua ni lini Serikali itatuhakikishia kwamba changamoto za walimu wa sayansi, hisabati na madarasa katika shule zetu zitakwisha? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anazindua Mbio za Mwenge kule Geita, aliorodhesha mikoa inayoongoza kwa utoro na Mkoa wa Lindi siyo mionganoni mwa mikoa inayoongoza kwa utoro; bahati mbaya ni mionganoni mwa mikoa inayofanya vibaya sana katika matokeo ya kidato cha nne na matokeo ya darasa la saba. Moja ya mkakati wa Mkoa ni kuhakikisha tunatoa chakula mashulenii.

Naomba sasa leo Serikali *iji-commithapa*; je, iko tayari sasa kutuhakikishia kwamba sisi wa Mkoa wa Lindi tuendelee na programu ya kuwashirikisha wazazi ili waendelee kuchangia chakula ili matokeo yaweze kuboreka katika shule zetu? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kuanzia mwezi Oktoba, 2017 hadi sasa tumeajiri walimu 200 wa masomo ya sayansi na hisabati. Mpango uliopo hadi tarehe 30 Juni tutaaajiri walimu 6,000 na lengo tunataka kuondoa kabisa tatizo la walimu wa sayansi na hisabati katika shule za sekondari ifikapo mwaka 2020, maana yake inakwenda polepole.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la miundombinu pamoja na chakula, nimhakikishie Mheshimiwa Hamidu Bobali na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Serikali haijakataza michango ya wananchi kuchangia miundombinu ya shule zikiwemo maabara. Kilichokatazwa ni kumpa adhabu mwanafunzi ya kukosa masomo kwa sababu tu mzazi wake hajatoa mchango. Kwa hiyo, hiyo ndiyo iliyokatazwa, lakini kuititia Serikali za Vijiji, mnaruhusiwa kuendelea kuhamasisha wananchi ili wachangie maendeleo

ya shule zao ikiwemo miundombinu pamoja na chakula.  
*(Makofî)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, wamesema wanaajiri walimu wa sayansi, hisabati na kadhalika, lakini bado tatizo la walimu hao ni kubwa. Nataka kujua tu, wamefanya sensa, ni walimu wangapi wa sayansi ambao kila siku wanaacha kazi kwa sababu ya maslahi duni katika Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nabu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, hilo swali ni la takwimu kwa hiyo, kama huna takwimu hapo, unaweza ukampelekea Mheshimiwa majibu baadae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili ni gumu sana, kwa sababu hatuna takwimu za kila mwaka kwamba ni walimu wangapi wa sayansi na hisabati wanaacha kazi.

Lakini *comfort* nilyonayo na ambayo nataka niwape Waheshimiwa Wabunge ni kwamba malalamiko tuliyonayo ni ya walimu kutaka kuhama haraka katika shule wanaopelekwa, yaani mwalimu anaweza akapelekwa kwenye shule fulani, akikaa baada ya wiki mbili anataka ahame. Hiyo ndiyo changamoto kubwa tuliyonayo ambayo tunaishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuacha kazi, hilo naomba sana tutoe majibu baadae.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo yake Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kuwa kuna upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi. Pamoja na mikakati mizuri ambayo Wizara mnaifanya, mtambue kabisa kwamba walimu wetu wa sayansi wana *work load* kubwa sana uki-*compare* na walimu wengine. Tuna shule moja Wilaya ya Kilolo inaitwa Shule ya Lukosi ina mwalimu mmoja wa sayansi kati ya watoto 700.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu kwa Mheshimiwa Waziri; ni *incentives* gani kama Wizara imejipanga kuhakikisha inawapa motisha hata hawa walimu wachache waliopo ili wawe chachu kwa watoto wetu waweze kufanya vizuri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri ambalo ameonesha *concern* kubwa kuhusu walimu wa sayansi, namna ambavyo tunaweza tukawafanya wajisikie kwamba Serikali inawajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo tumefanya kama Serikali, ni kuhakikisha kwamba tumeweka *package* ambayo ni nzuri zaidi kwa walimu wa sayansi hata wanapoanza kazi kuliko hata walimu wa sanaa. Kwa hiyo, hiyo ni sehemu ya motisha kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasisitiza sana kwamba wanapofika katika shule, Walimu Wakuu na Maafisa Elimu wawapokee vizuri, wawape *counseling* ili wakubali kuishi katika maeneo wanayopelekwa, hilo ndiyo jambo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine tutaendelea kuboresha kwa sababu mengine hatuwezi kuweka motisha kubwa sana, kwa sababu nao ni watumishi sawasawa na watumishi wengine. Sasa kama utabagua, una watumishi ambao ni walimu halafu unabagua; huyu lazima apewe nyumba, huyu kwa sababu una uhasama naye, asipewe nyumba. Hicho nadhani itakuwa ni kitu ambacho siyo kizuri sana katika Taifa letu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swalii la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu la nyongeza ni kama ifuatavyo; mwaka 2016 tulipata tatizo kule Lindi kwenye shule ya sekondari ambayo ni shule kongwe. Wananchi wamejitalidi kadri walivyoweza lakini bajeti yake ni shilingi bilioni mbili. Serikali itatusaidiaje juu ya ujenzi wa shule hiyo ambayo iliungua moto mwaka 2016? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Salma Kikwete kwa sababu amekuwa akijitolea sana kuhusu kuinua elimu katika Mkoa wa Lindi, na hasa hii shule ya sekondari ya Lindi, ameichukua imekuwa kipaumbele kikubwa sana kwake. Kwa kweli namshukuru sana, ameongoza harambee nyingi, hata juzi tulikuwa kwenye harambee pale Dar es Salaam kwa ajili ya kuichangia hii shule na tukapata karibu shilingi milioni 282; na mwaka 2018 ilifanyika harambee zikapatikana shilingi milioni 550. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Salma Kikwete na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi na wananchi wa Lindi kwa ujumla

kwamba shule hii ambayo iliungua madarasa tisa na ofisi tatu za Walimu mwaka 2016, mwaka ujao wa fedha tutahakikisha kwamba madarasa 27 na ofisi tisa za walimu ambazo wamepanga kujenga yatakamilika. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Na. 79

### **Ujenzi wa Barabara**

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. JOHN J. MNYIKA)** aliuliza:-

Ujenzi wa barabara za mzunguko/mchepuko kwa kiwango cha lami ni muhimu katika kupunguza msongamano kwenye barabara kuu ya Morogoro.

(a) Je, ni lini barabara ya Tangibovu – Kibaoni – Goba – Mbezi – Malamba Mawili – Kinyerezi utakamilika?

(b) Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara nyingine za mzunguko/mchepuko katika Jimbo la Kibamba utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam na kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano mnamo

mwaka 2010 ilianza kutekeleza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za pete (*ring roads*) na zile za mchepuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zinazojumuishwa kwenye mpango huo ambazo ziko katika Jimbo la Kibamba ni barabara za Bunju 'B' – Mpiji Magohe – Victoria – Kifuru hadi *Pugu Kilitex* yenye urefu wa kilometa 33.7 na barabara ya mchepuo ya Tangibovu – Goba – Mbezi Mwisho – Msigani – Malambamawili – Kifuru – Kinyerezi hadi Banana, yenye urefu wa kilometa 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya mchepuo kuanzia Tangibovu – Goba – Mbezi Mwisho – Msigani – Malambamawili – Kifuru – Kinyerezi umetekelizwa kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara yenye urefu wa kilometa 16 kuanzia Tangibovu – Goba – Mbezi Mwisho umekamilika mwaka 2016;

(ii) Ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara yenye urefu wa kilometa nane kuanzia Msigani – Kifuru – Kinyerezi umekamilika mwaka 2017; na

(iii) Ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara yenye urefu wa kilometa mbili kutoka Mbezi Mwisho hadi Msigani pamoja na barabara ya kuingia na kutoka kwenye Kituo cha Mabasi Mbezi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Bunju 'B' – Mpiji Magohe – Victoria – Kifuru hadi *Pugu Kilitex* yenye urefu wa kilometa 33.7 ambayo inapita kwenye Jimbo la Kibamba utaanza mara baada ya usanifu kukamilika na fedha za ujenzi kupatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swalii la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri,

tunafahamu kwamba swalii hili limekaa muda mrefu kwa sababu hizi barabara zinafahamika kwamba zimekamilika kwa kiasi fulani kwa sasa hivi. Kuna barabara za muhimu ili kuweza kukamlisha matumizi na kupunguza foleni kwa wakazi wa Dar es Salaam na hasa Jimbo la Kibamba inayoanza Mbezi Mwisho - Mbezi Sekondari inayokwenda kuunganisha Bunju pamoja na Kibaha. Barabara hii mnategemea kuikamilisha lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hiso barabara nilizotajaji, kuna wananchi wa maeneo hayo walibomolewa nyumba zao, wengine wamewekewa 'X' nyekundu wanaka pale bila kuwa na amani kwa sababu hawajui lini wataondolewa; je, ni lini Serikali imepanga kulipa fidia ili kuweza kupisha wananchi wale, waendelee na kazi nyingine za maisha? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza napenda nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba upande wa Serikali tumejipanga vizuri kupunguza au kupambana na suala la msongamano wa magari. Kwa ujumla wake, zipo barabara zenye urefu wa zaidi ya kilometra 124 ambazo tunaendelea kuzishughulikia ili kuhakikisha kwamba msongamano unapungua na hatimaye unaweza kwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii lake la nyongeza, anataka kujua, lini hii barabara ya Mbezi - Kibamba itakamilika? Kubwa alilotaka kujua ni kama kuna *compensation*. Niseme tu kwamba kwa wale ambao wanastahili kulipwa fidia watalipwa baada ya fedha kuwa zimepatikana. Kwa hiyo, utaratibu unaendelea kwa wale wanaostahili. Niseme tu kwamba kwa upande wa Kibamba zipo barabara nyingi ambazo tunaendelea kuhakikisha kwamba tunasaidia kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, iko barabara ambayo inatoka Kibamba kwenda Kisopwa kilometa 12. Kilometra nne kutoka Kibamba kwenda Mloganzila imeshakamilika kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Kibamba, Serikali imejipanga vizuri kwa ajili ya kufanya marekebisho ya hizi barabara ili ziweze kupertika kiurahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge atapenda kujua maelezo ya ziada, ipo mipango mingi na barabara zipo nyingi, naomba tu tuonane ili wakati mwingine aweze kupata kwa undani kwamba ni barabara kiasi gani ambacho kinakwenda kutengenezwa upande wa Kibamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba kwa barabara hizi za kupunguza msongamano upande wa Kibamba tunazo barabara nyingi sana ukilinganisha na maeneo mengine kutookana na umuhimu wake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 80

### **Barabara ya Ntendo – Muze**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kujenga barabara ya Ntendo – Muze (kilometra 37.04) kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Barabara ya Ntendo – Muze yenyeye urefu wa kilometra 37.04 ina umuhimu wa kipekee kiuchumi kwa Bonde la Ziwa Rukwa, kwani ndiyo inayotumika kusafirisha mazao kutoka Bonde la Ziwa Rukwa kwenda kwenye masoko. Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara ya Ntendo – Muze imeendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii ili ipitike bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali kwa kiwango cha changarawe na zege hususan sehemu korofi na miteremko mikali ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Kwa sasa Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa na nchi jirani na hatimaye barabara za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi milioni 170 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa kiwango cha zege sehemu zenyeye miinuko na miteremko mikali maeneo ya Mlima Kizungu. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 ili barabara hii iendelee kupata matengenezo yatakayoiwezesha kupitika majira yote ya mwaka. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nashukuru Serikali kutambua umuhimu wa barabara hiyo kiuchumi. Barabara hiyo ipo toka enzi ya mkoloni na kutoekana na milima na miinuko iliyopo katika barabara hiyo, kipindi cha masika husababisha ajali nyingi sana, jambo ambalo huwatia hasara wananchi, pia Serikali kwa matengenezo ya mara kwa mara. Kwa nini Serikali isikubali kutengeneza hiyo barabara kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, maeneo ya mlimani ni kilometra nane, barabara hiyo ni finyu sana, ikitokea lori limekwama, hakuna gari yoyote inayopita na

husababisha adha kubwa kwa wananchi, kwa nini eneo hilo lisipanuliwe na kuwekewa kingo mlimani? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hili eneo la barabara hii ambalo linapita kwenye milima mikali amekuwa akilifuatilia sana mara nyingi, na mimi binafsi tumezungumza naye sana juu ya eneo hili na nilimwahidi pia kwamba baada ya Bunge hili nitatembelea eneo hili ili tuone namna bora zaidi ya kuweza kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua hii sehemu ambayo ina milima ndiyo maana kwa upande wa Serikali tunajenga barabara hii kwa kutumia zege na ninaamini kabisa tutakapokuja kufanya uamuzi wa kuweka lami katika barabara hii hatutarudia kufanya matengenezo kwenye sehemu hii ambayo tumeweke zege kwa sababu barabara iliyotengenezwa kwa zege ya *cement* inadumu kwa muda mrefu na inakuwa imara. Kwa maana hiyo ni kwamba matengenezo yanayoendelea ni sehemu ya mkakati wa kupunguza na kukamilisha matengenezo ya barabara katika sehemu hii korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wananchi wa Kwela kwamba tutalitazama vizuri eneo hili na ninatambua kwamba eneo hili la milima mikali na kule chini kuna utelezi mkali ambapo tunaweka changarawe. Kwa hiyo, tutaliangalia kwa macho mawili ili tuone namna bora ya kuboresha eneo hili. Barabara hii kama ulivyo sema ni muhimu, tutajipanga kama Serikali tuweze kuiangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wavute subira, wakati tunaendelea na michakato mbalimbali ya kukamilisha

barabara katika maeneo mbalimbali, eneo hili tutalitazama kwa makini. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara za haya maeneo, hebu watazame Wabunge huko. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni lini Serikali itakamilisha kutengeneza Barabara ya Bigwa – Kisaki kwa kiwango cha lami ikiwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimelitembelea eneo hili la barabara kutoka Bigwa – Kisaki kwenda mpaka Dutumi, nimeona upo umuhimu wa kufanya maboresho mbalimbali pamoja na kupanua madaraja. Ukienda upande wa Dutumi lipo daraja jembamba sana. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la barabara hii ni muhimu kwa sababu tunategemea pia barabara hii kuitisha mitambo na vifaa vingine wakati wa ujenzi wa umeme kule *Stiegler's Gorge* kilometa 189 kutoka Ngerengere.

Kwa hiyo, tutaitazama barabara hii na ni muhimu. Kwa sasa kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuboresha ili huduma ziendelee kufanyika wakati tunaendelea kujipanga kutengeneza hii barabara kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo.

Na. 81

### **Miradi ya Maji Mkoa wa Ruvuma**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kuanzisha miradi ya maji mikubwa na midogo na mingine imekabidhiwa kwa wananchi lakini haitoi maji.

Je, Serikali inaweza kueleza ni miradi ipi ya maji mikubwa na midogo iliyokamilika na isiyokamilika katika Mkoa wa Ruvuma na Wilaya zake zote?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naomba Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Halmashauri nane ambapo katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Serikali imetekeliza miradi katika vijiji 230 kwa Mkoa wote wa Ruvuma ambapo miradi katika vijiji 94 imekamilika na inatoa huduma ya maji. Miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji katika Halmashauri zote za mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Ruvuma umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 18.44 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi, ukarabati, usanifu, usimamizi na ufuutililaji wa miradi ya maji.

Aidha, Serikali itaendelea kutatua tatizo la maji safi na salama kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuibua miradi mipyä kwa kubaini vyanzo vya maji na kujenga miundombinu ya maji katika Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma sambamba na mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji mijini, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetekeleza miradi ya uboreshaji wa huduma ya maji katika Miji ya Songea, Namtumbo, Mbanga na Tunduru. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 miradi hiyo imekamilika kwa wastani wa asilimia 97 na imegharimu kiasi cha shilingi bilioni 2.6. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, swali la nyongeza.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tafsiri ya swali langu, nilipenda kujua miradi ambayo inatekelezwa katika Mkao wangu wa Ruvuma mimi kama mwakilishi wa mkoa ule, lakini majibu ya Mheshimiwa Waziri yameeleza kwamba kuna miradi ambayo inatekelezwa katika vijiji 230, vimekamilika vijiji 94.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kunisaidia kujua miradi hiyo ipo katika maeneo gani? Mimi kama mwakilishi wa wanawake wa Mkao wa Ruvuma nipate kujua ni ipi inatekelezwa ili nilete msukumo katika Serikali? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, ipo maradi miwili sugu ambayo inatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru. Kuna Mradi wa Mtina na Mradi wa Matemanga. Miradi hii ni ya muda mrefu sana na ilitakiwa iwe imekamilika. Hivi ninavyozungumza, Halmashauri imesitisha mikataba ya wale wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofahamika ni kwamba tafsiri ya wananchi ni kuona miradi inakamilika na inatoa maji. Je, nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha miradi hii inakamilika? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna

anavyowapigania wananchi wake, Mwenyezi Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wangu aliniagiza kwenda Mkoa wa Ruvuma kufanya ziara na kuangalia hali ya upatikanaji wa maji. Pamoja na kuangalia, nilijiridhirisha kupita katika Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma, lakini kuna kazi kubwa sana inayofanyika katika vijiji mbalimbali. Moja, Ngunguru, Mbesa, kuna Chandarua, Jeshini na Muungano, yote kuna sehemu ya utekelezaji wa miradi ya maji. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge anataka kujua vijiji vyake kwenye utekelezaji wa maji, nipo tayari baada ya Bunge nimpe nyaraka hii ambayo imeidhinisha vijiji vyote ambavyo utekelezaji wa maji upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, kumekuwa na kususua sana kwa miradhi ya maji kwa mfano Matemanga. Mimi Naibu Waziri nilifika pale kuona hali ya upatikanaji wa maji, lakini tumekuja kujifunza kwamba pamoja na Serikali kupeleka fedha, lakini kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya sababu ni watu kupeana kazi kishemeji shemeji au kiujomba jomba. Kwa hiyo, kwa kuwa kazi ya Waziri au kazi ya Wizara yetu ni kuhakikisha wananchi wanapata maji, tumeiomba Halmashauri isitishe mkataba na yule mkandarasi, watafute mkandarasi mwagine haraka ili wananchi wale waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Ngonyani, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Ngonyani, uliza swali lako halafu yote mawili atajibu Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri, samahani naomba ukae, ngoja aulize swali lake halafu utajibu yote mawili.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, ni pamoja na vijiji vya Wilaya ya Namtumbo. Nampongeza sana kwa safari yake na mambo makubwa tuliyoyafanya katika Wilaya ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu nifahamu, kwa kasi ile alioitumia kutatua miradi mitano ambayo ni ya *World Bank*, atatumia kasi ile ile kutatua miradi mitano mingine ili tutimize ile miradi kumi ya *World Bank*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kasi hiyo hiyo ambayo tumeitumia kukamilisha miradi inayoendelea, tutaendelea nayo kwa sababu bado tuna miradi 376 ambayo hajakamilika kutoka kwenye miradi 1,810. Kwa hiyo, kasi ni hiyo hiyo. Tunachosisitiza ni kwamba Halmashauri ziendelee kusimamia vizuri wakandarasi watekeleze miradi na sisi wakati wowote kutoka kwenye Mfuko wa Maji ukileta *certificate* tunalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji aliyomjibu Mheshimiwa Chikambo, Mheshimiwa Chikambo katika swali lake aliomba aletewe orodha ya miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wote, nilitaka tu nizungumze kwamba Wizara ya Maji inatenga fedha na inapeleka katika Halmashauri. Watekelezaji ni Halmashuri. Wao ndio wanaoweka mpango kazi kuona ni vijji gani watatekeleza. Kazi yetu sisi kuweka ni miongozo na wakishatekeleza, wanaleta hati, sisi tunalipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pia hilo ni jukumu la Waheshimiwa Wabunge wao wenyewe kwa sababu ni Madiwani kwenye maeneo yao kujuua ni miradi ipi inatekelezwa ni miradi mingapi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tutaendelea. Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, sasa aulize swali lake.

Na. 82

### **Ujenzi wa Bwawa la Matwiga - Wilayani Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwawa la Matwiga Wilayani Chunya?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Jimbo la Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia programu ya maendeleo ya sekta ya maji ilipanga kutekeleza mradi wa bwawa la Matwiga kwa awamu mbili. Katika awamu ya kwanza Serikali imekamilisha ujenzi wa bwawa la Matwiga lenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo 248,000 kwa ajili ya kuhudumia vijiji 16 vya Matwiga, Isangawana, Mazimbo, Mtanila, Igagwe, Kalangali, Lupa, Ifumwe, Lyeselo, Nkung'ung'u, Majengo, Magungu, Lualaje, Mwinji, Mamba na Mtande. Ujenzi wa bwawa hilo ulianza tarehe 17 Mei, 2015 kwa kwa kumtumia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Bwawa (*DDCA*) ambapo ulikamilika tarehe 23 Desemba, 2017. Hivi sasa mradi huu uko katika kipindi cha mwaka mmoja wa matazamio (*Defect Liability Period*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mvua nyingi zilizonyesha katika kipindi hiki ambapo bwawa lipo katika muda wa matazamio, kumetokea uharibifu kwenye baadhi ya miundombinu ya utoro wa maji (*spillway*) ambapo mkandarasi ameagizwa kufanya marekebisho na kuyakamilisha mara baada ya mvua za masika kusisima.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya utekelezaji wa ujenzi wa Bwawa wa Matwiga inahusu ujenzi wa miundombinu ya kutoa maji kwenye bwawa hili kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji vilivyokusudiwa. Tathmini ya kumpata mtaalam mshauri wa kusanifu miundombinu ya usambazaji wa maji inaendelea na usanifu wa miundombinu unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2018. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, swali la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili bwawa mwaka 2017 liliharibika *spillway*. *Spillway* ilikuwa upande wa mashariki mwaka 2016/2017 ikaharibika ile ambayo ilikuwa upande wa mashariki na mkandarasi akairekebisha akaiweka upande wa magharibi ambayo mwaka huu imeharibika. Sasa Serikali inasemaje kuhusu hilo na kuwahakikishia wananchi wa sehemu hizo kwamba *spillway* haitaharibika tena baada ya kuikarabati mwaka huu? La kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, bado niko kwenye maji Chunya Vijiini; Mji Mdogo wa Makongorosi una watu zaidi 20,000 na una uhaba sana wa maji. Hata ule mradi wa maji visima kumi kila kijiji Makongorosi walikosa maji. Sasa hivi wananchi wa Makongorosi pamoja na Mbunge wao, wamechimba kisima kwenye kijiji cha Ujerumani. Kisima kina maji mengi sana lakini hakina miundombinu ya kuweza kutoa maji hapo kuyapeleka kijiji.

Je, Serikali iko tayari kusaidia mradi huo ili kumtua mwanamke ndoo kichwani? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri inayoifanya katika Jimbo lake. Kama nilivyoeleza kuhusu suala la kuharibika kwa *spillway*, sisi kama Wizara ya Maji tunatoa fedha katika kuhakikisha wananchi wale wanapata mradi uliokuwa bora ambao utaweza kuwahudumia wananchi kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa ni kipindi cha pili mradi huo unaharibika, labda nitatuma timu ya wataalamu wetu wa Wizara kwenda kuhakikisha mradi ule ili mwisho wa siku ukamilike kwa wakati, lakini mradi utakaokuwa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali la pili kuhusu yeye pamoja na wananchi wake kuchimba kisima, lakini bado kumekuwa na changamoto ya miundombinu ya kuwafikiwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie sisi kama Wizara ya Maji hatututakuwa kikwazo katika kumsaidai yeye pamoja na wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosholeza. Kubwa nimwombe Mhandisi wa eneo hilo achangamke, asilale. Alete mchanganuo tuangalie namna gani tunaweza tukamsaidia ili wananchi wake waweze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Haule, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Bwawa la Kidete pale Kilosa ni bwawa ambalo kila mwaka linaleta maafa makubwa sana, reli inang'oka, wananchi wa Mabwelembwele, Masanze, Tindiga pamoja na Magomeni wamekuwa wakiathirika sana mafuriko makubwa. Mwaka 2017 nilipouliza Mheshimiwa Waziri alinijibu kwamba Serikali imeshatenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili muhimu la Kidete.

Je, ni lini Serikali itapeleka pesa hizo ili ziweze kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Kilosa? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Kidete nimelitembelea, nikakuta *topography* jinsi ambavyo imekaa, kidogo ni tete, kwa sababu juu ya bwawa kuna reli, chini kuna kijiji. Ukijenga bwawa ukaweka tuta kubwa ni kwamba maji yatazamisha reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na changamoto hiyo, tumeunda timu ya wataalam ambao walianza kazi mwezi uliopita na Mheshimiwa Mbunge nitakuomba tu wiki hili, nina imani watakuwa wameshamaliza kazi hiyo ili niweze kukujibu ni nini sasa kinafuata baada ya kukamilisha huo usanifu? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuwa Wilaya ya Ugunga na Jimbo la Igunga kwa ujumla lina uhitaji mkubwa sana wa mabwawa kama ilivyo Lupa; na kwa kuwa mabwawa ya Mwanzugi na Igogo sasa yamefikia uhai wake, yalijengwa miaka ya 1970, hayana nafasi tena ya kuendelea.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutujengea mabwawa mengine mawili kwa ajili ya umwagiliaji kama yalivyokuwa haya mabwawa mawili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwajigiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba mabwawa mengi uhai wake umeisha kwa sababu

ya mabwawa hayo kujaa udongo badala ya kujaa maji. Kwa bahati nzuri Jumamosi iliyopita, nilikwenda kutembelea Chamwino, nimeenda kutembelea Bwawa la Chalinze nalo nikakuta lina shida hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimeunda kikundi cha wataalam ili tujaribu kutafuta teknolojia ambayo inaweza ikayaondoa matope kwenye bwawa bila kutumia gharama kubwa. Tukishafaulu hilo Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie, tutatumia teknolojia hiyo ili kuhakikisha mabwawa yote nchini tunaondoa udongo badala ya kuanza kuchimba mengine. Sawa, mengine tutachimba, lakini haya yaliyopo ni lazima tuyahifadhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye, swalii la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nipongeze kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, inaonekana wanakwenda kwa kasi nzuri, lakini miradi mingi ya mabwawa na miradi ya umwagiliaji mingi inaanishwa lakini haikamiki, aidha, kutokana na upungufu wa fedha au kuwa imekuwa *designed* vibaya. Mfano mzuri ni miradi ya vijiji vya Utimbe, Runyu na Longa katika Jimbo la Mtama.

Sasa Serikali halioni kwamba ni vizuri wakaacha kubuni miradi mipywa *wa-concentrate* na kumalizia miradi hii ambayo kwa miaka mingi hawajaimaliza na pesa zimezama kwenye miradi hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba changamoto hiyo tumeiona katika Wizara yangu kwamba miradi mingi ilibuniwa lakini haikukamilika na haikukamilika kwa sababu miradi mingi imekuwa inatekelezwa na hela za wafadhili ambao wao wenyewe walikuwa wanachagua miradi, lakini

pia wanaweka *ceiling* ya fedha na wanalazimisha kwamba mradi huo lazima utekelezwe kulingana na *design* kwamba ile hela iliyotolewa haiwezi kufanya mradi sasa ukawa umekamilika na kuweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri na Kamati yangu imeliona hilo, tumelijadili na kuanzia sasa tunataka kuweka utaratibu maalum kwamba kama kuna fedha haitoshi, hakuna haja ya kutekeleza huo mradi. Lazima tuweke fedha ambazo tukishauanzisha mradi, tuchimbe bwawa, tuweke na *scheme* ili wananchi waendelee kufaidi matunda ya Serikali yao. Hilo Mheshimiwa Mbunge tumeshalionya na tunalfanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 83

### **Kupangisha Majengo kwa Fedha za Kigeni**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA** aliluliza:-

Wamiliki wa majengo wameanza kupangisha majengo kwa kutumia fedha za kigeni kama vile dola ya Kimarekani badala ya fedha ya Kitanzania hali inayosababisha kuendelea kuperomoka kwa thamani ya shilingi.

Je, Serikali ina mpango gani kuchukua hatua kulinda thamani ya shilingi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya fedha za kigeni sambamba na shilingi ya Tanzania hapa nchini yanasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Kigeni ya mwaka 1992, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006 na tamko la Serikali la mwaka 2007 kuhusu matumizi ya fedha za kigeni kulipia bidhaa na huduma katika soko la ndani.

Aidha, mwezi Desemba, 2017 Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alitoa tamko lingine kwa Umma kwamba kuanzia tarehe 1 Januari, 2018, matumizi ya fedha za kigeni hapa nchini yazingatia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bei zote hapa nchini zitangazwe kwa shilingi ya Tanzania. Bei hizi zinajumuisha kodi ya nyumba za kuishi na maofisi, bei ya ardhi, gharama za elimu na afya, bei za vyombo vya usafiri na vifaa vya kielektroniki.

Pili, bei ambazo walengwa wake wakuu ni watalii au wateja wasio wakazi, zinaweza kutangazwa kwa fedha za kigeni na malipo yake yanaweza kufanyika kwa fedha za kigeni. Bei hizi zinajumuisha gharama za usafirishaji kwenda nchi za nje kupitia Tanzania, gharama za mizigo bandarini kwenda nchi za nje, gharama za viwanja vya ndege na visa kwa wageni na għarama za hoteli kwa watalii kutoka nje ya nchi. Walipaji wanaotumia fedha za kigeni watambuliwe kwa vitambulisho vyao kama pasi za kusafiria na nyaraka za usajili kwa makampuni.

Tatu, viwango vya kubadilishana fedha vitavyotumika katika kuweka hizo bei katika sarafu mbili viwekwe wazi na visizidi vile vya soko. Ifahamike wazi kuwa ni benki ina maduka ya fedha za kigeni ndiyo pekee yanayoruhusiwa kupanga viwango vya kubadilisha fedha kutokana na ushindani katika soko la fedha za kigeni.

Nne, mkazi yejote wa Tanzania asilazimishwe kulipia bidhaa au huduma yoyote hapa nchini kwa fedha za kigeni. (*Makofi*)

Tano, vyombo nya dola viwachukulie hatua za kisheria wale wote watakaobainika kukiuka maagizo haya ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na matamko ya Serikali ya kupiga marufuku matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni ili kulinda thamani ya shilingi, hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei ya huduma na bidhaa, kuhamasisha usafirishaji na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi kuitia programu ya *Export Credit Guarantee Scheme* na kudhibiti biashara ya maote katika soko la fedha za kigeni hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutoa matamko ambayo hayatekelezeki. Hivi tunavyozungumza, matumizi ya dola yako pale pale. Bado zipo Taasisi za Serikali ambazo zinapata huduma au kutoa huduma kwa dola.

Je, ni lini Serikali itapitia upya sheria zake na kuona uwezekano wa kulinda shilingi kama ilivyo nchi ya Kenya au nchi ya Afrika Kusini ambapo huwezi kupata huduma bila kutumia *rand?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, utitiri *Bureau De Change* hapa nchini umeongeza m dororo wa shilingi na imekuwa kama ni vichaka nya kutakatisha fedha.

Je, Serikali haoni kama kuna haja ya kuwa na sheria mahususi za kubana *Bureau De Change?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa lazima tufahamu ni Bunge hili ndilo linalopitisha sheria na hivyo kama upungufu wowote,

Bunge hili litaleta mapendelekezo na Bunge liweze kuitisha sheria au kufanya mabadiiliko kwenye sheria zinazotumika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tufahamu kwamba katika misingi ya kiuchumi, matumizi ya fedha za kigeni hayasababishi kushuka au kudorora kwa thamani ya fedha yoyote ile duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tufahamu, Mheshimiwa Mbunge ametaja nchi ya Afrika ya Kusini; napenda kuliambia Bunge lako Tukufu katika fedha ambayo imepita katika misukosuko mikubwa ni fedha ya nchi ya Afrika ya Kusini pamoja na kwamba wana sheria ya kutotumia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba wananchi na Watanzania waelewe kwamba yapo mambo muhimu ambayo yanatasababisha misukosuko ya thamani ya fedha ya Taifa lolote, nayo ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni nakisi ya urari wa biashara; pili, mfumuko wa bei na tatu, ni tofauti ya misimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu limefanya vizuri sana katika hatua hizi ambazo nimezitaja; nakisi ya urari wa biashara; na ndio maana Serikali ya Awamu ya Tano inasisitiza kwenye kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini ili tuweze kusafirisha bidhaa zile ambazo zina thamani kubwa na kuhakikisha kuwa nakisi ya urari wa biashara ndani ya Taifa letu unakuwa ni mdogo na tumefika hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba Bunge lako tukufu waendelee kuipa *support* Serikali yetu, Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Serikali ya viwanda inayosisitiza kuongeza thamani ili tuweze kuhakikisha kwamba thamani ya shilingi yetu inakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, amesema utitiri wa *Bureau De Change*. Kama Mheshimiwa Mbunge amekuwa ni mfuatilaji mzuri, Serikali ya Awamu ya Tano imeongeza usimamizi katika *Bureau De Change*. Tumefunga zaidi ya maduka 92 ya kubadilishia fedha hapa nchini ikiwa ni katika jitihada za kuhakikisha kwamba maduka haya hayawi ni vichaka vyta kusafirisha fedha zetu na hayawi ni vichaka vyta kutakatisha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kusimamia, tumepewa dhamana ya kusimamia sheria mimi na Mheshimiwa Waziri wangu, sheria zote za kifedha, sheria za Taasisi za kifedha, tutaendelea kusimamia na kuhakikisha thamani ya shilingi yetu inaendelea kuimarika. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, sasa aulize swali lake.

Na. 84

### **Benki za Kibashara Mijini**

**MHE. GODFREY W. MGIMWA** aliuliza:-

Je, ni nini tamko la Serikali juu ya idadi kubwa ya Benki za Biashara kufunguliwa kwenye mijji mikubwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mabadiliko ya mfumo wa kiuchumi nchini unaotekelizwa tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990, shughuli nyingi za kiuchumi hususan benki zinaendeshwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sekta binafsi lengo lake ni kufanya biashara na kupata faida, uanzishaji wa huduma za Kibenki hutegemea upembuzi yakinifu ambao unazingatia zaidi fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo husika, uwepo wa miundombinu wezeshi na usalama. Kiuhalisia miji mikubwa inakidhi vigezo muhimu vya uwekezaji kwa sekta ya fedha kama vile uwepo wa fursa nyingi za kuchumi, miundombinu ya kisasa na usalama ikillinganishwa na maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na miji mikubwa kuvutia zaidi wawekezaji wa sekta ya fedha, Serikali inajitahidi kuboresha miundombinu katika maeneo ya vijijini ili kuweka mazingira bora na salama yatakayovutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi kuwa Serikali inaboresha kwa kasi miundombinu ya mawasiliano, umeme, maji na taasisi za usalama za umma ili kuhakikisha kuwa wawekezaji wanavutiwa kusogeza huduma mbalimbali zikiwemo huduma za kibenki karibu na wananchi. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, swali la nyongeza.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na nitakuwa na maswali mawili.

Mheshimiwa naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba inapeleka miundombinu kwenye vijiji na miji midogo. Hata hivyo, bado hakujakuwa na mbinu mbadala ambayo inaweza ikasababisha mabenki haya yakaenda kuanzisha benki katika vijiji. Napenda kufahamu, ingawa hakuna sera, sasa Serikali kwa sababu imeshafanya haya yote, ina utaratibu gani sasa kuhakikisha kwamba Benki zinapeleka huduma zao kule vijijini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba mabenki mengi hasa Benki za Kilimo na Benki ya Wanawake

bado hazijapata fursa ya kupeleka huduma vijijiini. Mwezi huu na miezi inayofuata benki hizi zitakwenda kufungua matawi Dodoma na Mwanza, lakini bado hazijagusa katika vijiji husika ambako kuna asilimia kubwa ya wakulima na wananchi wetu wapo kule ambao wanategemea sana shughuli za kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu; je, kwa nini sasa Serikali inaendelea kuruhusu mabenki haya kuanzishwa au kufunguliwa katika mijji mikubwa na siyo vijijiini ambako ndiko kwenye tija?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kukushukuru, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBNU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ameuliza kuhusu mpango mbadala.

Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba mpango mbadala upo na Serikali inausimamia vizuri na ndio maana katika huduma za fedha jumuishi, Taifa letu kwa Afrika nzima linaongoza kuwa na huduma za fedha jumuishi kama mpango mbadala wa kuwafikia wananchi kule walipo. Katika ulimwengu mzima, Taifa letu linachukua nafasi ya tatu kwamba linafanya vizuri katika kuhakikisha huduma za fedha jumuishi zinawafikia wananchi wetu kule walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni mashahidi, kumekuwa na wakala wa mabenki yetu, kumekuwa na huduma hizi kupitia makampuni yetu ya simu, wananchi wetu tunawafikia. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba tuko katika soko huria katika sekta ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kulazimisha mtu ambaye anakwenda kufanya biashara kwamba lazima afungue sehemu fulani. Serikali inachokifanya ni kutengeneza

mazingira mazuri na ndiyo maana tunaongoza katika Afrika katika mfumo wa huduma wa fedha jumuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu Benki yetu ya Kilimo na Benki ya Wanawake; napenda kuliambia Bunge lako tukufu kwamba kama yeye alivyokiri, mwezi huu wa tano na mwezi wa sita Benki yetu ya Kilimo inafungua tawi lake hapa Dodoma na kule Mwanza na hii ni katika jitihada za Serikali yetu kuhakikisha huduma za benki hizi ambazo zinafanya kazi moja kwa moja na wananchi wetu zinawafikia wakulima. Tuzipe nafasi benki zetu hizi tutawafikia wananchi kule walipo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Tutaanza na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, sasa aulize swali lake.

Na. 85

#### **Mradi wa REA katika Halmashauri ya Chalinze**

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE** aliuliza:-

Maeneo mengi ya Halmashauri ya Chalinze yamefaidika na Mradi wa REA Awamu ya Pili lakini katika utekelezaji wa mradi huo Miji ya Kiwangwa, Hondogo, Mkange na Kibindu bado haijafikiwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifikia miji hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kiwangwa katika Jimbo la Chalinze umepatiwa umeme kupitia mradi

uliotekelawa na *TANESCO* kwa ufadhili wa Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA) awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulishakamilika na wateja zaidi ya 600 wameunganishiwa umeme. Kijiji cha Hondogo kimepatiwa umeme kupitia mradi wa *densification* awamu ya kwanza uliokuwa unatekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya *STEG international Services* kutoka Tunisia. Kazi za mradi huu zimegharimu shilingi bilioni 1.16 ambapo wateja zaidi ya 66 wameunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Mkange kitapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA Peri Urban* utakaotekelawa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kilovolt 33 wenye urefu wa kilometa 26 kutoka Miono hadi Saadani utakaonufaisha Vijiji vya Manda, Mazingara na Gongo. Gharama za kuvipatia umeme vijiji hivi ni shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Kibindu kitapatiwa umeme kupitia njia ya umeme ya msongo *wakilovolt* 33 yenye urefu wa kilometa 66 kutoka shule ya sekondari Changarikwa. Njia hii ya umeme itanufaisha pia vijiji vya Kwaruhombo, Kwamdu, Kwamsanja na Kwankonje. Gharama ya kufikisha umeme katika vijiji hivi ni shilingi bilioni tano. Kazi hizi zitatekelezwa kupitia mradi wa *REA Awamu ya Tatoo*, mzunguko wa pili unaotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwaka 2021. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini mahitaji ya umeme katika maeneo mengi hasa katika Vitongoji vya Halmashauri ya Jimbo la Chalinze imekuwa ni muhimu sana. Kwa mfano, kule Msinune, Kiwangwa bado umeme haujafika na ahadi ya Serikali ni kwamba umeme hautaruka Kitongoji chochote.

Je, Serikali imejipangaje katika kuhakikisha kwamba inawapelekea umeme wananchi wanaoishi katika vitongoji hivyo vikiwemo vile ambavyo viro katika Kata ya Vigwaza na Mbewewe na maeneo mengine ya Halmashauri yetu? Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nami niwe mmoja wa kumtakia heri katika siku yake ya kuzaliwa Mbunge wetu wa Chalinze, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Ridhiwani atakumbuka kwamba mwezi wa Kumi na Mbili tulifanya ziara pamoja naye na Waheshimiwa Wabunge wengine wa Mkoa wa Pwani kwenye majimbo yao; tulipita katika maeneo ya Kata ya Kiwangwa, Msinune na Bago na Mheshimiwa Mbunge atakumbuka pia tuna mradi wa *densification* unaoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maeneo ambayo ameyataja ya Msinune na Bago ni maeneo ambayo yapo katika mradi wa REA Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza. Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge Serikali ya Awamu ya Tano kwa kweli kupitia miradi yake hii inayoendelea itapeleka umeme katika vitongoji mbalimbali ambavyo vina changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana kwa kazi yake ya kufuatilia hasa upatikanaji wa nishati ya umeme Jimboni Chalinze. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda. Kwa hiyo, tutamalizia swali la mwisho, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Machano Othman Said sasa aulize swali lake.

Na. 86

### **Watu Wanaokaimu Nafasi za Wakurugenzi**

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Kurugenzi nyingi za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki zimekuwa zikiongozwa na Makaimu, hali ambayo inapunguza ufanisi wa kazi.

Je, ni sababu gani za msingi zinazoifanya Serikali kushindwa kuwathibitisha makaimu hao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
(K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna Kurugenzi mbili ambazo Wakurugenzi wake wanakaimu kwa muda mrefu. Kurugenzi hizo ni Idara ya Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Jamii na Idara ya Biashara, Uwekezaji na Sekta za Uzalishaji.

Aidha, hivi karibuni Kurugenzi nyingine zinakaimiwa na Maafisa Waandamizi au Mabalozi kutokana na baadhi ya Wakurugenzi kustaaifu, kuhamishwa na kuteuliwa kuwa Mabalozi kwenda kuwakilisha nchi katika Balozi zetu za Beijing, Paris, Oman, New Delhi, Khartoum na Brussels.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya msingi iliyoifanya Serikali kutothibitisha Makaimu Wakurugenzi ni pamoja na Wizara kuwa katika mchakato wa kupitia muundo wake ili kujua idadi halisi ya Kurugenzi zinazohitajika, hivyo kuleta

ufanisi katika kazi. Mchakato wa kupitia muundo huo umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa taratibu za uteuzi wa Kurugenzi kwa ajili ya kuthibitishwa na kujaza nafasi hizo zinakamilishwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machano Said, swali la nyongeza.

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Wizara naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kumekuwa na Makaimu kwa sababu bado kuna muundo mpya unatengenezwa, lakini Ofisi ya Mambo ya Nje Zanzibar inakaimu karibu miaka miwili na ukiacha kukaimu, pia wana uhaba wa *staff* na samani za Ofisi katika Ofisi ya Zanzibar.

Je, ni lini Wizara hii itashughulikia Ofisi ya Zanzibar ili iwe sawa na sehemu nydingine za Muungano?

La pili, mionganoni mwa Kurugenzi zisizopungua 12 za Makao Makuu ya Wizara hii zote haziongozwi na Mzanzibar hata mmoja na kwa sababu Wizara hii ni kioo cha Muungano, Mheshimiwa Waziri anatuahidi nini katika muundo mpya kwamba Kurugenzi nydingine zitapata wafanyakazi kutoka upande wa pili wa Muungano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Machano kwa namna anavyowakilisha maslahi ya Zanzibar katika Bunge

la Jamhuri ya Muungano. Siyo mara ya kwanza kumsikia akifanya kazi hii kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niseme tu kwamba ni kweli kuna changamoto alizotitaja kwenye Ofisi ya Zanzibar nimwahidi tu kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha changamoto hizo zinafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la Wakurugenzi waliopo idadi yao Wazanzibar kuwa ni wachache, nimhakikishie tu kwamba Wizara ina Idara 14; siyo 12 kama yeye alivyosema. Nimhakikishie tu kwamba katika uteuzi utakaofanyika, bado Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba kigezo kukubwa inakuwa ni weledi, lakini kuangalia kwamba pande zote za Muungano zinawakilishwa vilivyo katika Wizara. Nashukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Matangazo yaliyotufikia, nawaona wageni wengi Bungeni, lakini majina yao bado hayajaja hapa mbele kwamba wageni wanatoka wapi, yatakapoletwa, basi tutawatambulisha wageni waliopo ukumbini leo.

Tangazo nililonalo ni zoezi la upimaji na ushauri wa afya, linaloratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yaani NHIF.

Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba kutakuwa na zoezi la upimaji na ushauri wa afya litakaloratibiwa na mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Wabunge, Watumishi na familia zao kuanzia leo tarehe 16 Aprili, 2018 hadi tarehe 28 Aprili, 2018. Huduma zitakazotolea ni kama ifuatavyo:-

- (i) Upimaji wa magonjwa ya moyo;
- (ii) Upimaji wa tezi dume;
- (iii) Uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi;
- (iv) Uchunguzi wa saratani ya matiti;

- (iv) Uchunguzi wa magonjwa kisukari; na
- (vi) Upimaji wa macho.

Zoezi hili litafanyika katika Kituo cha Afya cha Bunge kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni kila siku kwa kipindi cha wiki mbili. Zoezi hili linashirikisha Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*.

Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa wote kuchunguzwa afya zenu ninyi pamoja na familia zenu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo tunaendelea. Matangazo ya wageni yatawajia nitakapoletewa orodha yao.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Theonest.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mlinga.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Stanslaus Mabula.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Stanslaus Mabula Mwongozo.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Hussein.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, nimesha...

**MHE. GOODLUCK A.MLINGA:** Mlinga. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Sawa Waheshimiwa Wabunge, nimeshachukua majina yenu.

Niwakumbushe kabla sijaanza kuwaita, kanuni ya kuhusu Mwongozo, leo Mheshimiwa Mbunge atakayesimama kuomba Mwongozo ambao hauna uhusiano na Kanuni ya 68(7) nitamjibu vile ipasavyo, kwa sababu hiyo kanuni tumeshazungumza mara nyingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa anayesimama hapa awe anauliza swali lilitotokea hapa kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7) bila kuisoma kwa ajili ya kuokoa muda, mapema leo kwenye swali namba 84 liloulizwa na Mheshimiwa Mgimwa juu ya tamko la Serikali kuendelea kuruhusu idadi kubwa ya mabenki kufunguliwa kwenye miji mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linahusu fedha na uchumi wa nchi sambamba na jambo hili, nataka tu meza yako inisaidie, tunapozungumza habari za uchumi wa nchi haina tofauti sana na taarifa ya CAG. Hivi majuzi tu baada ya taarifa ya CAG mijadala mikubwa ililuka kwenye Bunge humu na nje ya Bunge pia na hasa pale ambapo Waheshimiwa Mawaziri walikuwa wanajaribu kueleza namna juu ya uchumi ni *stable* au hauko *stable*, lakini matamko mengine yamefuatia kuonesha kwamba jambo hili inawezekana sio sawa, huku nje wananchi wanachanganyikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka mwongozo wako ni nini kifanyike kama hivi ndivyo inavyoendelea. Je, ni sawa au si sawa. Nakushukuru sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu ulikuwa unahusiana na suala alilouliza Mheshimiwa Mabula, naomba niongezee kutokana na hilo Mawaziri wamekuwa wakijibu *randomly*, alijibu Mheshimiwa Harrison Mwakyembe nadhani na Mheshimiwa William Lukuvi kama sijakosea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Jafo.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Selemani Jafo yes.

Sasa nataka mwongozo wako nini kauli ya Kiti chako, ina maana ya baada ya wao kutoa kali hii ina maana hili suala limeisha? Kama ndiyo hivyo nami nataka nijipange na wananchi wa Ulanga tunakujaje kutokana na ripoti hiyo ya CAG. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7) sambasamba na Kanuni ya 100, 101(1) na (2) kama ikikupendeza nizisome.

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia hizo Kanuni nyingine.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 101(1) na (2) ikikupendeza nizisome.

**NAIBU SPIKA:** Endelea, maadam unaomba Mwongozo endelea na maelezo yako.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; ukiangalia katika *Order Paper* tuna Wizara mbili ambazo leo zitahitimisha hapa Ofisi ya Rais kuna TAMISEMI na ile ya Utawala Bora, lakini ukiangalia utaratibu mzuri wa Bunge kama Kamati utaona kwamba katika Fungu 56 ambayo ndiyo mshahara wa Waziri ule wa TAMISEMI na pia kuna *Teachers Service Commission Vote 2*. Ukienda kwenye Utawala Bora kuna *Vote 32* ukiachia mambo mengine. Sasa

utakuta ule utaratibu mzuri wa kuweza kuishauri na kuisema Serikali huwa hatuupati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo, ukienda kwenye *Vote 56* ukienda *Subvote 2001, Item 22010* kwenye *item* hiyo utakuta kwamba kuna fedha ambazo zimeongezeka zaidi ya bilioni nne ambayo ukiangalia kwenye randama utaambiwa hizi fedha ni kwa ajili ya chaguzi Serikali za Mitaa na kuna mabilioni ya fedha huko zimewekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasa tunaenda kila wakati kwenye mshahara wa Waziri *vote* moja baadae ni *guillotine*. Sasa wakati Bunge kukaa kama Kamati Wabunge inakuwa kama tunakwenda tu hatuelewi mambo mengi hapa tunapitisha tu, mabilioni ya fedha yanapitishwa unaambiwa ni uchaguzi wa Serikali za Mitaa lakini tunakwenda baadae unakuta hakuna kilichotumika na *CAG* amesema kuna wizi ubadhirifu wa kutosha wakati Wabunge wenyewe tunapitisha haya mafungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, utaratibu mzuri wa Bunge kukaa kama Kamati na namna ya kuishauri Serikali na kuisema Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Mkofi*)

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 47(1), (2) na (3) ikikupendeza nisiisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulivyokaa humu ndani asubuhi ya leo wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wapo wanateketea kwa mafuriko, mvua inanyesha tangu juzi, jana na taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa zinasema mvua itaendelea mpaka mwanzoni mwa mwezi Mei. Watu wanakufa, taarifa za asubuhi inasemekana watu takribani sita wamekufa na wengine kadhaa wamepata majeraha hiyo ni mvua ya siku mbili.

Je, mvua ikiendelea kwa wiki mbili mfululizo nini kitatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua hizi hazipaswi kuwa ni *disaster* kwa Jiji kwa Dar es Salaam iwapo miundombinu ya nchi yetu na miundombinu ya Jiji letu iko vizuri, mvua hizi zinapaswa kuwa neema kwa sababu kuna maeneo mengine yanakuwa na changamoto ya maji tungeweza kutengeneza mifumo mizuri ya miundombinu ya kutunza maji. Sasa kwa vile imekuwa ni kila siku, kila mvua zikinyesha ni watu kufa ni mafurika, barabara zetu kuharibika ninaomba sasa tujadili ukiona imekupendeza ni namna gani sahihi ya kuzuia hizi changamoto, Serikali imejipangaje kwa sababu ni suala linalotokea kila mwaka. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja ikikupendeza tuijadili. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa. Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 47(1) naomba niisome; "Baada ya muda wa maswali kuisha Mbunge wowote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zinavyooneshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge ijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma."

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani Geita hususani Wilaya ya Nyang'hwale kumekuwa na mauaji ambayo yanaendelea. Tarehe 5 na 6 Aprili, 2018 yamefanyika mauaji ya akina mama wanenye kwa kunyongwa kwa kutumia khanga zao na siyo usiku ni mchana. Hivi leo tayari nimepewa taarifa kupitia simu kuna binti mdogo mwenye umri wa miaka 17 amenyongwa jana, kwa hiyo mauji haya yanaendelea na pia nimepewa taarifa kwamba kijiji jirani cha Lwabakanga wamenyongwa watu wawili, lakini pia jirani upande wa Jimbo la Solwa Kijiji cha Salawi kuna watu wawili wamenyongwa jana; kwa hiyo ninaomba kama

itakupendeza basi Bunge liweze kujadili suala hili kwa sababu hofu imetanda, akina mama hawaendi kufanya shughuli zao za mashambani na kipindi cha kuvuna mazao kimefika, mpunga na mahindi wanashindwa kwenda kuyavuna na mvua zinaendelea kunyesha ina maana mazao haya yataharibika, na hofu imetanda kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, omba kutoa hoja ili tuweze kujadili suala hili. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama pia kwa Kanuni ya 68(7) kwa ajili ya kutaka *clear statement* kutoka Serikalini kutokana na kauli ambayo ilitolewa na Naibu Waziri ambayo imeleta mkanganyiko mkubwa sana kati ya Serikali na walimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Wizara ya TAMISEMI kauli ya...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kishoa Kauli ya Waziri yupi?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Mheshimiwa Joseph Kakunda aliyoitao humu Bungeni ambayo ilikuwa inakinzana na Naibu Katibu Mkuu wake wa Wizara kuhusiana na fidia ya walimu ambao wamehamishwa kutoka shule za sekondari kwenda shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Naibu waziri anajibu swalii la Mheshimiwa Rehema humu ndani alisema kwamba hawa walimu hawastahili kupata fidia kwa sababu maeneo wanayohamishiwa ni ndani ya kata, wakati huo Naibu Katibu Mkuu wake anasema hawa walimu wana haki ya kupata fidia ya posho pamoja na fedha ya usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri akasema tena

humu ndani kwamba hawa walimu hawana sababu ya kupata *on job training* kwa sababu walikuwa ni walimu wa shule za msingi wamejiendeleza na wakati huo Naibu Katibu Mkuu wake anasema wanastahili kupata *on job training* kwa sababu wametoka shule za sekondari wanahitaji kupata saikolojia ya watoto wa shule za msingi.

Sasa nilikuwa naomba *clear statement* kutoka Serikalini kwa sababu mpaka hivi ninavyoongea sasa kuna walimu wanaandamana kwenda kwenye Halmashauri na wanatumiwa *defender* za askari kwa ajili ya kupigwa kwa sababu wanakwenda kudai haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ituambie hawa Walimu mna mpango gani nao, fidia zinazotakiwa kutolewa zinatolewa lini? *Who is responsible?* Naomba Mwongozo wako kwa ajili ya *contradiction* hii ambayo inaendelea kuwatesa sana walimu wetu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joshua Nassari nitakupa nafasi naona nilikusahau kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo mbalimbali lakini pia kauna Waheshimiwa Wabunge ambao wametumia Kanuni ya 47 kuleta mambo ambayo wao kwa tathmini yao yanaonekana ni mambo yanayoweza kujadiliwa hapa Bungeni kama mambo ya dharura.

Waheshimiwa Wabunge, nianze na Mwongozo wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaye ameusema Mwongozo wake kutumia Kanuni ya 68(7) na akatoa maelezo ya kuhusu swali namba 84 ambalo lilikuwa linahusu fedha na uchumi kwa maana ya kwamba mabenki kufunguliwa maeneo ya mijini na vijijini, wakati akitoa hayo maelezo ametoa pia maelezo ya ziada kuhusu taarifa iliyotolewa na CAG na mijadala inayoendelea hapa Bungeni, lakini pia nije ya Bunge kuonesha kwamba wananchi huko nije, kama wanachanganywa hivi na maelezo yanayotoka kwa sababu watu hawajui kama ni sawa ama si sawa.

Wahehimiwa Wabunge, kwa kuwa Kanuni yetu ya 68(7) inataka kuzungumzia jambo lilitotokea hapa Bungeni, Mheshimiwa Stanslaus Mabula amelihusisha jambo ambalo liko kwenye swali namba 84 na kile kilichozungumzwa na CAG kama mtu ambaye anatueleza hali ya uchumi, lakini pia matumizi ya fedha hapa nchini. Kwa mujibu wa Kanuni zetu pia sheria tulizojitungia wenyewe, tusiwe wepesi sana wa kuzungumza mambo yale ambayo hatujazipitia sheria kwa sababu tukizungumza tunaonekana tumetoa msimamo fulani hivi kwa sababu ndivyo wananchi wanavyotuona, maana sisi ndiyo wawakilishi wao.

Waheshimiwa Wabunge, nimeipitia hii sheria kwa sababu iko hapa mbele ile sheria kama ambavyo haimkatazi CAG kuzungumza na Vyombo vy'a Habari kwa namna hiyo haimkatazi mtu yejote kuzungumzia taarifa ya CAG. Sheria hii hajasema CAG azungumze na vyombo vy'a habari na pia sheria hii haijamkataza mtu yejote ikiwa ni pamoja na Waziri, Naibu Waziri yejote anayetaka kuzungumzia taarifa hii. Ndiyo maana vyama vy'a kisiasa vingine siyo vyote kwa sababu tunavyo vyama vingi, baadhi ya Vyama vy'a Siasa vimeshatoka vyenyewe kueleza kile wanachoona inafaa. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, sheria hizi mkizipitia majibu huwa hayatolewi kwa mdomo, ukisema kwamba Waziri anajibu hoja za CAG, yeje anatoa mawazo yake hilo ni moja, lakini jambo la pili.....

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasikilizana na wengine hamkupata fursa ya kusoma sheria. Kwa hiyo, mzisome sheria vizuri tuwe tunasikilizana, kwa hiyo humu ndani anayeleta taarifa ya CAG Bungeni ni Waziri ndivyo sheria inavyosema, CAG hana mahali pa kupeleka hiyo taarifa isipokuwa kuitia kwa Waziri. Kwa hiyo, Waziri anapotoa maelezo siyo kwamba amejibu hoja za CAG, hoja za CAG zinajibwa kwenye Kamati kwa mujibu wa sheria na

anayejibu kwenye Kamati ni Afisa Masuuli husika, sasa tuisitake kuliweka hili jambo kwa namna ambayo tutanataka kuonesha hakuna utawala wa sheria ya nchi hii, sheria zipo tuzisome vizuri kabla hatujatoa maelezo ambayo yanaupotosha umma na yanapelekea sisi Wabunge kama hivi kuzungumzia mambo ambayo pengine hatukupaswa kuwa tunayazungumzia tungekuwa tunafanya mambo ambayo hata ninyi mmeyaombea Mwongozo hapa hasa Mheshimiwa Masoud. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwenye hili la Mheshimiwa Stanslaus Mabula Mwongozo wa Kiti ni huo sheria iko wazi kwamba ikishaletwa taarifa ya CAG hapa Bungeni mtu yejote anaruhusiwa kuizungumzia kwa sababu ni taarifa kwa umma, anayetoa majibu anatoa majibu kwa Kamati yale ndiyo yanayoitwa majibu mengine yote ni maoni ya kila mtu kama ambavyo nimeshawapa mifano kwamba kuna vyama ambavyo si lazima nivitaje vimeishaisoma na vyenyewe vinatoa maoni yake.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Goodluck Mlinga ambaye anasema anaongezea kwenye maelezo ya Mheshimiwa Stanslaus Mabula. Kwa hiyo, Mwongozo nilioutoa kwa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ndiyo huo Mheshimiwa Mlinga kama na wewe wananchi wakoa wanataka kuijadili hiyo taarifa wanaweza kuendelea kufanya hivyo huko kwenye Jimbo lako. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo mwingine umeombwa na Mheshimiwa Masoud ambaye ametusomea Kanuni ya 68(7)na pia ametaja Kanuni ya 101(1)na (2)ametoa maelezo kwa kirefu kuhusu *Order Paper* ya leo na kwamba tutahitimisha hoja ya Waziri wanchi ofisi ya Rais, TAMISEMI na hoja ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Akatoa maelezo kwamba mafungu yanayozungumzia mishahara ya Mawaziri ili Wabunge wapate kuihoji hiyo bajeti pia wapate majibu ya Serikali na ikiwezekana hii ndiyo sehemu ambayo wanaweza kushika shilingi. Kwa maelezo yake ametaja pia vifungu ambavyo vinaonesha fedha

zimeongezeka na pengine ingetolewa fursa Waheshimiwa Wabunge wangeweza kuhoji zaidi hapo katika kutimiza jukumu lao la kuismamia na kuishauri Serikali.

Katika maelezo amesema kwamba utaratibu tunaoutumia wa kupidisha mafungu ambao tunauita *guillotine* hautoi fursa ya Waheshimiwa Wabunge kupidia mafungu mengine kwa sababu ya muda. Mpaka sasa tumeshapitisha bajeti ya ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na mafungu yote yalipitiwa haikutumika *guillotine*.

Waheshimiwa Wabunge, hapa Mheshimiwa Spika aliwakumbusha kwamba unapoleta hoja uwe umeshazungumza na Wabunge kadhaa na akatumia neno la kiingereza la *lobbying*. Sasa Mheshimiwa Mbunge anasimama hapa anataka kushika shilingi, hajazungumza hata na jirani yake hiyo shilingi utaishikaje?

Kwa hiyo, imetokea utaratibu ambao tumejiwekea wenyewe na unatusumbua. Kila mtu anayesimama anataka kushika shilingi anataka ijadiliwe, lakini ukiangalia anashika shilingi kwa sababu zipi hakuna hata Mbunge atakayeungana naye hoja isipokuwa kwa kusimama na yeye kutaka kuzungumza, kwa hiyo muda wa kutokupitia mafungu ni wenyewe tunaupoteza la kwanza.

Jambo la pili Kanuni zetu namna tulivyoziweka zinaruhusu utaratibu huo, kwa hiyo kama utaratibu huo tunaona haufai ili tuwe tunaendelea mpaka pale tunapomaliza bila kupidisha mafungu kwa pamoja tunaweza kufanya hivyo, lakini hatuwezi kufanya hivyo wakati tukipitisha bajeti na Kanuni zetu zinaruhusu utaratibu wakupitisha mafungu yote.

Waheshimiwa Wabunge, tusishike shilingi wakati hatujafanya *lobbying* kwa jambo tunalotaka kushikia shilingi halafu tunaishia kuiachia baada ya muda mfupi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Masoud mwongozo wangu ni huo kwamba Kanuni zetu zinaruhusu huo utaratibu wa

kupitisha mafungu na Wabunge tuone ni namna gani tunaokoa wakati badala ya kuupoteza.

Waheshimiwa Wabunge, alisimama Mheshimiwa Lwehikila akieleza kuhusu matumizi ya Kanuni ya 47 jambo la dharura, akasema Dar es Salaam kuna mafuriko na mafuriko haya yanababishwa na miundombinu mibaya na mpaka sasa ametaja idadi ya watu ambao wamefariki. Mheshimiwa Lwehikila alitaka jambo hili lijadiliwe kwa dharura.

Mheshimiwa Hussein Amar nitayajibu haya yote kwa pamoja. Mheshimiwa Hussein Amar naye alisimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47 akieleza yale ambayo yeye ameyaeleza kama mauaji yanayotokea Nyang'hwale, Mkoani Geita na kwamba kuna watu kadhaa tayari ambao wameshafariki na kwa maelezo aliyoyatoa yeye ni kana kwamba hawa watu wananyongwa.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 47 inayo masharti pale ambayo yanatakiwa kutimizwa kabla jambo hatujaliita la dharura. Haya mambo yanayotokea Dar es Salaam na pia yanayotokea Nyang'hwale, Serikali iko humu Bungeni imeyasikia na iyafanyie kazi, lakini Bunge halitajadili kama mambo ya dharura kwa sababu yanao utaratibu wa kufanyiwa kazi na Kanuni yetu ya 47 inataka Bunge lijadili mambo ambayo hayawezি kutatuliwa kwa utaratibu uliopo wa kawaida. Kwa hiyo, Serikali, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hizi taarifa kuhusu Nyang'wale zifuatiliwe ili watu waweze kuwa salama katika maeneo yao na waendelee na shughuli zao za kiuchumi.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama pia Mheshimiwa Jessica Kishoa akitumia Kanuni ya 68(5) na akatoa maelezo kuhusu kauli ya Mheshimiwa Waziri aliyowahi kuitoa na amemtaja Naibu Waziri Mheshimiwa George Kakunda akisema maelezo yake aliyoyatoa yanapishana na ya Katibu Mkuu wake. Mheshimiwa Kishoa hakueleza jambo hili linahusiana vipi na mjadala tuliokuwa nao leo kwa maana ya kwamba kipindi chetu cha maswali na majibu na

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

ndiyo maana nikawaambia muisome ile Kanuni kila siku tunarudia mambo haya. Jambo ni lazima liwe limetokea Bungeni mapema siku hiyo ili liweze kutolewa ufanuzi. Kwa hivyo, Mheshimiwa Jessica Kishoa ulichokiomba Kiti hakina Mwongozo wowote kwa sababu jambo halijatokea hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, nitamruhusu Mheshimiwa Nassari halafu tutaendelea na ratiba yetu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu ilikuwa ni hiyo hoja ambayo umemaliza kuizungumza suala la CAG na majibu ya Mawaziri. Sasa kwa sababu sidhani kama ni busara kubishana na Kiti nadhani ni busara tu kwamba nikabaki kimya lakini tukubaliane kutokukubaliana. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa orodha ya wageni waliopo Bungeni leo nitaileta kwenu.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tunao wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika, wageni 66 wa Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, ambao ni viongozi wa Wizara wakiongozwa na Mhandisi Mussa Iyombe ambaye ni Katibu Mkuu, Dkt. Zainab Chaula - Naibu Katibu Mkuu wa Afya, Ndugu Tixon Nzunda - Naibu Katibu Mkuu - Elimu, Dkt. Binilith Mahenge - Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Ndugu Rehema Madenge - Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Ndugu Mariam Mvano - Kamishna *Teachers' Service Commission*. Hawa wameambatana na Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. (*Makofii*)

Wageni wengine ni familia yake ikiongozwa na Mama Kauthar Jafo ambaye ni mke wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa George Kakunda ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, wakiongozwa na Ndugu Warda Said Nassoro ambaye ni Mke wa Naibu Waziri. Karibu sana. Tunao pia mgeni wa Mheshimiwa Josephat Kandege, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambaye ni Mke wake naye anaitwa Flora Josephat Kandege. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na wageni nane wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni viongozi wa Chama cha Viziwi Tanzania wakiongozwa na Dkt. Haroon Magosho ambaye ni mlezi wa chama na Ndugu Theresia Nkwera ambaye ni Rais Chama cha Viziwi. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambao ni wakulima wa zao la katani Mkoa wa Tanga, wakiongozwa na Ndugu Eliamini Mrutu. Karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni jamaa zake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofii*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni viongozi wa CHADEMA kutoka Mkoa wa Mbeya na Arusha. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Musa Ntimizi ambao ni Wafanyabiashara kutoka Igala, Kata ya Goweiko, Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora, wakiongozwa na Ndugu Habib Sungu ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Uyui. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni viongozi wa Chama cha Wauza Pikipiki na Bajaj kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. Tunao pia wageni 67 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki Mkwawa kutoka Mkoani Iringa

wakiongozwa na Ndugu Ponsian Joshua. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni walio tufikia siku ya leo, wageni wetu mnakaribishwa tena siku nyingine kuja kujifunza shughuli za Bunge. Tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais,  
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais,  
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa  
Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji kabla ya wenye hoja hawajaja kuhitimisha. Tutaanza na Mheshimiwa Josephat Kandege ambaye atakuwa na dakika 15, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa sababu ndiyo mara ya kwanza nikihudumu katika nafasi ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba unipatie fursa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kunija alia kusimama leo kuchangia na kutoa baadhi ya ufafanuzi katika hoja zilizoletwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba uniruhusu kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Joseph John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu kunitua nihudumu katika nafasi ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Tatu, naomba niishukuru familia yangu, mke wangu na watoto wangu kwa

namna ambavyo wamekuwa wakiniwezesha kuweza kuhudumu katika nafasi hii. Nafasi ya nne, si kwa umuhimu ni kwa Chama changu cha Mapinduzi, wapiga kura wangu wa Jimbo la Kalambo kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakishirikiana nami katika kuhakikisha kwamba tunaweza kuhudumu katika nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa muda naomba uniruhusu niwatambue Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri ikiongozwa na Kamati yetu chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Dkt. Jasson Rwekiza na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mwanne Mcchemba, kwa maelekezo na ushauri ambao wamekuwa wakitoa katika Wizara yetu, hakika ni hazina kubwa sana kwa Taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba njikite kufafanua baadhi ya hoja kabla Mheshimiwa Waziri hajaja kufafanua hoja zitakazokuwa zimebaki. Katika michango ambayo imetoka kwa Waheshimiwa Wabunge ukianzia na Kamati kuna suala zima la ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge katika vikao kwa maana ya *DCC*, Mabaraza pia na kikao cha *RCC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakipata fursa ya kushiriki katika vikao hivi, michango yao imekuwa ya muhimu sana, imekuwa ikileta tija, tunahitaji sana uwepo wa Waheshimiwa Wabunge kushiriki katika vikao hivi. Ndiyo maana Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetoa waraka ikiwaelekeza Makatibu Tawala na Wakurugenzi kuhakikisha kwamba ratiba zao ambazo wanazipanga ni zile ambazo zitazingatia ratiba za Waheshimiwa Wabunge kuweza kushiriki katika vikao hivi ili michango yao ya maana ambayo tunahitaji iweze kuchukuliwa, kwa sababu wao ndiyo wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi ni pamoja na suala zima ambalo liliongelewa kwenye Kamati, hapa Bungeni halikutokea sana, lakini ni ukweli usiopingika kwamba Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakihitaji na

jambo ambalo ni la muhimu kuhakikisha kwamba hata ziara za viongozi wa Kitaifa wanapata taarifa ili washiriki, maana wao ndiyo wawakilishi wa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Nabu Spika, kuna hoja iliyojitokeza kuhusiana na suala zima la asilimia 10 ya mapato ya ndani kutengwa kwa ajili ya kwenda kwa akina mama pamoja na vijana. Waheshimiwa Wabunge, pia kwa wakati fulani waliongelea juu ya kuanzisha asilimia mbili kwa ajili ya kwenda kwenye kundi la watu wenye uhitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mujibu wa sheria iliyopo sasa hivi ambayo haioneshi dhahiri, umeandaliwa utaratibu wa kuhakikisha kwamba kwa kupitia *Finance Bill* ya mwaka 2018/2019 kipengele hicho ambacho kinampa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kuingiza katika sheria hiyo kipengele ambacho kitazitaka Halmashauri zote kuhikisha kwamba wanatenga na wasipotenga Wakurugenzi wachukuliwe sheria safari hii kitaweza kwenda kuwekwa humu. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba pesa hizi zinakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waheshimiwa Wabunge wengi walichangia juu ya suala zima la kuwawezesha akina mama na vijana kupata elimu ya ujasiriamali. Ni ukweli usiopingika kwamba ukienda kukisaidia kikundi bila kuwa na elimu ya ujasiriamali ni sawa na unapeleka fedha ambayo una uhakika kwamba haitatumika na kuleta mapinduzi makubwa ambayo tunatarajia yapatikane kwa vikundi hivi kwa maana ya akina mama, vijana lakini pia na kundi maalum la hawa watu wenye uhitaji maalum. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba jambo hili linaenda kutekelezwa na ninaamini Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha jambo hili pia atalifafanua kwa uzuri zaidi ili nia njema ambayo imekusudiwa na Serikali iweze kutimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa suala zima ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kuhusiana na uanzishwaji wa *TARURA*. Tunashukuru kwa pongezi ambazo zimetolewa kwa maeneo ambayo *TARURA* imeanza kufanya

kazi vizuri matunda yake dhahiri yanaonekana. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba chombo hiki ambacho kimeanzishwa kinaenda kufanya kazi ambayo tunatarajia ili yale maombi ambayo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakitoa/wakiomba baadhi ya barabara zao za kwenye halmashauri zao zipandishwe hadhi yanaenda kusita kwa sababu watakuwa wanaridhika juu ya utendaji wa chombo hiki cha *TARURA* ambacho kimeanzishwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kukiamini chombo hiki, chombo hiki bado ni kipyä. Tunahitaji kukiunda vizuri na Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda kwamba wakati *TARURA* inaanzishwa tumelazimika kuchukua watumishi waliokuwa kwenye Halmashauri ndiyo hao ambao wakaajiriwa. Lakini naomba niwahakikishie, *vetting* inaendelea kufanyika ili tuhakikishe kwamba wale tu ambao wana sifa na weledi ndiyo ambao watabaki kuendelea kutumika katika chombo hiki. Ni azma yetu kuhakikisha kwamba wale tu ambao wana ufanisi ndiyo ambao wataendelea kufanyakai *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ambayo imesemwa na juu ya suala zima la kuongeza pesa *TARURA*. Tunakubaliana na hoja hizi ambazo zimetolewa na Serikali katika kipindi ambacho Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati fulani akiwa anatoa ufanuzi, alisema ni vizuri tukatazama ndani ya Serikali namna bora ya kuweza kuhakikisha kwamba tunakiwezesha chombo hiki, lakini pia tukiwa na uhakika kwamba chombo hiki kinaenda kufanyakazi iliyokusudiwa na Waheshimiwa Wabunge na siyo suala tu la kuwa na bajeti kubwa ambayo haiendi kufanya kazi iliyokusudiwa. Kwa hiyo, tunaomba tukipatie fursa chombo hiki, tukijenge, tukiimarishe maana mwaka mmoja si umri mrefu. Naamini kadri siku zinavyokwenda chombo hiki kitasimama vizuri na tumepata pongezi kutoka maeneo mbalimbali ambapo *TARURA* imeanza kufanya kazi nzuri. Naomba nipongeze sehemu zote ambazo wamefanya kazi vizuri na wale wengine ambao wanaenda kwa kusuasua wajirekebishe, wahakikishe kwamba kile ambacho tumekusudia ndani ya Serikali kinaenda kufikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima ambalo limejitokeza kuhusiana na ujenzi na ukamilishaji wa zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali za wilaya. Ni ukweli usiopingika kwamba Watanzania wana kiu kuhusiana na suala zima la kupata huduma iliyo bora ya afya, kutokana na llani yetu ya CCM tumeliweka hili kwamba ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba kila kijiji inaenda kujengwa zahanati kwa kushirikisha wananchi lakini pamoja na kushirikisha Serikali, kila Kata tunakuwa na kituo cha afya na pale ambapo hamna hospitali ya wilaya, hospitali ya wilaya inaenda kujengwa.

Naomba niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba azma hii ya Serikali ni thabiti na ninatambua kabisa kwamba kila Mheshimiwa Mbunge sehemu ambayo hakuna kituo cha afya au hakuna hospitali ya wilaya angetamani hata leo au jana iwe imejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, safari ni hatua, ni vizuri tukakubaliana kwamba nia njema ya Serikali ambayo imeanzishwa ya kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya afya, zahanati tunaenda kuifanya. Katika nafasi hii nikiwa nahudumu nimepata fursa ya kutembelea maeneo mengi, muitikio wa wananchi kuhusiana na suala zima la ujenzi wa vituo vya afya haitiliwi mashaka, muitikio ni mkubwa sana, naomba niendelee kuwaomba wananchi kuendelea kushiriki katika kutoa nguvukazi yao na kusimamia kuhakikisha kwamba kila shilingi ambayo inatolewa inaenda kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufafanua hayo machache, naomba kipekee nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Selemani Jafo, Naibu Waziri mwenzangu Mheshimiwa George Kakunda kwa ushirikiano na maelekezo ambayo nimekuwa nikipata katika kazi yangu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu spika, Wenyeviti wote wa Kamati na Wabunge kwa ujumla kwa

ushirikiano ambao kwa kweli hata siku moja sijapungukiwa. Hakika Mwenyezi Mungu atasimama pamoja na ninyi kwa sababu dhamira ya kuwatumikia Watanzania iko dhahiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuwa Naibu Waziri katika Ofisi yake ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniokoa kwenye ajali mbaya ya gari iliyoitokea tarehe 6 Aprili, 2018 nikiwa katika utekelezaji wa mjukumu yangu, niliponea chupuchupu. Aidha, kwa mukhtadha huo naomba nimilie kijana wangu Mhandisi Izengo Ngusa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, aliyefariki usiku wa kuamkia jana kwa ajali ya gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru familia yangu, hususan Mke wangu Bi Warda na watoto wetu wote nane, wakiwemo sita nilioachiwa na marehemu mke wangu kwa kunipa ushirikiano wa kifamilia.

Aidha, naomba sana niwashukuru wapiga kura wa Sikonge na Chama cha Mapinduzi kwa imani wanayoendelea kuwanayo kwangu pamoja na majukumu ya Kitaifa. Ninamshukuru Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa uongozi wake wenye nidhamu ya kazi, weledi, uaminifu na uadilifu. Sisi Naibu Mawaziri wake ametufunza mengi sana kuhusu namna bora ya kutimiza majukumu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati niwashukuru Watumishi wote katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kazi za kujituma katika kutimiza majukumu yao, kipekee naomba nimpongeze na kumtambulisha Bungeni Mwalimu Magreth Lubelege, kama yupo asimame ambaye licha ya kufundisha katika shule ya kawaida huko katika Manispaa ya Ilala, alikuwa pia akienda kuwafundisha watoto watukutu kwenye mahabusu yao, Upanga. Aliwawezesha wengi kufaulu mitihani ya darasa la saba kabla hajastaifu tarehe 30 Julai, 2017. Wengi wa watoto hao wako sekondari, wako vyuoni, wako vyuo vikuu na wengine tayari wameajiriwa. Mwalimu Magreth Lubelege ni shujaa kwani amewabadilisha watoto watukutu kuwa watoto wazuri. Maneno yake ni mafunzo kwa wengine, anasema alipoulima na waandishi wa habari na nanukuu' "Mtoto kuwa gerezani si kwamba, hafai anafundishika ikiwa ataaelekezwa na kufundishwa kwa upendo." Mwisho wa kunukuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa walimu wote nchini kwamba, tumieni maneno ya Mwalimu Magreth Lubelege, waelekezeni watoto na kuwafundisha kwa upendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Waziri wetu alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imepata wachangiaji 71 waliozungumza Bungeni na wachangiaji 49 waliochangia kwa maandishi, nawashukuru sana Wabunge wote waliochangia. Wameonesha hisia zao za kutuunga mkono katika majukumu yetu yenye changamoto za mahitaji mengi yaliyopo kulinganisha na ukomo wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wote mlioutoa Waheshimiwa Wabunge tumeuchukua tukiamini kwamba, pale mlipokuwa wakali mlsukumwa na hisia za kutorodhishwa na utendaji wetu katika baadhi ya maeneo, tumewaelewa. Mnataka weledi, mnataka uaminifu, mnataka uadilifu, mnataka uzalendo na mnataka tuzingatia sheria, taratibu na kanuni za kazi, STK tutazingatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika masuala mahsus, ufanuzi wangu katika masuala hayo utakuwa ni ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Waheshimiwa Wabunge wengi ambao Mheshimiwa Waziri atakaposimama atawataja wamezungumza kuhusu umuhimu wa Serikali kujenga madarasa, vyoo, ofisi, nyumba za walimu, majengo ya utawala, mabweni, mabwalo, maktaba, maabara na kadhalika. Serikali ikiachiwa jukumu hilo peke yake tutachelewa mno, kwa mfano, kuanzia Julai, 2016 hadi Disemba, 2017 Serikali kupitia mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo pamoja na Mpango wa *Equip*, ilipeleka kwenye Halmashauri kiasi cha shilingi bilioni 106.5 mipango miwili kwa pamoja kukamilisha miundombinu ilioanzishwa na wananchi kwa mwaka 2017/2018. Katika mwaka 2018/2019 tumetenga shilingi bilioni 8.7 kwa ajili hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ni makubwa mno wakati bajeti za Serikali zina ukomo. Hivyo, tunahitaji kuendelea kushirikiana na wananchi, wadau wa elimu wa ndani na nje ya nchi, huku mhimili mkubwa ukiwa ni wananchi wenyewe. Waraka Namba Tatu wa Elimu wa mwaka 2006 unaoainisha majukumu ya wazazi, jamii na wananchi wa maeneo husika bado uko hai, kilichokatazwa ni kuwatumia walimu kulazimisha michango kwa kuwapa adhabu wanafunzi, kuwatoa darasani ambao wazazi wao hawajachanga michango, hicho ndicho kilichokatazwa. Adhabu hiyo, haikuwa halali kwa mtoto kwa sababu hana kosa lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia siku ulipositishwa utaratibu huo michango yote ya wananchi kwa ajili ya miundombinu, chakula na hata kambi maalum za kimasomo inatakiwa iratibiwe na Serikali za Vijiji kupitia mikutano yao ya kisheria na taarifa lazima zitolewe kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, kuhusu viwango vya michango vilivyokubaliwa na kiasi kilichochangwa ili Halmashauri iratibu utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili na la muhimu sana, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia

kuhusu tatizo la upungufu wa walimu kwenye shule za msingi, pamoja na shule za sekondari, hususan walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukiri kwamba tatizo hilo lipo kama ifuatavyo; mahitaji katika shule za msingi ni walimu 273,454 waliopo 175,946, kwa hiyo, upungufu ni walimu 97,508. Mahitaji ya walimu wa masomo ya sayansi na hisabati katika shule za sekondari ni 35,136 waliopo ni 19,459, kwa hiyo, upungufu ni walimu 15,677. Tuna ziada ya walimu wa masomo ya sanaa katika shule za sekondari ambaao ni walimu 21,165 ambapo wengi wao wana vipindi vichache sana vya kufundisha. Serikali inaendelea kuchukua hatua zifuatazo kurekebisha tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kwanza, kwa kuwa walimu wa masomo ya sanaa waliozidi katika shule za sekondari ni rasilimali watu ya Serikali, ili rasilimali watu hiyo itumike vizuri na kwa kuzingatia upungufu mkubwa wa walimu uliopo katika shule za msingi, imeamuliwa walimu hao 21,165 wahamishiwe kwenye shule za msingi. Huo ni uhamisho wa kawaida kutoka kituo kimoja cha kazi kwenda kituo kingine cha kazi, kazi hiyo ni hiyo hiyo ya ualimu. Mshahara ni ule ule haubadilishwi, daraja ni lile lile, kipaumbele cha juu katika uhamisho huo ni kuanza na walimu ambaao zamani walikuwa katika shule za msingi wakajiendoleza kwa kusoma diploma au shahada ya kwanza ambaao umahiri wa saikolojia ya watoto wa shule za msingi tayari wanao na wanayafahamu mazingira yaliyoko katika shule za msingi, wakiisha hao tunaenda kwa walimu wenye diploma na wakiisha tunaenda kwa walimu wenye shahada ya kwanza. Walimu wenye shahada ya uzamili hawahusiki na uhamisho huo isipokuwa kwa kibali maalum au maombi binafsi ya mwalimu mwenyewe na hayo ni maelekezo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa agizo hili hadi ilipofika tarehe 31 Machi, 2018 jumla ya walimu 8,834 wamehamishiwa katika shule za msingi. Tumeyasikia malalamiko, tatizo kubwa liliopo ni utayari wa wanaohamishwa. Kuhamisha bila kuzingatia maelekezo

tumeona katika baadhi ya maeneo na pia mazingira yale ya wanakopokelewa, jinsi ambavyo wale wanaotakiwa kuwapokea jinsi wanavyowapokea, hilo nalo limekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaagiza Wakurugenzi na Maofisa Elimu katika Halmashauri zote kutengeneza mazingira bora ya utayari wa wanaohamishwa na pia wanaowapokea kwa kuanzia na wao wenye Maafisa Elimu wa Wilaya na Wakurugenzi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi zinazotakiwa kuzingatiwa pale anapohamishwa mtumishi, *standing orders*, lazima zifuatwe. Mfano, kama mtumishi anahamishiwa mbali na kituo chake cha kazi, lazima kumlipa posho stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mukhtadha huo natoa wito kwa walimu wa sanaa waliozidi katika sekondari wakubali uhamisho ili waendelee na kazi hadi watakapostaafu kwa umri. Serikali inatambua kuwa licha ya tofauti ya lugha ya kufundishia mafunzo ya msingi kuhusu zana za kufundishia na saikolojia ni yale yale hakuna tofauti kubwa. Mukhtadha wa masomo ni ule ule, kama ni somo la historia ni lile lile, jiografia ni ile ile, kiswahili ni kilekile na kiingereza ni kile kile. Mwalimu anapofika kwenye kituo kipyta cha kazi anachotakiwa kufanya ni kuchambua zana za kufundishia na ndani ya muda mfupi atajenga umahiri na weledi unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya masomo Maafisa Elimu wanaweza kuandaa mafunzo elekezi kwa njia ya mikutano ili kuelimishana vizuri zaidi kuhusu utekelezaji wa agizo hili la Serikali linalolenga kupunguza upungufu wa Walimu kwenye shule za msingi kwa asilimia 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine ni kuwa Serikali itaendelea kuajiri walimu kama hivi, tumeponga ifikapo Juni tuwe tumeajiri walimu 16,130, mwaka ujao tutaaajiri walimu wengine 15,000 lengo ni kupunguza na kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa walimu wa sayansi katika shule za sekondari, ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia ni umuhimu wa taulo za kike kwa wanafunzi wa kike. Suala hili ni muhimu sana, lakini linatakiwa kuandaliwa kwa umakini kwa kuzingatia sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kwanza ni tofauti zilizopo kati ya familia zinazoweza kuwanunulia watoto hao taulo hizo na familia maskini ambazo hazina uwezo huo.

Jambo la pili, ni tofauti za kimazingira zilizopo baina ya shule za mijini kwenye urahisi wa kupatikana taulo hizo na shule za vijijini hasa vijiji vya mbali sana na miji ambako hata kama mtu ana fedha anaweza asipate taulo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya tatu, tofauti za ubora wa taulo zenyewe kutokana na viwanda zilikotengenezwa ili kuwa na uamuzi sahihi wa taulo zipi ni muafaka kutumika kwa wanafunzi wote wa kike katika shule zetu.

Nne, tofauti za bei ya taulo hizo kutoka eneo moja hadi lingine ambayo inaweza ikasababisha ugumu wa kupanga bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzingatia sababu hizo, Serikali imeichukua hoja hiyo, ili mwaka 2018/2019 utumike kufanya uchambuzi na tathmini ya kina, ambayo hatimaye itatushauri kuhusu namna bora zaidi ya kutekeleza pendekezo hilo. Hatua ambazo tumeshaanza kutekeleza kwa sasa ni pamoja na kutoa maelekezo yafuatayo:-

(i) Kila shule iwe na mradi wa maji ikiwemo uvunaji wa maji ya mvua kwenye maeneo ya vijijini na shule za mijini waunganishe huduma za maji kutoka mamlaka za maji mijini.

(ii) Vilevile katika ujenzi wa vyoo vya shule wahakikishe chumba maalum kinatengwa mahsus kwa ajili ya watoto wa kike kujihifadhi; na

(iii) Mwisho Wakuu wa Shule waendelee kuwatambua wanafunzi wanaotoka katika familia maskini zisizo na uwezo wa kuwanunulia watoto wao wa kike taulo za kike, ambao kwa kawaida huwa ni wachache. Kwa kutumia mwongozo wa ruzuku ya uendeshaji wa shule za sekondari wanaolekeza kutumia asilimia 10 ya ruzuku kwa ajili ya dawa na mahitaji maalum kwa wanafunzi wa kike, wawe na utaratibu wa kuwanunulia taulo hizo wanafunzi hao maalum kwa utaratibu utakaoratibiwa na Mkuu wa Shule husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge ni wale ambao waliomba maombi maalum yanayohusu Majimbo yao, hususan kwa upande wa sekta za elimu na maji tumeyachukua kwa ajili ya kuyafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara za sekta husika. Maombi hayo ni pamoja na usajili wa shule, kupandisha hadhi shule kuwa kidato cha tano na sita na wananchi kupatiwa huduma za maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi waliozungumzia ni kuhusu gharama ambazo hazimo katika fedha za elimu ya msingi bila malipo. Naomba kulihakikishia Bunge kuwa gharama za umeme na maji zimo ndani ya fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule. Suala la mahitaji ya walinzi wa shule, *matron and patron*, kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu na hata wale wa kike bado linafanyiwa uchambuzi wa kina ili hatimaye utekelezaji wake uwe mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo Waheshimiwa Wabunge ningependa kufafanua hapa ni changamoto za miradi ya maji katika maeneo yao. Napenda nikiri kwamba zimekuwepo changamoto kadhaa ambazo tumekuwa tukizitatua kwa kusaidiana na Wizara ya Maji. Miradi ya maji ni miradi ya miundombinu ambayo kabla ya utekelezaji lazima kujua chanzo cha maji, uwezo wa chanzo cha maji, aina ya mradi utakayotumika kama ni kuchota maji kwa mashine ya kuendeshwa kwa mkono au kuendeshwa kwa nguvu za nishati ya jua au kwa umeme au kwa mafuta au maji yanayotiririshwa kwa mteremko na

kadhalika. Hatua hii ni upembuzi yakinifu na hatua ya usanifu ndiyo huelekeza gharama zinazohitajika kutengeneza mradi. Tukishajua gharama za mradifi fedha hutengwa kwenye bajeti na hatimaye mchakato wa kuwapata Wakandarasi wa ujenzi na wasimamizi wao hufanyika ambao hatimaye Mamlaka za Serikali za Mitaa husaini nao mikataba ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ipo miradi ambayo fedha nyingi zimetumika, miundombinu isiyozingatia viwango vilivyomo kwenye usanifu imejengwa chini ya kiwango, ikiwemo iliyojengwa bila ya kuzingatia uwezo wa chanzo, wakati mwingine wamefukuzwa wakandarasi katikati ya utekelezaji na hivyo miradi kuachwa bila kutimiza lengo lake la kuwashudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zillizopo zinaonesha moja kwa moja sababu ni Mkandarasi asiyé na uwezo unaotakiwa ndiye aliyepewa mkataba. Kwa kuwa taratibu za kuingia mkataba na wakandarasi zinafahamika duniani kote, kwamba huwezi kuingia mkataba na Mkandarasi bila kwanza kumfania *due diligence* yaani upekuzi maalum ili kutathmini uwezo wake wa kutengeneza mradi kabla ya kusaini mkataba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kakunda, kengele ya pili imeshagonga, kwa hiyo, unga mkono hoja tuendelee.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwamba, tutaendelea kuwa wakali sana dhidi ya taratibu ambazo hazifuatwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamuita Mheshimiwa Waziri, niseme tu ni kwa sababu ya mazingira ya Mwalimu Magreth na jambo kubwa alilolifanya, otherwise Wabunge hamruhusiwi kuwaita

wageni, maana asije akasimama mtu akasema wageni wangu wale pale wasimame wasikilize swali ninalouliza.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, mtoha hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola)aliyetuwezesha, ambapo ilikuwa siku ya kwanza, ilikuwa asubuhi, ilikuwa jioni, tukakamilisha siku ya kwanza. Tukaenda hivyo mpaka leo tumefika ilikuwa asubuhi na itakuwa jioni siku ya sita na tutakamilisha jukumu letu tulilopewa katika Wizara hii kuwasilisha hoja hii mezani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu sana naomba nimshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, aliyenipa dhamana kubwa sana ya kusimamia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambayo ina watumishi takribani 388,000 sawa na watumishi asilimia 74.02 ya watumishi wote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Spika, nikushukuru wewe kwa kazi kubwa na Wenyeviti wa Kamati, pia niwashukuru sana viongozi wote wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI, ikiongozwa na mkubwa wangu Mheshimiwa Jasson Rweikiza na Mheshimiwa Mama Mwanne Mchemba, lakini wapiganaji wote wa Kamati hii walikuwa wametoa maelekezo ya kutosha mpaka na sisi tukapata umahiri wa kuweza kuwasilisha hoja hii hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa dhati ya moyo wangu niwashukuru Wabunge wote. Michango ilikuwa mizuri sana yenye afya ambayo kwa namna moja au nyingine inatuwezesha kama Wizara tuone nini tunapaswa kufanya katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru familia yangu kwa msaada mkubwa. Mkiona ninapendeza maana

yake nyuma kuna watu wanafanya shughuli hiyo, lakini niwashukuru watoto wangu wote, najua wengine saa hizi wako masomoni, Mungu awafanyile wepesi masomo yao yaende vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana, baba yangu amefariki, nimshukuru sana mama yangu mzazi kwa malezi mazuri. Siku zote amekuwa mama mlezi kwa kipindi chote, namshukuru sana mama yangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe. Mjadala huu unavyoendelea walikuwa wakiufuatilia japokuwa katika vipindi vya vipande vipande, wengine wakati mwingine wanakaa mpaka saa sita usiku, saa tano usiku, kuona mjadala jinsi gani unaendelea katika ofisi abayo nimepewa dhamana Mbunge wao kuweza kuvisimamia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ilikuwa ni hoja nzito, Wabunge waliochangia kwa kweli wamepatikana takribani 123. Kati ya hao Wabunge 71 walichangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na Wabunge takribani 52, wengine walikuwa wanaongezeka saa hizi kwa maandishi, hawa wamechangia kwa maandishi. Najua kwa mujibu wa mwongozo wa kanuni zako na suala zima la muda, naomba Wabunge wote mliochangia mridhie kwamba kumbukumbu yenu itaonekana katika *Hansard* za Bunge za Taarifa yetu hii ya Wabunge waliochangia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema ukweli hoja zimekuwa nyingi, lakini hoja hizi zote nazichukulia kwamba ni hoja zilizolenga kujenga mwenendo na utendaji mkubwa wa Wizara yetu. Hoja ya kwanza ambayo Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Rweikiza, mkubwa wangu na ninaomba Wabunge wengine wote mridhie, sitaki kuwataja Wabunge hapa kwa majina inawezekana mtu mwingine nikamuacha ikaja kuwa nongwa, kwa nini nimesema, lakini sijatajwa. Naomba wote tuliozungumza tubebwe na Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI. Akitajwa ye ye basi, chukulia na mimi nimetajwa katika hoja hiyo kwa sababu nilichangia

Bungeni. Maana naweza nikasema dada yangu Mheshimiwa Zainab Mndolwa hapo, wengine wakasema kwa nini umemtaja yule peke yake na mama Kauthar yupo hapa jukwaani ikawa nongwa hapa shughuli ikaanza kwa nini umemtaja yule peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja ambayo ilionekana Wabunge wengi wamechangia, Mwenyekiti wa Kamati alizungumzia ni suala zima la mapokezi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hoja hii ukiiangalia imetamalaki mahala mbalimbali, hata katika hoja za CAG katika vipindi tofauti ilikuwa ikielekeza jinsi gani fedha hazifiki katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kamati yetu ya Utawala Mheshimiwa Rweikiza amezungumza hapa kwamba ndiyo hoja ambayo hata katika Kamati walizungumza sana. Naomba nikiri wazi kwamba hoja hii ni ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ni-*appreciate* juhudhi kubwa za Serikali kwa sababu kwa ujumla wake kutoka Hazina kwa kipindi hiki cha sasa hivi katika mwaka wa fedha 2017/2018 mpaka tunapofika mwezi Februari tumeweza tumepokea takribani shilingi bilioni 231.33 sawa na asilimia 50 ya fedha za mengineyo. Hata hivyo, katika suala zima la maendeleo tulipokea jumla ya shilingi bilioni 914.39 sawa na asilimia 50 ya bajeti iliyokuwa *approved* ya mwaka wa fedha 2017/2018. Hata hivyo, ruzuku ya maendeleo inatolewa kulingana na ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika imani yangu kubwa kwamba kwa sababu bajeti iliyotolewa mpaka mwezi Februari mwaka huu tumefika asilimia 50, lakini hapa katikati tunatarajia kupokea pesa za ile miradi viporo ambayo ninyi Wabunge tuliwaita, Wenyevitii wa Halmashauri, Wakurugenzi na Maafisa Mipango. Hazina inafanya harakati nadhani kabla ya mwezi Juni tutapata baadhi ya *fundya* fedha imani yangu kubwa mwaka huu wa fedha kiwango cha fedha kilichopokelewa kitazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili naomba sana niwahimize wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, ninachoamini ni kwamba fedha zote zinatoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali, tunapaswa katika ile ajenda ya pamoja kama Taifa, kuhamasishana suala zima la watu wawewe kulipa kodi ambapo naamini kodi ikilipwa Mfuko Mkuu wa Serikali hautaona aibu kupeleka pesa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 tumetenga miradi mikakati. Ajenda yetu ni nini? Licha ya Halmashauri kutegemea fedha zile kutoka Serikali Kuu lakini miradi ya Halmashauri ibuni miradi ambayo itasaidia kuchagiza upatikanaji wa fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Katika hili niwasihi Wabunge wote katika Kamati zetu za Fedha kule katika Halmashauri zetu tusiwaonee aibu Maafisa Mipango, badala ya kubuni mipango wao wanakaa tu Maafisa Mipango haiwezekani. Halwezekani leo hii kuna Halmashauri zimepeleka miradi mikakati mpaka leo hii lakini kuna Maafisa Mipango wengine wamelala msikubali Waheshimiwa Wabunge katika Halmashauri zenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha imetengwa kwa lengo kubwa kuhakikisha kwamba tunapata watu mahiri kwa ajili kuhakikisha wanafanya *resource mobilization* tupate fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, jambo hili nina imani kwamba kama Taifa kwa pamoja tutaweza kufika mahala pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lilikuwa ni suala zima la *TARURA* bahati nzuri msaidizi wangu Mheshimiwa Kakunda amelizungumza hapa kwa kina, lakini kama tunavyofahamu ni kwamba hii ni taasisi mpya ambapo mtandao wa barabara kama nilivyosema awali tuna mtandao wa barabara takribani kilometra 145,000, lakini kilometra karibuni 108,000 zote zinasimamiwa na *TARURA* maana yake changamoto ni kubwa, lakini ukiangalia mgao wa bajeti ambayo tunaitegemea ni ile asilimia 30 kutoka *Road Fund*. Wabunge mlisema hapa kwamba ikiwezekana formula iweze kurekebishwa. Waziri Mkuu wakati anazindua *TARURA* mwezi Julai, 2017 alilizungumzia hili kwamba Serikali

ikae na jambo hili tunalifanyia kazi kama Serikali kwa pamoja kuona namna gani bora vipi baadaye, *TARURA* kiwe chombo kinachowenza kusimama kipate fedha kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaozalisha uchumi, kule maeneo ya vijijini ambao mazao na mifugo inakotoka waweze kusafirisha malighafi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Serikali tunaenda kulifanyia mpango mpana zaidi tuangalie ikiwezekana vyanzo vingine nya mapato, maana yake hata tukiitegemea mgawanyo huu hatuteweza kujibu shida za mitandao ya barabara ya kilometra 108,000.9. Ni lazima kama Wabunge wote endapo Serikali itakuja na mpango mkakati wa kutafuta fedha, kuhakikisha fedha hizi zinakuwa *ring fenced* kuenda kujibu matatizo ya barabara vijijini, naomba Wabunge wote tuungane na Serikali katika ajenda hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengine, nimesikia akina Mheshimiwa Lusinde walisema barabara zetu, madaraja yetu, kule Nzega kuna daraja kule la ndugu yangu Mheshimiwa Bashe maeneo yote ya nchi hii, ndugu yangu Mheshimiwa Lubeleje alizungumza barabara zake za Mtanana, tunayafahamu haya Wabunge wote naomba niwaambie. Ajenda yetu kubwa ni kuhakikisha tutabaini barabara zote, lakini tutaisimamia *TARURA* iweke *legacy* katika nchi hii ni taasisi inayofanya vizuri kuboresha miundombinu ya barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha ajenda ya *TARURA*, jambo lingine liliilojitokeza ni suala zima la uwekezaji wa elimu msingi bila malipo. Kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kila mwezi kuanzia mwezi Disemba, 2015, Serikali ilikuwa ikitoa bajeti ya fedha takribani shilingi bilioni 23 kwa ajili ya ku-services uuala zima la programu ya elimu bure. Hata hivyo mwaka jana tulikwama, Wabunge wengine ninyi mlisema humu ndani kwamba fedha zile hazitoshi. Tulimuomba Mheshimiwa Rais akasema tusubiri mwaka wa fedha umefika sasa, bahati nzuri mwaka huu tumepata

*additional* fedha karibuni 3.6 bilioni ambayo inaongezeka katika suala zima la elimu msingi bila malipo. Jambo hili litatupa nguvu kuhakikisha programu hii inaenda vizuri, kwa sababu nikijua wazi kwamba kuna wanafunzi ama watoto walioongezeka wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba nikiri kwamba jambo hili Watanzania naomba niwasih Wabunge tuache kubeza mambo mengine ambayo yana maslahi mapana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge wamesema mpango huu hauna maana yoyote, ndugu zangu naomba niseme kuna watoto wa maskini ambao walikuwa wanashindwa kabisa kupata elimu, tuone kwa nini mwaka 2016 Januari mara baada ya suala zima la elimu msingi bila malipo, kwa nini tuliweza kuwapokea mpaka watoto wenye umri wa miaka kumi wanataka kuja kuanza darasa la kwanza. (*Makof!*)

Kuna wakati mama mjane, baba amepotea, ana mtoto wake anataka kumpeleka shule lakini anaambiwa lete *uniform*, lete dawati, mchango wa shule wanashindwa, lakini baada ya elimu msingi bila malipo tumeona watu wengi wakiwatoa watoto waliowaficha, waliokuwa wakiwatwisha vikapu vyta vitumbua na karanga, sasa wamepelekwa shule. Kwa hiyo, jambo hili ni kubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nafahamu jambo lolote lenye mafanikio lina changamoto yake, changamoto ndio suala zima la ujenzi wa madarasa, madarasa yanakuwa pungufu, madawati na hali kadhalika walimu. Hata hivyo, naomba niwaambie Serikali haikulala, Serikali katika mwaka huu wa fedha tumeamua kuwekeza vyta kutosha. Inawezekana kuna bajeti zingine msizone katika vitabu hivi lakini naamini mtaviona katika mpango wa Serikali katika maeneo mbalimbali hasa vilevile katika suala zima la Wizara ya Elimu, ndiyo maana mwaka huu mnawenza mkaona tutakuwa tunafanya *arrangement* ya ndani ya Wizara kati yetu na Wizara ya Elimu, inawezekana watu wengine

wanahoji kwanini fedha nydingi za miundombinu hatuzioni TAMISEMI wakati ninyi ndiyo mnaojenga madarasa na vyoo vya shule za msingi Kamati ilisema, hili tunalifanyia kazi mtaona ujenzi wa madarasa, ujenzi wa vyoo, ujenzi wa nyumba za walimu jinsi gani Serikali imejipanga kwenda kujibu matatizo katika sekta ya elimu katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Bashe alizungumza hapa kwanini TAMISEMI inaonekana bajeti zake zote zimeenda katika *recurrent expenditure*. Kama nilivyosema, TAMISEMI ukiangalia bajeti ya mishahara *recurrent expenditure* yote ni ya nchi nzima mwaka huu ni trillioni 7.4; lakini bilioni 4.1 yote ni mishahara kwa watumishi waliopo chini ya ofisi ya Rais, TAMISEMI, hata katika bajeti *process obvious* utaona gharama hizi zinaongezeka kwa kiwango kikubwa kwa sababu bajeti peke yake katika ofisi hili inachukua asilimia 56 ya bajeti ya mishahara ya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata leo Wabunge mkisema kwamba walimu waongezewe mishahara, wauguzi waongezewe mishahara maana yake unaongeza *recurrent expenditure* kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni jambo jema, kwa hiyo msishangae ndugu zangu kwamba bajeti peke yake ni trillioni 1.8 ya *development budget out of* trillioni 6.58 ni kwa sababu ni kwamba watumishi wengi na *transaction* nydingi za kiutumishi ziko katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa mambo ambayo yalitamalaki sana ni suala zima la ujenzi wa miundombinu ya afya. Tumetoka mbali na hapa nilisema siku *nilipo-table* hotuba bajeti yangu, Tanzania tumetoka mbali ukiangalia hospitali za wilaya, vituo vya afya, zahanati changamoto ni kubwa, nilisema wazi tutafika kipindi ambacho nchi hii imeweka historia, Mheshimiwa Dkt. John Pombe ameweuka historia, ataweka historia kubwa ndani ya miaka hii mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii katika vituo vya afya, nenda Hospitali ya Amana, nenda Muhimbili, nenda kokote,

nenda hata hospitali ya Tabora pale mtani wangu siku ile juzi alivyokuwa anachangia hapa Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, idadi ya watu wamejazana ni kwa sababu hatuna *back up strategy* kule katika ngazi zetu za kata, hatuna vituo vya afya vyenye kufanya upasuaji ndiyo maana mama kama hitaji la upasuaji ni lazima aende katika *Referral Hospital*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli chini ya Serikali ya Awamu ya Tano ndiyo maana ajenda ya kwanza tumeanza kujenga vituo vya afya 208 kwa mara ya kwanza. Vituo hivi ni historia ambayo hajjawahi kuwekwa kipindi chochote cha nchi hii kuweza kuweka miundombinu, tena niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge nilisema tutapeleka fedha hizi kwa kutumia *force account* na Wabunge kweli mmesimamia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika watu wanaostahili heshima kubwa ni Wabunge ninyi mmeweka historia kusimamia fedha zile kwa *force account*. Shilingi milioni 500 kwa mwanzo ukizipeleka katika Halmashauri wakatumia Wakandarasi tu hakuna kitu, lakini tulielezana, tulikubaliana, mkaenda kusimamia, sasa mafanikio makubwa yamepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hiyo tu mwaka huu katika bajeti tumeamua kujielekeza katika suala zima la ujenzi wa hospitali za Wilaya. Hili lilikuwa ni tatizo kubwa sana Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama siku moja amekuja ofisini kwangu ametoka "jicho nyanya" anaomba Hospitali ya Wilaya kwake, anasema mimi Waziri mzima sina Hospitali ya Wilaya, sasa kawape salamu wale watani zangu wa Songea kwamba kule unaenda kujenga Hospitali ya Wilaya ya kwako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya nchi hii naomba nizitaje Hospitali ya Wilaya hizo kila mtu aweze kujifahamu. Tutajenga Hospitali za Wilaya 67 mwaka huu kwa maelekezo maalum na ramani maalum, wataalam wangu nimewatuma kazi hiyo, wakishirikiana na watu wa Wizara

ya Afya, Mkoa wa Arusha tukianza tunajenga Hospitali ya Wilaya ya Longido na Ngorongoro, katika Mkoa wa Dodoma tunajenga Hospitali ya Wilaya ya Chamwino, Bahi na Chemba, katika Mkoa wa Dar es Salaam tunajenga Wilaya ya Kigamboni na Wilaya ya Ilala kwa rafiki yangu pale Mheshimiwa Mwita Waitara pale Kivule tutaenda kujenga, katika Mkoa wa Geita tutaenda kuweka *Geita DC* na Nyang'hwale; Katika Mkoa wa Iringa tutajenga Mufindi, Kilolo pamoja na Iringa; katika Mkoa wa Kagera tunaenda kujenga *Kagera DC*, Karagwe na Kyerwa, Mkoa wa Kigoma tutaenda kujenga Uvinza, Buhigwe na Kasulu; Mkoa wa Katavi tutaenda kujenga Mlele, Mpimbwe na Mpanda; Mkoa wa Kilimanjaro tutaenda kujenga Siha na Rombo. Siha tunaenda kumalizia pale na Rombo kwa Mheshimiwa Joseph Selasini tunaenda kujenga; Mkoa wa Lindi tunaenda kujenga Ruangwa na *Lindi DC* kwa rafiki zangu hawa akina Mheshimiwa Bobali na mwenzake Mheshimiwa Dismas Bwanausi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Manyara tunaenda kujenga katika Wilaya ya *Mbulu DC* na Wilaya ya Simanjiro; Mkoa wa Mara tunaenda kujenga *Bunda DC*, Musoma na Rarya; Mkoa wa Mbeya tunaenda kujenga Busokelo, *Mbeya DC* na Mbarali; Mkoa wa Morogoro tunaenda kujenga Gairo, Morogoro na Malinyi; Mkoa wa Mtwara tunaenda kujenga *Mtwara DC*, Nanyamba pamoja na Masasi; Mkoa wa Mwanza tunaenda kujenga Buchosa pamoja na Ilemela; Mkoa wa Njombe tunaenda kujenga Wanging'ombe, *Njombe DC* pamoja na Makambako; Mkoa wa Pwani tunaenda kujenga Kibiti, *Kibaha DC* pamoja na *Kibaha TC*; katika Mkoa wa Rukwa tunaenda kujenga Nkasi, Sumbawanga na Kalambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Ruvuma tunaenda kujenga Nyasa, *Songea DC* pamoja na Namtumbo, Shinyanga tunaenda kujenga *Shinyanga DC*, Ushetu pamoja na Bariadi; Mkoa wa Simiyu tunaenda kujenga Itilima pamoja na Busega; Mkoa wa Singida tunaenda kujenga *Singida DC* tena tunaipeleka kule llong'ero ambapo watu walikuwa wanalilia sana muda wote pamoja na

*Mkalama DC; Mkoa wa Songwe tunaenda kujenga Ilaje DC pamoja na Songwe DC; Mkoa wa Tabora tunaenda kujenga Uyui pamoja na Sikonge. Mkoa wa Tanga tunaenda kujenga Korogwe, Tanga DC pamoja na Muheza. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tunaenda kutafuta fursa zingine katika baadhi ya maeneo kuhakikisha jinsi gani tutafanya tupate fedha zingine kama tulivyofanya katika vituo vya afya kuhakikisha tunaenda kuongeza Hospitali za Wilaya kwa kadri itakavyowezekana katika mwaka huu wa fedha. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili najua ndugu zangu wa Tanga pale Korogwe walikuwa wamepanga hospitali ile ijengwe Korogwe TC, lakini katika suala zima la *proper resource allocation* Hospitali ya Korogwe iko pale Mjini Korogwe DC, ikaonekana siyo vema twende tena tukawapelekee Korogwe TC pale pale. Kwa hiyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imefanya maamuzi hospitali tunaenda kujenga kwa Maji Marefu, wale wa Korogwe DC hospitali yao wataipeleka Korogwe TC kwa ajili ya wananchi waweze kupata huduma vizuri. Haya ndiyo mambo ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo mengine ni suala zima ni ajenda ya viwanda. Niwashukuru sana Wabunge kuna siku ambayo tumethubutu hapa. Mheshimiwa Rais ajenda yake ni kwamba jinsi gani tutafanya uwekezaji wa viwanda katika nchi yetu na ndiyo maana katika ofisi yetu tukaona kwamba tuna Wakuu wa Mikoa, tuna Wakuu wa Wilaya na Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Tutafanya vipi tuunge mkono ajenda hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliamua kutoa maelekezo kuwa Mikoa yote ijenge viwanda 100 katika kila Mkoa kwa mwaka mmoja. Bahati nzuri tarehe 20 Machi, Wakuu wa Mikoa tulikutana hapa Dodoma kufanya tathmini ya kwanza ndani ya miezi mitatu tumefanikiwa vipi katika jambo hili. Bahati nzuri ndani ya miezi mitatu tumejenga viwanda vidogo 1,285, ujenzi wa viwanda hivi ni sawa sawa na asilimia 49.4 ya utekelezaji wa lengo. Mimi naomba niwapongeze

Wabunge wote katika maeneo yenu, lakini niwapongeze Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana Maafisa Maendeleo ya Jamii tuliwaita hapa kwa ajili ya kuwapa *terms of reference*, nini wanapaswa kufanya katika suala zima la ujenzi wa viwanda, tumeanza kupata mafanikio makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi viwanda vidogo ndugu zangu ndivyo vinavyoajiri watu wetu kati ya wanne, watano mpaka 10. Viwanda 1,285 hata kiwanda kimoja kikiwa na wastani wa kiwango cha chini watu watano, unazungumza takribani watu karibuni 6,000 wamepata ajira ndani ya miezi hii mitatu. Haya ni mafanikio makubwa ambayo naomba Waheshimiwa Wabunge tuungane kwa pamoja katika suala zima la ajenda hii tutafanya vipi zaidi kuongeza ajira kwa vijana wetu na mwisho wa siku tutaenda kujenga uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika ofisi hii mambo ni mengi na jambo lingine ambalo liliitokeza ni suala zima ambalo Mheshimiwa Dunstan Kitandula alilizungumza hapa, kwamba ameona hotuba yote mwanzo mpaka mwisho haina habari ya mambo ya lishe. Tena anasema Mheshimiwa Selemani Jafo ulikuwa mionganoni mwa wapiganaji wa lishe! Naomba niwaambie *budget speech* maana yake inatoa *summary* ya baadhi ya mambo mengi huwezi uka-*capture* yote, lakini kuna majedwali, kuna vitabu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 katika bajeti ya mwaka huu tumetenga takribani shilingi bilioni 15 tumetoka shilingi bilioni 11 tumeenda shilingi bilioni 15 ambapo hii maana yake tunaenda kujibu, hata hivyo siyo kutenga fedha kwa mara ya kwanza kutokana na agizo la Makamu wa Rais tuliamua kuwasainisha mikataba Wakuu wa Mikoa wote nini wanapaswa kufanya katika suala zima la afya haswa suala la lishe, tunajua wazi leo hii

hatuwezi kupata watoto ambao wanasoma vizuri kama lishe yao itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema suala la udumavu, mtoto akipata udumavu katika siku 1,000 za kwanza, mtoto huyo hata akiwa mkubwa anakuwa poyoyo hawesi kuelewa hata mwalimu akimfundisha. Mwalimu akimwambia Juma sema 'a' na yeye anasema Juma sema 'a' haelewii lolote! Lazima tuwekeze katika suala zima la lishe. Hivyo, Mheshimiwa Kitandula na Wabunge wote naomba niwaeleze kwamba mwaka huu tumechanga sekta ya lishe shilingi billioni 15 ili kuhakikisha kwamba tunatengeneza kizazi kilicho imara kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watu wote wanaenda vizuri katika suala zima la lishe na kupambana na udumavu.

Jambo lingine lilikuwa suala zima la mifumo ya elektroniki, naomba nishukuru sana, mwanzo ukusanyaji wetu wa mapato ulikuwa na changamoto kubwa na ripoti ya CAG ilikuwa inazungumza wazi jinsi gani uvujifu wa mapato umekuwa ukiendelea kila siku, lakini hata hivyo tumejitahidi sana hivi sasa makusanyo ya mapato yote sasa tunatumia mifumo ya elektroniki, hata hivyo hatutegemei tena huko tunakokwenda baadaye watu kutumia vitabu vya risiti ya kawaida, lengo letu ni kuzisaidia hizi Halmashauri ziweze kukusanya mapato ya kutosha kwa lengo kubwa ni kwamba Halmashauri zetu zikiwa na nguvu kubwa ya kiuchumi zitawenza kufanya mambo sahihi mengi sana katika suala zima la kuendeleza maendeleo katika Wilaya zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lilikuwa suala zima la posho ya Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Jambo hili tumelichukua kama Serikali, ninafahamu wazi tulipokuwa katika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere pale Dar es Salaam Madiwani wote kupitia kwa Wenyeviti wao wa Halmashauri na Mameya walileta hoja hii na Mheshimiwa Rais alisema tumeichukua hoja hii, tunaweka vizuri mfumo wa kiuchumi wetu pale utakapokuwa vizuri basi tutaangalia jinsi gani jambo hili tuweze kulitendea wema kwa kadri itakavyofaa.

Kwa hiyo, hoja hii ni hoja ya msingi tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge, tumeipokea tutaeendelea kuweka miundombinu vizuri ya ukusanyaji wa mapato na kuangalia pale tutakapokuwa na hali nzuri tutaliwekeea utaratibu mzuri wa wananchi na hasa Madiwani wetu ambaa wanafanya kazi kubwa sana. Naomba nikiri wanafanya kazi kubwa iliyopitiliza tuweze kuangalia ile posho yao iweze kuongezeka ili waweze kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni suala zima la maeneo mapya ya utawala. Hoja hii imechangiwa na Wabunge wengi, tunesikia kwamba mtaa mmoja una watu karibu 20,000, kule Mondole na Msongola tunesikia hilo akina Mheshimiwa Malembeka wakilalamika, naomba tulichukue jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uwezeshejai wa mamlaka mpya na hasa katika sehemu zile za wilaya; kwa mfano kaka yangu Mheshimiwa Malocha alizungumzia sana jimbo lake, maana Jimbo lake lipo kama mbalamwezi, ana changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuseme tumeyachukua haya, lakini tutaangalia utaratibu wa kufanya, kwa sababu lengo letu kubwa kama Serikali kwa sasa ni kujikita katika maeneo mapya tulioanzisha lazima kwanza tuyaboreshe, hili ndilo jambo la kwanza. Kama kuna zile *special cases* kiserikali tutaangalia nini cha kufanya ili kuweza kujibu matatizo ya wananchi. Lakini kipaumbele cha kwanza sasa tulichokiweka ni suala la kutatua matatizo ya zile Halmashauri na wilaya mpya kama kule Tanganyika, tulizozianzisha; lazima zisimame vizuri kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lilikuwa linahusu utawala bora. Watu walizungumza kwamba kuna wakati mwininge watu wanatumia vibaya madaraka yao. Sheria ipo ndiyo , ya kumuweka mtu kizuizini, lakini viongozi wanatumia madaraka yao vibaya. Kama nilivyosema, ni kwamba sisi tumeendelea kutoa mafunzo awamu kwa awamu. Hivi sasa nilisema wazi kwamba yale ni mafunzo ya

utawala tuliyoyamaliza kwa Wakurugenzi pamoja na Wakuu wa Wilaya; na hapa katikati tutatoa tena mafunzo kwa Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ninyi Waheshimiwa Wabunge mnafahamu; hata humu ndani ya Bunge kwamba tabia hatufanani hata siku moja, ndio tabia ya binadamu. Kwa hiyo, kuna vitu vingine vinaweza vikarekebishika lakini vingine ni mambo ya kibinadamu. Hata hivyo jukumu kubwa la ofisi yetu ni kuhakikisha kwamba tunasimamia utaratibu. Tumesikia Waheshimiwa Wabunge, tutalisimimamia jambo hili na hasa maeneo mbalimbali yenye changamoto kubwa tutayaweka sawa ili yaweze kwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine hata wiki hii iliyopita nimeweza kuyatolea maelekezo, kwamba kuna baadhi ya mambo yalikuwa yamesimama, nimetoa maelekezo yale mambo ndani ya siku 14 yaanze kufanya kazi zake ili kwamba tuhakikishe utawala bora unafanya kazi yake. Nilitoa maelekezo kule Tunduma kwa Mkuu wetu wa Mkoa, na nina imani mambo yale yatakwenda vizuri na muda si mrefu ile migogoro yetu itakuwa imeisha na tutahakikisha tunawatumikia wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kuna hoja nyiningine ilikuwa inahusu miradi ya *TSP*, *ULGSP*, kwamba kwa nini miradi 18 peke yake, kwa nini miji minane peke yake, naona pale kaka yangu wa Kasulu, Mheshimiwa Nsanzugwanko juzi amenitumia *ki-note* anasema namuona Mheshimiwa Zitto mwenzangu barabara zake zinajengwa, mimi kwangu choka mbaya kwa nini na mimi ni halmashauri ya mji. Ni kwamba tulianza na miji 18 ile ambayo nimesema kuna Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza na miji mingineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua, kama nilivyosema tumetengeneza barabara za kisasa na tunaendelea kutengeneza na mwaka 2020 tutamaliza miradi hii. Miradi ya halmashauri ya miji pamoja na Manispaa zipatazo 18 ujenzi ndio unaendelea hivi sasa. Hata hivyo hii

kazi inafanyika kwa awamu. Kuna miji ambayo imesahaulika ambayo imeingizwa katika programu hii inayokuja kuna Mji wa Nzega, *Mbulu TC* na Kasulu, wataalam wetu wako mbioni wanaifanya taratibu, itakapoiva tu jambo lile litakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kwamba halmashauri za miji zote ziwe katika ubora ule tunaoukusudia. Hata hivyo, kuna jambo lingine mahususi ambalo hata leo hii asubuhi watu wamelitolea mwongozo suala la eneo la Jangwani. Nimezungumza katika Mradi wa *DMDP* ajenda yake kubwa mionganoni mwa yakufanya ni kwamba licha ya ujenzi wa barabara za kisasa, ujenzi wa masoko na sehemu za kupumzikia lakini ajenda yetu kubwa tumetenga takribani dola milioni 20 kwa ajili ya kuhakikisha tunalishughulikia Bonde la Msimbazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ndugu zangu mambo haya ya majanga huwezi kuyazuia. Mheshimiwa Naibu Spika, hata nchi zilizoendelea, angalieni leo kule Marekani wakati mwingine California utakuta maji yamefurika mitaani, hali ni mbaya na wananchi wako katika hali mbaya. Hili jambo si Tanzania peke yake, inapoteokea matatizo haya ya majanga wakati mwingine hayajalishi ukubwa wala uchumi wa nchi, hayachagui. Jana tulikuwa tunaangalia kule Arusha hali ilikuwa mbaya kweli kweli katika baadhi ya maeneo, maeneo mengine yanasonombwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuseme, kwamba kama Serikali kwa bahati nzuri tumeliweka kwenye mkakati, tumejipanga kutumia dola milioni 20. Pia kwa bahati nzuri hapa na Mheshimiwa Zungu kaka yangu vilevile ameniletea andiko la mpango mkakati ili kama ikiwezekana Serikali tuangalie *option*; nini tufanye katika Bonde la Msimbazi na eneo la Kariakoo. Jambo hili pia lote tunalichukua kwa pamoja. Nia yetu kama Serikali ni kuangalia ile njia sahihi na nzuri ili hatimaye tuweze kujibu matatizo ya Watanzania katika maeneo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba niseme kwamba kuna suala ambalo limezungumzwa na manaibu

wangu wamelitolea ufanuzi, suala la walimu wa kuhamishwa kutoka sekondari kwenda shule ya msingi; limeleta mkanganyiko mwingi sana. Nafahamu jambo lolote likiwa geni/jipya lina changamoto yake kubwa. Hata hivyo tufahamu kwamba lengo la Serikali ni kuwapa huduma wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi ya wilaya leo hii zilikuwa na walimu wa sanaa na walimu wa *arts*, mwalimu wa *arts* tunatarajia kwamba mwalimu awe na vipindi visivyopungua 20 kwa wiki, lakini imefika wakati mwingine kuna mwalimu mwingine wa kiingereza au kiswahili wiki nzima ana kipindi kimoja tu. Akiingia saa nne asubuhi leo Jumatatu mpaka wiki ijayo saa nne asubuhi ndio anaingia darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia mionganoni mwa maeneo ambayo tuna changamoto kubwa ni suala la masomo ya kiingereza. Leo hii nenda katika shule zetu mtafute mwalimu wa kiingereza mwambie akupigie ung'eng'e wake wa kiingereza, msikilize vizuri. Tuna walimu wengi lugha vilevile wako huku sekondari ambao hawakuwa na vipindi. Jambo la kuwachukua na kuwapeleka katika shule za msingi si baya. Hata hivyo Waheshimiwa Wabunge hoja yenu mliyozungumza, suala la *induction course*, hili ni jambo mahususi na zuri, tunaomba tulichukue kwa ajili ya kulifanyia kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafahamu walimu hao kweli kwa sarakasi tulizokuwa tunapiga huko sekondari na huku unajua kuna elimu, kunaitwa "*mlamwa luwaza*" kuna mambo ya uchopekaji, kuna lugha nyingi zinatumika. Kwa hiyo huyu mwalimu wa sekondari lazima akajifunze kuchopeka huko shule ya msingi anachopeka vipi. Jamani kuchopeka inaita *intergration* katika lugha nyingine. Sasa kuna lugha inafundisha uchopekaji wa masomo, kwa hiyo, lazima hawa walimu, mlivyosema hoja yenu kwamba ikiwezekana wapate *induction course*, jambo hili kama Serikali tunalichukua kwa ajili ya uboreshaji kwa sababu

tunajua ufanisi wao wa kazi utatokana na suala zima lilivyo.  
*(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la malipo, tumepeleka sasa hivi takribani bilioni arobaini. Katika bilioni 40; asilimia 20 ni kwa ajili ya kuwagawanya walimu; asilimia 20 maana yake tunazungumza wastani wa shilingi bilioni nane. Bilioni nane, imani yangu kubwa, Waheshimiwa Wabunge nimewasikia. Kuna wale walimu ambao tumewahamisha na wanastahili kulipwa. Ninaamini katika Halmashauri nydingine hakuna tatizo, ila kuna baadhi ya Halmashauri kweli ninakiri inawezekana matatizo yapo. Tutaweza kushughulikia *case by case* kutokana na halmashauri ambazo hazikufanya vizuri. Lakini nina amini Halmashauri zingine watu wamefanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tutawaangalia wale wakurugenzi ambao tumepeleka fedha katika halmashauri yake kwa ajili ya walimu wale wanapohamishwa, kwa nini amezizua, hazikuweza kufanya kazi hiyo; tutashughulika nao. Kwa sababu haiwezekani, tumetoa maelekezo watu wapo maofisini wanashindwa kutekeleza maeleo haya. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge jambo hili kama Serikali sisi tumelichukua kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaboresha katika maeneo mbalimbali ya utendaji wetu wa kazi. *(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya TAMISEMI yapo mengi na ndiyo maana nikiangalia hapa kila jambo ninalolitazama naona tamu, linataka ultolee maelekezo, lakini hatuwezi kuyamaliza yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi naomba niseme wazi kwamba kuna miradi mingi sana imetengwa katika mamlaka ya Serikali za Mitaa na jukumu letu kubwa ni kuhakikisha kwamba bajeti hii ambayo mimi nitaomba Wabunge wote mridhie ipite na ipite kwa sababu ndiyo bajeti ya mishahara ya watu wetu wote. Walimu takribani 300,000 na watumishi wengine 388,000; asilimia 74.6 leo unashika shilingi unataka kuondoa shilingi, unataka kumnyima

mwalimu mshahara wake? Kwa hiyo mimi nina amini wote tutakuwa katika agenda moja ya kuhakikisha hii bajeti inapita vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba nikiri kwamba hoja zote za Waheshimiwa Wabunge sisi tumezipokea na zingine zitakuja kwa ufanuzi mbalimbali wa kimaandishi na hoja hizi lengo letu kubwa si kuzisikia na kutoa maandishi, ni kwa ajili ya kwenda kujipanga kuyatekeleza. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuititia timu yangu mahiri iliyopo hapa kuna Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege tutahakikisha mwaka 2018/2019 tunakuja kuwatumikia katika majimbo na mikao yenu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaongeza kasi yetu ya utendaji wa kazi na tutakuja kubainisha changamoto mbalimbali zinazobainika katika maeneo yetu, lengo letu kubwa ni kwamba lazima tuwatumikie wananchi katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, mnajua kuna baadhi kuna mapungufu baadhi mengine yapo, hayo vilevile tutayasimamia kwa karibu zaidi. Ajenda kubwa ni kuhakikisha kwamba kila mtu katika eneo lake anaweza kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi naomba niwasih wahehsimiwa Wabunge, naomba tupendane sote kwa pamoja; tukipendana tukiwa na upendo bila kujalisha mipaka ya aina yoyote tutaweza kupata mafanikio makubwa kwa sababu bajeti tunayojadili leo ni bajeti inayohusu mustakabali wa nchi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa zote. Kwa hiyo, nawasihi sana upendo kwetu ndio litakuwa jambo la msingi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ridhaa yako, kabla sijahitimisha hoja yangum naomba kutoa hoja maalum, kwamba katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imetengewa shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Halmashauri. Kwa kuwa Halmashauri ya Handeni inapaswa kuhama na kujenga Ofisi katika Kata ya Kabuku, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaliomba

Bunge lako tukufu liridhie mabadiliko ya bajeti yaliyotengwa kwa ajili ya kujenga Ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ihamishwe kwa ajili ya kujengea Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. Halmashauri ya Mji wa Handeni itachukua majengo ya Ofisi zitakazoachwa na Halmashauri ya Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja llitolewa lamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, na tutaendelea na utaratibu wetu. Nimwite sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais. Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kutoa maelezo yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge letu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na kuhitimisha hoja za Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake yanayoniwezesha kutekeleza majukumu ya kusimamia menejimenti ya utumishi wa umma na utawala bora, eneo ambalo ni mtambuka katika utawala wa nchi na utendeshaji wa shughuli za Serikali. Napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa maelekezo na ushauri wao ambao unatuwezesha kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Bunge,

Katibu wa Bunge na uongozi wote wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa mnaopatia Ofisi yetu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu ziwaendee viongozi na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa maoni na ushauri waliooutoa ambaao umesaidia katika utekelezaji wa majukumu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa awamu zilizotangulia, Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kuheshimu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kutekeleza sera na mipango ya taifa kwa muda mrefu iliyobuniwa kuwaondolea wananchi umaskini na kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa sera, mikakati na mipango hii unahitajika watumishi wa umma wenye weledi, uadilifu, uchapakazi na umakini kwa kuwa utumishi wa umma ni nguzo muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Ikumbukwe kuwa kila taasisi ya umma imejengwa na watumishi wa umma, na bajeti zilizoombwa leo hapa zitakazopitishwa, wizara zote utekelezaji wake kwa kiwango kikubwa unategemea watumishi wa umma ambaye mimi ndio Waziri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuendelea kuiboresha sekta ya utumishi wa umma, kuhimiza misingi ya weledi (*professionalism*), kuweka mifumo ya menejimenti inayowezesha watumishi kuwajibika na kuwa na maadili ili watoe huduma kwa wananchi na wadau wengine kwa kufanya kazi kwa ufanisi, bidii na kuzingatia matokeo na hivyo kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utumishi wa umma lazima uongozwe na kusimamiwa ili kuhakikisha kuwa unaboreshwu kulingana na mahitaji ya wananchi bila kuathiri misingi yake. Ili kulinda misingi Serikali imekuwa ikifanya mabadiliko katika

usimamizi wa utumishi wa umma mara kwa mara ili kuendana na misingi niliyoieleza hapo awali. Kama ilivyo kwa awamu zilizotangulia, Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuuboresha utumishi wa umma ili uendelee kuwa na manufaa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kwa Serikali ya Awamu ya Tano, hatua mahususi za kusimamia sera na mifumo ya menejimenti, matumizi ya teknolojia na habari na mawasiliano, nidhamu, mapambano dhidi ya rushwa, uadilifu na uwajibikaji imeendelea kuchukuliwa. Tunaamini kuwa kwa kuzingatia mambo haya watumishi wa umma watafanya kazi kwa weledi na bidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia Wizara yangu; Wabunge 74 wamechangia hotuba yangu kwa kuzungumza hapa ndani ya ukumbi wa Bunge na Wabunge 17 walichangia kwa maandishi. Wabunge hawa wakiongozwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Mcemba wametoa michango na ushauri ambao tutauzingatia wakati wa kutekeleza majukumu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyoona hii ni idadi kubwa ya Wabunge waliochangia, napenda kuwashukuru sana, muda ungetosha ningewataja mmoja mmoja, lakini kwa sababu ya muda naomba wanisamehe. Napenda kuwashukuru sana na kuwaahidi kuwa maelezo kwa kila hoja iliyotolewa yatapatikana kabla ya mkutano huu wa Bunge kumalizika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja katika Wizara yangu zilijikita katika maeneo mahusisi yafuatayo, yaani yale yaliyozungumza kama unataka kufanya majumuisho mengi yamegusia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza upungufu wa watumishi hasa katika sekta ya afya na elimu ambayo imechangiwa na Wabunge 39, upandishwaji vyeo iliyozungumzwa na Wabunge wengi, watumishi kukaimu nafasi na madaraka kwa muda mrefu kama ilivyojitezea kwenye maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, umuhimu wa kuboresha maslahi ya watumishi ambapo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa imelitolea maoni na ushauri. Aidha Wabunge wawili nao wamelizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mapambano dhidi ya rushwa, masuala ya utawala bora ikiwemo wasiwasi na usalama wa wananchi wetu na shughuli za Idara ya Usalama wa Taifa, suala ambalo lilichangiwa na Wabunge 17 na leo nitalitolea ufanuzi; vita dhidi ya umaskini kama ilivyojitezea katika maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na michango ya Wabunge waliochangia kuhusu shughuli za *TASAF*, *MKURABITA* na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majina ya Waheshimiwa Wabunge wote kama nilivyosema yaingie kwenye hansard kwa kumbukumbu sahihi za shughuli za bajeti za Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, masuala haya ni sehemu kubwa ya ajenda ya Serikali ya Awamu ya Tano kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020 na napenda kuchukua nafasi hii kuyazungumza kwa kifupi hasa kwa kuwa muda hautoshi kujibu hoja zote kama zilivyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nitajitahidi kujibu hoja kwa kadri muda utakavyoruhusu, na naomba nianze na suala la ajira katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na rasilimali ya kutosha na yenye weledi katika kutekeleza majukumu yake kulingana na vipaumbele vyake. Hata hivyo, ajira katika utumishi wa umma hutegemea

uwezo wa bajeti ya Serikali, pale bajeti inaporuhusu Serikali imekuwa ikitoa nafasi za ajira. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga nafasi za ajira 49,356 ikiwemo nafasi 16,000 za walimu wa shule za msingi na sekondari, nafasi 15,000 kada ya afya na kada nyngine za kilimo, uvuvi, mifugo, vyombo vya ulinzi, magereza, uhamiaji na nafasi 15,245 kwa ajili ya kada nynginezo wakiwemo Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata, Wahasibu, Wahadhiri wa Vyuo Vikuu, Maafisa Tarafa, Maafisa TEHAMA, Ugavi, Utawala na Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili lilidochangiwa na Wabunge wengi ni lile la upandishwaji vyeo. Kama ilivyo kwa ajira, upandishwaji vyeo na uteuzi hutegemea sifa za muundo na utendaji mzuri, bajeti ya kugharamia mishahara na kulinda tange kwa kada husika ili kuwepo uwiano wa utendaji wa wasimamizi mahali pa kazi. Kutokana na misingi hii katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga nafasi 162,221 za kuwapandisha vyeo watumishi wenyе sifa stahiki katika kada mbalimbali. Katika nafasi hizi, nafasi 2,044 zimetengwa kwa ajili ya kujaza mapengo mbalimbali ya vyeo vya uteuzi katika ngazi ya madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi huu katika nafasi ya madaraka utapunguza kero ya kukaimu nafasi hizo kwa muda mrefu kama ilivyobainishwa na Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia hoja yangu. Kutokana na kutolewa fursa hii, natoa rai kwa mamlaka za ajira na mamlaka nyngine zinazohusika, kuhakikisha kuwa zinaanzisha michakato hiyo mapema na kwa kuzingatia vigezo vilivyobainishwa katika miongozo mbalimbali iliyotolewa inayohusu uteuzi wa watumishi kushika madaraka. Pale ambapo hakuna watumishi wanaokidhi vigezo hivyo, waajiri wasisite kuomba kuhamishiwa watumishi wenyе sifa stahiki kutoka maeneo mengine katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nyongeza ya mishahara nalo limezungumzwa na wachangiaji wengi, suala hilo nalo ni la kibajeti na limeangaliwa kwa mapana yake.

Kutokana na umuhimu, Serikali inakusudia kutoa nyongeza ya mwaka kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine liliolzungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusiana na mapambano dhidi ta rushwa. Napenda kulihakikisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha uadilifu, kuhakikisha viongozi na watumishi wa umma wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia viapo nya uadilifu na kuwajibika kwa matokeo ya kazi na maamuzi yao ili kuondokana na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hizi, Serikali itaendelea kuiwezesha TAKUKURU kutekeleza majukumu yake kwa kuwajengea uwezo watumishi wake, hasa katika maeneo ya uchunguzi, uendeshaji kesi za rushwa na ufisadi na kujenga ofisi hatua kwa hatua katika Wilaya mpya ambazo hazina ofisi za taasisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maadili ya viongozi, Serikali itaendelea kujenga mifumo mbalimbali ya taratibu za kazi zinazoendana na mabadiliko ya teknolojia kwa kuwa ndio msingi mkuu wa uboreshaji wa utawala bora. Tutaendelea kuimarisha mfumo wa kufuatilia tabia na mienendo ya viongozi wa umma kwa njia ya kisasa zaidi ili wawze kujiepusha na vitendo vizivyo nya kimaadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa viongozi wote kuwa mienendo bora ya uzalendo na hali ya juu kwa kuwa maendeleo yanatokana na mwelekeo bora wa viongozi. Viongozi wajenge tabia ya kujiliza katika kila jambo kuwa wayafanyayo hayaleti mgongano wa maslahi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge waliochangia walionesha wasiwasi kuhusu usalama wetu na shughuli za Idara ya Usalama wa Taifa. Idara hii hutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Taifa Namba 15 ya mwaka 1996. Kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha sheria hii, majukumu ya msingi yaliyoainishwa ni kukusanya taarifa,

kuchambua na kuishauri Serikali ipasavyo juu ya hatua za kuchukua ikiwemo usimamizi wa rasilimali za nchi. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 5(a) Idara hii haihusiki na usimamizi wa sheria (*law enforcement*) kwa kuwa kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu, mionganoni mwa vyombo vyaa ulinzi na usalama jukumu hili ni la mamlaka nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba nichukue nafasi hii kufafanua Sheria ya Usalama wa Taifa inasema nini. Usipojua kazi za Idara ya Usalama wa Taifa utawapa lawama kwa shughuli ambazo si zao. Nataka kurejea sheria inasema nini, kifungu cha 5(1)(a), nataka kusoma kwa kiingereza halafu ntaleaza maana yake nini kwa kiswahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ya Usalama wa Taifa kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Bunge hili inasema hivi; *"To obtain, correlate, and evaluate intelligence relevant to security, and to communicate any such intelligence to the Minister and to persons whom, and in the manner which, the Director-General considers it to be in the interests of security."*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo kazi kubwa ya chombo cha usalama nchi yoyote ile; kukusanya habari na kuishauri Serikali iliyopo madarakani. Sasa yale mnayosema wanatukamata ovyo, wanafanya hivi, nataka niseme mafungu mengine mawili sheria inasema nini. Namba mbili inasema; *"It shall not be a function of the Service,"* haitakuwa shughuli ya Idara kufanya mambo yafuatayo, moja; *"To enforce measures for security,"* (haitatumia mabavu kumkamata mtu ili ku-enforce security), sheria ndivyo inavyosema. Pili, nilikuwa nawasikiliza muda wenu basin a mimi mnisikilize. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili inasema haitakuwa kazi ya Idara ya Usalama, kwa kiingereza; *"to institute surveillance of any person or category of persons by reason only of his or their involvement in lawful protest, or dissent in respect of any matter affecting the Constitution, the laws or the Government of Tanzania"* (haitakuwa kazi ya Idara ya

Usalama kufuatilia mhalifu, haitakuwa kazi ya Idara ya Usalama).

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niiseme hiyo kwa sababu mazungumzo mengi yaliyozungumzwa hapa yameelekezwa huko. Mtu ameuawa *it is a police case*, mtu amepotea *it is a police case*, hakuna nchi ambayo Idara ya Usalama inashughulika kukamata wahalifu. Inawezekana mnatumia hayo kujenga hoja zenu, lakini sheria ndivyo inavyosema. Kama mnataka wawe wanafanya hayo mnayoyataka leteni sheria hapa mbadilishe watafanya. Mimi mtumishi wa Bwana nitatenda kama Bwana anavyotaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii hutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria ya Usalama kama nilivyosema. Kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha sheria hii majukumu ya msingi yaliyoainishwa ni kukusanya taarifa, kuchambua na kuishauri Serikali ipasavyo juu ya hatua za kuchukua ikiwemo usimamizi na rasilimali za nchi. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 5(2)(a) Idara hii haihusiki na usimamizi wa sheria (*law enforcement*) kwa kuwa kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu mionganoni mwa vyombo vya ulinzi na usalama jukumu hilo ni la mamlaka nyine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mgawanyo huu si sahihi kuihusisha Idara hii na matukio ya uhalifu yanayotokea kwa nyakati tofauti. Aidha, uhalifu kama huu hauikumbi Tanzania peke yake bali upo katika mataifa mengine na uchunguzi wake huchukua muda. Ipo mifano hai inayodhihirisha ugumu katika kubainisha wahalifu kwa kuwa wao hutumia mbinu mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka jinsi Serikali ilivyokabiliana na uhalifu kama huo katika Wilaya ya Rufiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuiunga mkono Serikali katika mapambano dhidi ya uhalifu wa aina yoyote na wajiepushere kutoa matamko yanayoweza kuchochea uvunjifu wa amani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi yetu inazo programu mahususi zinazochangia jitihada za Serikali katika kupambana na umaskini. Programu hizi hutekelezwa kuititia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), Programu ya Kurasimisha Rasilimali za Wanyonge (*MKURABITA*) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Serikali itaendelea kutekeleza programu hizi ili kupunguza kiwango cha umaskini nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini ili kuhakikisha kuwa wanaonufaika ni wale tu wanaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza maelezo hayo kwa utangulizi, ninaomba sasa kuititia hoja sitozipitia zote ambazo zimejitokeza katika mjadala wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wamesema kuna ukiukwaji wa misingi ya utawala bora kwa kutumia macho, vitendo vya mauaji, utekaji nyara, kupigwa watu na upendeleo mwangi. Hapa majibu tunasema Serikali haiungi mkono vitendo vyote vya ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na ndiyo maana kila vitendo hivi vinapojitokeza Serikali huchukua hatua mara moja kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika hivyo, Serikali inaomba wanasiasia na wananchi kwa ujumla kuunga mkono hatua za Serikali zinazochukuliwa katika Jeshi la Polisi lenye dhamana ya usalama wa raia. Jeshi lenye dhamana ya usalama wa raia ni Jeshi la Polisi, si Idara ya Usalama. Hata hivyo, ni jukumu la kila raia kutoa taarifa sahihi kwa Jeshi la Polisi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kumekuwepo na ukiukwaji mkubwa wa sheria za nchi na Katiba ya nchi, mfano kuzuia mikutano ya hadhara, kukosekana kwa uhuru wa mawazo, wanaokosoa Serikali au kuishauri wanapata misukosuko na wengine wanapoteza, watumishi wa kiroho kupata misukosuko baada ya kudai kuwepo kwa Katiba Mpya au Serikali kukosolewa kwa maslahi, magazeti kufungiwa na waandishi kutozwa faini kwa sababu ya kutoa taarifa zisizopendeza Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hapa napenda kujibu hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kuwa Serikali inakiuka sheria ya nchi na Katiba katika kutekeleza majukumu yake. Mtu yeote au taasisi inayoona inanyimwa haki ya kisheria na Kikatiba ina nafasi ya kupeleka malalamiko yake kwenye vyombo vinavyotoa haki ambayo ni mahakama. Aidha, pamoja na uhuru huo kuwepo, ufanyike kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magazeti kufungiwa, hufanyika kwa mujibu wa sheria zilizopitishwa na Bunge. Tena Sheria ya Magazeti ilikuwepo ya mwaka 1976 tukailalamikia, Bunge hili limepitisha Sheria ya Magazeti, ndani ya Sheria ile ya Magazeti kuna chombo kinaitwa *Content Committee* ya senior citizens, kazi yao wao ni kufuatilia vyombo vya habari, yule ambaye amekwenda kinyume na maadili anaadhibiwa. Wale watu wameadhibiwa na *Content Committee*, Waziri anashauriwa na *Content Committee*, anapofunga Waziri anafungia kwa mujibu wa sheria na waliomshauri wamo ndani ya Sheria ya Vyombo vya Habari iliyopitishwa na Bunge hili linaloendelea leo hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la watumishi wa kiroho kupata misukosuko, Serikali haina ushahidi wa jambo hilo; na mimi nasema suala la watumishi wa kiroho ningependa sana nilichangie lakini sitaki kuchangia, ila niseme tu kifupi; ukitaka kumshauri mzee wako huitishi mkutano wa hadhara ukasema ninamshauri baba, hakuna njia ya kumfikia huyo baba yako kimya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la watumishi wa kiroho kupata misukosuko, Jeshi la Polisi linafanya uchunguzi wa uhalifu wowote bila kujali umefanywa na nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumzwa sana, ni sheria ipi inayowapa mamlaka Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwaweka watu ndani saa 24

na ni hatua zippi zimechukuliwa na Wakuu wa Mikoa na Wilaya inapobainika kwamba wananchi wamewekwa ndani kimakosa na hili nataka nilieleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wamepewa mamlaka ya kisheria, *Regional Administration Actya* mwaka 1997 (Sheria ya Tawala za Mikoa mwaka 1997) imewapa madaraka kumuweka mtu yejote ndani anayebainika kutenda kosa lolote lenye kuhatarisha amani na utulivu wa jamii husika. Anayeona hakutendewa haki, kwamba hakuwekwa kwa misingi hiyo ana ruhusa ya kulalamika kwa wakubwa wake wa kazi, hakuridhika, ruhusa kwenda mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa kuwa Mkao wa Kigoma umekuwa ukitoa malalamiko yake kwa Serikali na yamekuwa yanapauzwa, hususani kupotea kwa Diwani na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibondo bila maelezo yoyote, wananchi watajichukulia hatua na kufanya wanavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani ndugu yangu Mheshimiwa Zitto pale ulikuwa unatuhimiza tu kwamba jambo hili tulifanyie kazi, lakini ninavyomuelewa Mheshimiwa Zitto alivyo msomi, kijana, anaipenda nchi, ana akili, simuoni Mheshimiwa Zitto anahamasisha watu kuchukua sheria mkononi, yale maeneo aliyaweka tu kutuhimiza watu wa Serikali kwamba *please take action. Point noted,* tumeipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yake, majibu yake; Serikali haipuuzi malalamiko ya upotevu wa watu nchini ikiwemo Diwani na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibondo kama anavyodai Mheshimiwa Mbunge. Suala la kupotea kwa Diwani huyo lilisharipotiwa katika Jeshi la Polisi na uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tena hapa mimi nataka nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Zitto, huyu Diwani anayemtetea tumtafute mpaka tumpate, wala sio wa

chama chake *ACT*, ni Diwani wa CCM, inaonesha jinsi alivyo mzalendo anavyopenda haki itendeke kwa kila mtu, sasa uendelee hivyo hivyo mdogo wangu Mheshimiwa Zitto, usiyumbe katika mengine, endelea hivyo hivyo. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasisitiza mwananchi mwenye taarifa kuhusu jambo hilli ajitokeze kusaidia polisi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Kama nilivyosema mwanzo, *this is another police case*, kesi nyngine ya polisi, si ya vyombo, kesi nyngine ya polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Selasini; kuna mwandishi wa habari aitwaye Cyprian Musiba amekuwa akitoa matamko hatarishi katika vyombo vy ya habari yakiwemo na magazeti anayoyafanyia kazi lakini Serikali ikiwemo na Idara ya Usalama wa Taifa imekaa kimya na hajatoa tamko lolote la kubeza, hivyo wananchi waelewe viyi kama matishio hayo yana kibali cha Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Selani, nataka nikueleze kuwa sheria iliyotungwa na Bunge hilli inataka Idara ya Usalama wa Taifa ifanye kazi zake kwa faragha. Kwa hiyo, hii hoja uliyoitoa kwamba hata Idara ya Usalama wa Taifa imekaa kimya, nilishawahi kueleza humu ndani siku moja, hautawahi kusikia hata siku moja taarifa imetolewa na Msemaji wa Idara ya Usalama wa Taifa. Kwa hiyo, suala la wao kuwaita watu na kusema jamani sisi tumeishauri Serikali hivi, huyu bwana tumemchukulia hatua hii, si kazi yao, kazi yao ni kukusanya habari, kuishauri Serikali, wamemaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria ya nchi Jeshi la Polisi ndilo linalopewa dhamana ya kufanya uchunguzi matamko yote yenye kuhatarisha usalama wa raia na ambayo ni makosa ya jinai na pale inapojiridhisha huwapeleka wahusika mahakamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Idara ya Usalama wa Taifa kukaa kimya ni utekelezaji wa sheria, kama

nilivyosema, wanafanya kazi yao kwa faragha. Hujawahi kuwasikia na hutawasikia wanaita *press conference*. Hata hivyo, mtu ye yote ambaye ataona ameathiriwa na matamko hayo ana haki ya kuyapeleka malalamiko yake kwa Jeshi la Polisi ili hatua zaidi ya uchunguzi wa kisheria iweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Almas Athuman Maige; Idara ya Usalama wa Taifa itoe semina kwa Waheshimiwa Wabunge ili waweze kupata uelewa juu ya kazi na shughuli za Usalama wa Taifa. Mimi nakushukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Maige, kama nilivyoeleza tangu mwanzo, ukifuatilia maelezo yangu juu ya Idara hii utaona kwamba tunawauliza maswali inawezekana wakati mwingine kwa kutokufahamu na mimi tangu nimeingia katika Wizara nilipoliona hivyo, ombi limepokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali ilishapeleka maombi Ofisi ya Spika kuhusu kufanyika kwa semina hiyo katika kipindi hiki cha Bunge linaloendelea ili tuelewane wao wanafanya nini. Mpate muda wa kuuliza maswali, mjiridhishe ili tuendelee kuwahoji yale yanayowahusu, yale yasiyowahusu tushughulike na wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora safari hii ilikuwa ni Idara ya Usalama tu; utendaji kazi wa Idara ya Usalama wa Taifa hauridhishi, je, inacho Kitengo cha *Economic Intelligence* ambacho kingeweza kutoa ushauri kwa Serikali juu ya masuala mbalimbali ya kiuchumi yakiwemo ya usimamiaji wa miradi na mikataba ya uwekezaji? Ameuliza ndugu yangu Mheshimiwa Ngwali hapa, ametoka, basi lakini atasikia. Mheshimiwa Ngwali alikuwa Mjumbe machachari kwenye Kamati yangu, safari hii sijui amehama, sijamuona, na anatuhamasisha watu wa Serikali kufanya mambo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, muundo wa Idara ya Usalama unatokana na majukumu yaliyobainishwa katika Sheria Namba 15 ya mwaka 1996 inayounda taasisi hiyo. Moja, anasema Usalama wa Taifa

hauridhishi; nataka nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Ngwali, nchi hii iko salama, jahazi linakwenda, limeshikwa na nahodha madhubuti, kazi yake yeye ajishikilie tu mawimbi yakija asije akaanguka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama nilivyosema, shughuli zao hufanyika kwa faragha. Sasa muasisi wa Jamhuri ya Watu wa China, Mheshimiwa Mao Tse-Tung alisema hivi; "*no research, no right to speak*". Jambo ambalo hujalifanya utafiti, huna uhakika nalo usiliseme. Ndugu yangu Mheshimiwa Ngwali una uhakika gani kwamba hayo unayoyasema kwenye idara hayapo? Umeshawahi kuingia kule? Lakini kwa sababu shughuli zao wanafanya kwa faragha siwezi nikakujibu kwamba kitengo wanacho au hawana kwa sababu mila na desturi ya chombo cha usalama ni kufanya kazi kwa faragha. Lakini jibu la uhakika tu nilllokupa ni hilo moja kwamba nchi iko salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa TAKUKURU na Usalama wa Taifa, ndugu yangu Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, nakushukuru. TAKUKURU na Usalama wa Taifa waendelee kutumia utaalam na weledi kuishauri Serikali katika kukusanya mapato na matumizi ya fedha za umma; ushauri umepokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwengine miradi ya maji Handeni Vijijini ina ubadhirifu wa rushwa. Tumeeleza hivi; Serikali imedhamiria kutokomeza rushwa nchi hii, kuondoa umaskini na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU imekuwa ikifuatilia miradi ya maendeleo na nataka nikuhakikishe mpwa wangu, Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita, kwamba jambo ulilolitaja TAKUKURU ina taarifa nalo, inalifanya kazi muda mwafaka ukifika tutachukua hatua. Tukiwaona kwamba baada ya utafiti hawana hatia tutawaacha, tukiona wana hatia hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU wavezeshwe kuwa na ofisi nzuri na vitendea kazi ili waweze kufanya kazi

kwa ufanisi. Ndugu yangu Mheshimiwa Juma Selemiani Nkamia, nakushukuru kwa kututetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ofisi za Serikali ziwe na ushirikiano na TAKUKURU ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma. Maelezo yake ni kuwa Serikali itaendelea kuiwezesha TAKUKURU kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwapatia vitendea kazi na kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kadri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu. Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha Serikali imepanga kujenga ofisi saba za Wilaya na mwaka 2018/2019 zitajengwa ofisi kumi. Kwa hiyo, ninaomba tu Waheshimiwa Wabunge na ndugu yangu Mheshimiwa Juma Selemiani Nkamia na Mheshimiwa Emmanuel Papian basi mtuunge mkono, mpitishe bajeti hii ili ofisi zijengwe kama mnavyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyininge inasema Serikali iandae utaratibu wa kuingiza somo la maadili katika mitaala ya elimu ya msingi na sekondari ili kujenga kizazi chenye maadili na uzalendo ambacho kitaelewa, kitachukia na kupinga vitendo vya rushwa. Nataka nishukuru kwa ushauri huo. Somo la maadili limeingizwa katika mitaala ya elimu ya msingi na masomo yanayofundishwa ni uraia na maadili. Kwa upande wa shule za sekondari somo la maadili linajitokeza katika masomo ya *general studies* na *civics* (uraia).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mchakato wa kuanzisha mitaala ya somo la rushwa kwenye shule za sekondari unaendelea. Vilevile katika kuimarisha elimu ya maadili shulen na vyuoni kumefunguliwa na vilabu vya maadili katika shule na vyuo mbalimbali. Ushauri tumeupokea, tunaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyininge, Sekretarieti ya Maadili inapowataka viongozi kuwasilisha fomu waeleze pia nyaraka nyininge zote zinazotakiwa kuwasilishwa ili ziwasilishwe kwa pamoja. Hoja tumeipokea hitaji la nyaraka na mali za madeni ya viongozi wa umma hujitokeza pale sekretarieti inapotaka kufanya uhakiki wa matamshi ya

rasilimali na madeni ya viongozi wa umma baada ya kupokea fomu hizo ili kuthibitisha ukweli wa tamko lilitolewa na kiongozi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Zoezi la kutambua na kuandikisha kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza na mradi wa ruzuku kwa kaya maskini ifanyike mapema ili kaya maskini katika maeneno hayo yanufaika na mpango wa ruzuku. Takwimu zinaonesha yapo maeneno ya vijiji 4,408; mitaa 1,189; shehia 96 ambayo haijafikiawa katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ni kuwa utaratibu wa kufikia vijiji vyote ambavyo havijafikia umeandalowi katika sehemu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini tunaotarajia kuanza mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba Serikali ianze maandalizi ya kuwezeza mpango wa ruzuku kwa kaya masikini kuwa endelevu; ushauri umetoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge na Utawala ushauri umepokelewa. Hata hivyo *TASAF* inakitengo maalumu cha kukuza uchumi wa kaya ambacho kinaandaa kaya na walengwa kutoka kwenye mpango wakiwa tayari na stadi na kuendelea na maisha yao pale mpango ukapokwisha au watakaphitimu kwenye mpango ili kuwapisha wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nydingine ni kwamba Halmashauri zitumie maofisa maendeleo ya mamii ili kuelimisha wanufaika wa mpango wa ruzuku wa kaya maskini namna wanavyoweza kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujikwamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya maeneo walengwa wamenufaika kwa kuanzisha kilimo na ufugaji wa kutumia sehemu ya ruzuku. Maelezo ya Serikali ushauri tumeupokea, kwa kiasi kikubwa mpango wa kunusuru kaya maskini unafanya kazi na Maafisa Maendeleo ya Jamii amba wengi wao ni waratibu wa mpango katika ngazi za

Halmashauri. Serikali itahakikisha kuwa katika maeneo ambayo bado hayaajanza kuwatumia watumishi hao wawashirkishe katika shughuli za mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba Serikali iwafuatilie kwa karibu viongozi wanasiasa katika vitongoji, vijiji na kata kwani yako malamiko ya baadhi ya wananchi kuwa baadhi ya viongozi wanasiasa wanatambua na wahitaji kwa upendeleo bila kuzingatia vigezo. Maelezo ya Serikali, utambuzi wa kaya maskini katika maeneo yaliyoko kwenye mpango hufanywa na wananchi katika mikutano ya hadhara ambayo inasimamiwa na viongozi wa vijiji, miji na Halmashauri. Hata hivyo yanapotokea malalamiko uhakiki hufanyika na kuwaondoa wasiokuwa na vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hao wanaonufaika sasa na mpango wa *TASAF*, tulipoanza utekelezaji baadhi ya maeneo wananchi walilalamika, tukatumia vyombo vyaa Serikali katika ngazi zinazohusika na walipothitisha kwamba ni kweli wameongopa wametolewa katika mpango wa *TASAF*. Vilevile watumishi wa Serikali waliokuwa wamewasajili watu ambao wanajua hawakuwa na sifa ya kusajiliwa na wao wamechukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Serikali iongoze bajeti ya MKURABITA na kutoa kikamilifu na kwa wakati ili kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji wa ardhi na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Serikali ni kuwa Serikali imeendelea kuona umuhimu wa shughuli za MKURABITA na kuendela kutenga fedha katika bajeti kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga bilioni 4.3 ambapo hadi kufikia jumla ya shilingi bilioni 2.4 sawa na asilimia 57 zimepokelewa na kutumika. Aidha, mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya shughuli za MKURABITA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutoa fedha kama zinavyotengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine; katika utekelezaji wa shughuli za MKURABITA ambao umewanufaisha wengi wakiwemo wanawake bado vijana hawajanufalka kwa kiwango cha kuridhisha na mpango huu. Serikali ifanye utaraibu utakaowezesha vijana wengi kunufaika. Maelezo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 MKURABITA imejipanga kutumia fedha ya kituo kimoja cha urasimishaji kuwawezesha vijana kuwa wabunifu kuchangia katika upatikanaji wa ajira na hivyo kuwa wameshiriki katika kujenga uchumi wa Taifa. Aidha, jumla ya vituo vitano vya usafirahji biashara vitaanzishwa Tanzania Bara na viwili Tanzania Zanzibar, vituo hivyo tumevitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, benki na taasisi za fedha zikielimishwa kuhusu ardhi na hati ya haki miliki za kimila kutumika kama dhamana ya mkopo zitatoa mikopo kwa wananchi wanaomiliki ardhi kwa hati hizo. Maelezo ni kuwa kwa sasa benki na taasisi nyingine za fedha zinakubali hati miliki za kimila tutumika kama dhamana ya mkopo na pale itakapotokezea kwamba kuna benki inakataa Waziri wa Nchi anayeshughulika na masuala ya Utumishi na Utawala Bora nikiletewa habari nitafanyi kazi.

Mhehsimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inasema Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*) uwezeshwe kifedha kutanua wigo wa shughuli zake nchini na hivyo kuwafikia wanawake na vijana. Majibu ya Serikali ni kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imeongeza bajeti ya maendeleo ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea kutoka shilingi milioni 500 mwaka 2017/2018 hadi shilingi bilioni 1.7 mwaka wa fedha 2018/2019 ili kutatua wigo wa kuwafikia wanawake na vijana wengi zaidi. Aidha, Serikali itaendelea kuuwezesha mfuko huu kulingana na uwezo na itaendelea kushirikiana na mamlaka ya Seriakli za Mitaa na wao waendelee kutoa mikopo kwa walengwa waliopo katika eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine inasema Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (*Uongozi Institute*) itoe mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi walioteuliwa

ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria kanuni na miongozo ya kiutendaji, na hivyo kuepusha migogoro isiyo na lazima ambayo inaweza kuibuka. Hii imetoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa. Majibu ya Serikali ni kuwa Serikali kupiditia taasisi mbalimali ikiwemo *Uongozi Institute* ina jukumu la kutoa mafunzo ya uongozi na utawala bora kwa viongozi wanaoteuliwa ikiwa ni pamoja na viongozi wa Mikoa, Wilaya, Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria kanuni na miongozo ya kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miezi nane iliyopita mafunzo yaliyohusisha mahusiano ya kiutendaji katika viongozi wa siasa na watendaji, utawala bora na uwajibikaji maadili na kujenga sifa binafsi za kiuongozi yaliitolewa kwa Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupiditia Taasisi ya Uongozi. Aidha, taasisi imeandaa mafunzo ya aina hiyo kwa ajili ya wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa. Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa viongozi wanaoteuliwa pale inapohitajika kwa lengo la kuimarisha uhusiaono wa kiutendaji wa kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ile inayohusu kwamba Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kiwezeshwe kukamilisha awamu ya mwisho ujenzi wa jengo ambalo linaendelea katika *campus* ya Tabora. Maeleo ya Serikali ni kuwa Kamati inatambua umuhimu wa kukamilisha ujenzi wa jengo liliopo katika *campus* ya Tabora, ujenzi huu unatekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ya chuo. Aidha, katika mwaka wa fedha kiasi cha shilingi milioni 500 kimetengwa, shilingi milioni 800 kwa mwaka wa fedha zimetengwa kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niihakikishie Kamati inayonilea hapa Bungeni ya Katiba na Utawala kwamba mimi Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii nitasimamia na kuhakikisha kuwa jengo lile linakamilika ili *Tabora Secretarial College* ambayo ndiyo *Secretarial College*

ya kwanza ya Serikali katika nchi hii kuirudishia hadhi yake. Ndiyo maana hata katika mafunzo ya *degree* ya ma-secretary tumeanza Dar es Salaam, lakini tunafanya maandalizi Tabora ili *Tabora Secretarial College* itoe *degree* ya u-secretary kwa sababu ndicho chuo cha mwanzo cha ma-secretary cha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine Serikali iangalie uwezekano wa kuridhia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuajiri bila kibali na kuziachia kuendesha mchakato wa ajira kwa watumishi wa kada za afya. Maeleo ya Serikali ni kuwa kuajiri watumishi baada ya kupata kibali na matakwa ya Sheria ya Utumisha wa Umma Namba Nane ya mwaka 2002 pamoja na kanuni zake. Aidha, Bunge katika Sheria ya Mabadiliko Sheria Mbalimbali (*Written Laws Miscellaneous Amendment* Namba Mbili ya mwaka 2013 iliifanyia marekebisho Sheria ya Utumishi wa Umma Namba Nane ya mwaka 2002. Katika mabadiliko hayo Katibu Sekretarieti ya Ajira amepewa mamlaka ya kukasimu uendeshaji wa mchakato wa ajira kwa waajiri katika tangazo la Serikali la mwaka 2014 ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekasimiwa kuendesha mchakato wa ajira wa kada za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachosema kwamba ombi hili limepokelewa na Serikali, Halmashauri zimekasimiwa kufanya huo mchakato wa mahojiano mpaka ajira, lakini kila inavyotokea hivyo, kwa sababu kule Wilayani tunafahamiana huyo mtoto wa mjomba, huyu mtoto wa fulani, Sekretarieti ya Ajira inatuma wawakilishi katika mchakato huo ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka. Kwa sababu haki isipotendeka lawama si Halmashauri lawama ni ya Waziri mwenye dhamana ya Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine imelezwa kwamba kuna upungufu mkubwa wa watumshi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususani kada ya walimu wa shule za msingi, walimu wa masomo ya sayansi, hisabati, watumishi wa kada ya afya, watendaji wa vijiji, watendaji wa mitaa watendaji wa kata, maafisa ugani wa kilimo na

mifugo na watumishi wa kada nyinginezo. Majibu ya Serikali ni kuwa katika kila mwaka wa fedha Serikali imekuwa ikitenga nafasi za ajira mpya kulingana na mahitaji yake pamoja na vipaumbele vyake hususani katuka maeno ya elimu kilimo, afya, mifugo na uvuvi kutokana uwezo wa kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2018 Serikali imeajiri watumishi zaidi ya 18,000 ili kukabiliana na upungufu wa watumishi katika sekta za kipaumbele na zenyé upungufu mkubwa kwa watumishi. Aidha, Serikali imepanga kuajiri watumishi 52,436 katika mwaka wa fedha 2017/2018 wengi wao wakiwa wa idara ya elimu afya na serikali za mitaa. Hawa tunaowaaajiri mlisshapitisha katika bajeti iliyopita, ni tofauti na wale 49,000 tunaotaka kuwaajiri katika bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo katika mwaka wa fedha 2018 Serikali imetenga nafasi ya ajira jumla 49,536 na hapa Waheshimiwa Wabunge kwa faida ya Bunge letu na faida ya wananchi wapate kufahamu; ni kwamba zoezi la ajira lilisimama wakati umeanza mchako wa kuhakiki vyeti. Ilionekana si busara unampandisha mtu leo halafu kesho unaambiwa cheti *fake* unaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi lile la kutambua vyeti *fake* limekamilika ndiyo maana Serikali ikaanza kuwaajiri watu mbadala wale waliondolea zoezi hilo nalo sasa karibu limekamilika tutaendelea na ajira mpya kama nilivyosema, 52,000 wa mwaka jana 2017 na mwaka ujao Serikali imejipanga kuwaajiri 49,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya msingi sana, kwamba Serikali ifungue milango ya uhamisho kwa watushi amba wanahitaji kuungana na familia pale mwenza mmoja anahamishwa ili kuondoa usumbufu wa familia. Aidha, kumekuwa na usumbufu mkubwa wa mtumishi anapotaka kuhama na kuambiwa atafute mtu wa kubadilishana naye, na kwamba asipopatikana huyo mtumishi anakosa haki ya kuhama. Je, huo ni wajibu wa

mtumishi au Serikali kutafuta jinsi ya kujua ni wapi mtumishi huyo atapangwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya Serikali ni kama ifuatavyo; Serikali hajafunga milango ya watumishi wale wanaotaka kuhama ili kuungana na familia zao au kwa sababu nyingine zozote zile za msingi. Aidha, maelekezo yametolewa kwa waajiri kupitisha maombi ya watumishi yaliyowasilishwa kwao ili mradi yamezingatia taratibu zilizopo kwa kuwa si sera ya Serikali kuzuia uhamisho wa watumishi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba nitoa maagizo haya kwa mamlaka zote za Serikali za ajira katika nchi hii. Malalamiko makubwa waliyonayo watumishi wa umma ni kwamba wakiomba kuhama anapotakiwa kupitisha barua kwa mkubwa wake wa kazi wanawakatalia! Wanawakatalia! Sasa naomba kulieleza Bunge hili tukufu, mwenye mamlaka ya kumkatalia uhamisho ni yule anayeandikiwa barua, wewe uliyеandikiwa pale kupitia kwa, kiswahili sanifu kabisa kupitia kwa, wakishasema kupitia kwa wewe si mwamuzi wa mwisho, ndiyo maana inaandikwa kupitia kwa, peleka barua kwa mwajiri ili mwajiri apate kuamua. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natembelea mikoani nimekwenda mkoaa mmoja naambiwa hii ofisi yetu hajapitisha barua ya mtu kuhama hata siku moja.

Mimi ninasema, mimi ndiye Waziri wa Utumishi wa Umma, nikibaini kuna kiongozi wa utumishi anakataa kupitisha barua isinififikie mimi isimfikie Katibu Mkuu Kilimo, isimfikie Waziri Mkuu nitamshughulikia kwa mujibu wa sheria na taratibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafanya hivyo kwa sababu mtu huyo amejichukulia madaraka yasiyo yake, hukuandikiwa wewe barua umeandikwa kupitia kwa, sasa kupitia kwa wewe ndiyo unaamua? Sasa mimi niliye juu hapa nitafanya kazi gani kama wewe unaniamulia?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja imetolewa hapa na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, sasa rafiki yangu mwenyewe yuko wapi, amenikimbia? Anasema Serikali ilete muswada wa sheria wa kuibadili *eGA* kuwa mamlaka ili kuwa na nguvu za kisheria kusimamia na kudhibiti utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu kuhusu Serikali Mtandao na je, Wakala wa *eGA* umetengewa kiasi gani kukabiliana na teknolojia inavyobadilika? Swali zuri na ushauri umepokewa ndugu yangu Mheshimiwa Ngwali, mchakato wa kutunga sheria ya kuibadili Wakala wa Serikali Mtandao kuwa mamlaka tayari umeanza Serikalini, na hapa mimi nataka niishukuru Kamati yangu ya Utawala na Serikali za Mitaa, wao wamejenga hii hoja ndani ya Kamati wamenishauri mimi Waziri ninayehusika tuanze mchakato wa kuibadili kuwa mamlaka ya Serikali mtandao.

Mheshimiaw Naibu Spika, kazi hiyo imeshaanza mimi natekeleza kama nilivyoagizwa na Kamati yangu; mimi mtumishi wa Bwana, nitatenda kama Bwana anavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 Fungu 22 Wakala wa Serikali Mtandao imetengewa kiasi cha fedha shilingi bilioni nne kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizi pamoja na mambo mengine zitaanzishwa kituo cha utafiti, ubunifu wa maendeleo ya Serikali Mtandao Makao Makuu Dodoma ili kukabiliana mabadiliko ya kiteknolojia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika hoja ambazo naomba kuzisemea leo, kwamba Serikali iwezeshe kikamilifu Idara Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa kwa ajili ya kufanya tafiti, kukusanya na kuhifadhi taarifa na kumbukumbu muhimu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Miiongoni mwa njia ya kukusanya taarifa hizo ni kutembelea na kuhoji watu wenye umri mkubwa ambao wameshuhudia mambo mengi ambayo ni muhimu kwa taifa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya Serikali ni kuwa Serikali inatambua umuhimu wa kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka ili kuhifadhi urithi andishi kwa ajili vizazi nya sasa na vizazi nya maendeleo ya Taifa letu. Katika kutekeleza jukumu hili Serikali imekuwa ikitenga fedha kupitia bajeti ya kila mwaka kulingana na uwezo wa kifedha kwa lengo la kuiwezesha idara kutekeleza majukumu yake. Kutohana na fedha hizo idara imekuwa ikitekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kufanya tafiti kutambua, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka zenye umuhimu kutoka taasis za umma katika sekta mbalimbali na za watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasemea. Taratibu na mila za Bunge zinataka niyasome majina ya watoa hoja nilikuwa na mashaka ya muda, ukiruhusu nitawasoma waliotha hoja, usiporuhusu nitawaweka wataingia katika kitabu chetu cha kumbukumbu ya *Hansard*...

**NAIBU SPIKA:** Waweke waingie kwenye kumbukumbu kwa sababu kanuni zetu haziruhusu kutaja majina, usiwaite kwa sababu kanuni zetu haziruhusu waingine kwenye *Hansard*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelekezo, wote mliotoa hoja hizi majina yenu tutayaingiza kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge kama mtakavyoona tumejitahidi kuangalia maeneo yapi Wabunge walitaka maelezo, maeneo yapi lazima yafanyiwe kazi. Mimi nataka niseme kwa naiba ya Serikali nataka niwashukuru Wabuge wote kwa michango yenu.

Mimi Waziri hii ndiyo bajeti yangu ya kwanza, lazima niseme nimenufaika sana na michango mliyotoa Wabunge imetuwezesha, mmetuboresha, mmetuweka kuwa imara ili utendaji wa kazi ndani ya Serikali ya Tano uweze kuwa na ufanisi zaidi.

Sasa naomba kuhitimisha maelezo yangu kwa kuomba Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hoja hii ili kuwezesha ofisi yangu kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zake kwa ufanisi katika mwaka ujao wa 2018/2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, kwa hivyo tutaendelea na utaribu wetu.

Waheshimiwa Wabunge nikumbushe jambo moja kabla sijaendelea; Kanuni ya 99(14) inasema hivi; bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ya 154 maneno yoyote ya utangulizi, utambusho, salamu za pole, pongezi au shukrani pamoja na kutaja majina ya Wabunge waliochangia hoja havitaruhusiwa kwa Mbunge au Waziri wakati wa kujadili hoja ya bajeti, kwa sababu tunaelekea mbele huko zitakuwepo Kamati nydingi zinaleta taarifa hapa, lakini pia Waheshimiwa Mawaziri wakihitimisha hoja zao kanuni zetu zinakataza kutaja majina. Kwa hiyo, kama utaratibu wetu ulivyo mtaingiza hayo majina kwenye *Hansard*.

Baada ya kusema hayo kwa mujibu wa kanuni ya 28(2) inataka nikiwa nasitisha Bunge kabla ya wakati niwahoji kuhusu kuahirisha Bunge kabla ya saa saba mchana.

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)  
Hoja liliamuliw na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni leo.

*(Saa 06:40 Mchana Bunge liliisitishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Katibu

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais,  
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais,  
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa  
Mwaka wa Fedha 2018/2019

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 56 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za  
Mitaa**

Kif. 1001–*Admin and HR Mgt. Div.*.....Sh. 3,776,900,000/-

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hiki ndicho kifungu chenye mshahara wa Waziri na majina ninayo hapa mbele kwa mujibu wa Kanuni zetu kwa Wabunge ambao wangependa kuzungumzia ama kutaka ufanuzi kwenye masuala ya kisera. Tutaanza na Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**MWENYEKITI:** Wewe ni Utumishi? Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nachangia kwa kuongea nilizungumzia suala la Hospitali ya Kaliua na ni Sera ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma za afya zinatolewa kwa karibu na kila Wilaya inakuwa na hospitali lakini pia kila kata inakuwa na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa Kaliua *priority* yetu kwa mwaka huu viongozi waliitwa hapa Dodoma na wakaambiwa kwamba waseme kipaumbele chao na tukasema sisi ni Hospitali ya Wilaya kwa sababu pamoja na kuwa ni Wilaya mpya lakini katika Wilaya yenyе kata 26 tuna vituo vya afya vinne tu. Hata hivyo zahanati ni chache, watu wanapata huduma Tabora, Kigoma na pia Urambo. Kwa hiyo, tukajua kwamba mwaka huu Serikali ingetuangalia, jinsi ambavyo viongozi wetu walivyokuwa wameweahidi. Mpaka kwenye bajeti ya Mkoa ipo walitupa tuweze kuwa na hospitali nne katika Mkoa wa Tabora. Hata hivyo kwa masikitiko makubwa, wakati Mheshimiwa Waziri anatamka hapa leo Kaliua haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaiomba Serikali ituambie ni kwa nini pamoja na kuwa tuna shida kubwa na akina mama wengi wanapoteza maisha kutokana na kukosa huduma, lakini pia Kaliua mwaka huu kwenye kupata fedha za kumalizia Hospitali ya Wilaya ambapo kiukweli tulishalianza, tayari tulishajenga *OPD*, jengo la ghorofa moja kwa mapato ya ndani. Tulikuwa tunaiomba Serikali itusaidie tuweze kukamilisha ili tupate huduma za afya kwa karibu na hivyo tuweze kuokoa maisha ya akina wama na watoto ambao wanakufa kwa kukosa huduma za afya.

Mheshimiwa wenyekiti, nakushukuru, na kwa kweli nisipopata majibu ya kuridhisha nitaomba nikamate shilingi ili niweze kupata *commitment* ya Serikali kwenye hili, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Magdalena Sakaya *commitment* ya eneo lako peke yako linakuwa ni la kisera hilo? Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa kufika kipindi hiki cha Kamati ya Bunge lako. Ni kweli hoja hii nadhani si dada yangu Magdalena Sakaya peke yake aliyezungumza, tukumbuke kwamba nilizungumza wazi kwamba ukiachia Jiji la Dar es Salaam tuna Halmashauri takribani 184 na nilizungumza kwamba katika Halmashauri hizo tuna jumla ya hospitali 120, lakini zile za Serikali ni 77 na nikasema tuna safari ndefu sana ya kwenda na ndiyo maana mwaka huu tumeanza na hospitali zipatazo 67 tunajua bado tuna safari ya kwenda. Hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge alisema katika Kamati ya Mkoa walijadili kwamba kulikuwa na hospitali nne ina maana kwamba mikoa yote 26 ukizungumza mara nne maana yake tulijenga kwa wakati mmoja hospitali zaidi ya *100 plus*. Kwa hiyo tulichokifanya ni *distribution* ya kimkoa; na kila mkoa ukiangalia kwamba kuna wastani wa katи ya hospitali mbili mpaka tatu, lengo likiwa ni kuzigawanya rasilimali hizi zote katika nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba halmashauri zote zinajenga hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Magdalena Sakaya awe na subira kwamba Serikali itafanya kila liwezekanalо, kwa sababu mkakati wetu ni wa kuhakikisha kila halmashauri iwe na Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, dada yangu Magdalena Sakaya usiwe na hofu Serikali iko hapa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wa Kaliua na sehemu nyingine zote za nchi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya kwa mazingira haya inabidi tuendelee kwa sababu ilikuwa ni hoja mahususi kweye eneo lako lakini nikaona Waziri azungumze kwa sababu eneo hili tunazungumza yale ya Kisera kwa ujumla. Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi katika huu mshahara wa Waziri. Wakati nilipokuwa nikichangia kwenye bajeti ya TAMISEMI na Utumishi nilizungumzia jinsi ambavyo Sera ya Taifa inataka tuwawezeshe wananchi kiuchumi, na nikawa

nimeeleza masikitiko yangu jinsi ambavyo naona ule Mfuko wa Wanawake na Vijana ambavyo hautengwi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawa nimeishauri Serikali kwamba Waziri atakapokuwa amekuja hapa aje na maeleo ya kina ya lini muswada wa sheria utaletwa hapa Bungeni ili Bunge hili tukufu liweze kuweka utaratibu ambao utawezesha halmashauri zetu zote nchini kutenga fedha asilimia 10 ya wanawake na vijana. Sasa ningependa kujua Serikali ina mkakati gani na kwe kweli nisiporidhika ya namna ambavyo italeta sheria na mimi nakusudia kutoa katika mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba asilimia 10 ya makusanyo ya ndani yanatengwa na katika maeleo yangu niliyotoa asubuhi hapa inawezekana mama yangu hakunisikiliza vizuri. Nilisema kwamba Mheshimiwa Waziri anakusudia katika *Finance Bill* ambayo itapitishwa na itakuja kwenye Bunge lako kuna *revenue* ambayo itakuwepo pale ambapo Mheshimiwa Waziri atapendekeza kuingiza kwenye kifungu hicho ili iwe ni takwa la kisheria kwa Wakurugenzi wote na kwamba kama itatokea kwamba Mkurugenzi hatatekeleza kutenga hiyo asilimia 10 *then* sheria itachukua mkondo wake, kwa hiyo tulilisema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Makilagi nadhani anachojaribu kusema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ni kwamba usubiri *Finance Bill* itakuwa na hiyo hoja yako, nadhani umeshamuelewa? Ahsante sana. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kupata ufanuzi. Sina nia ya kushika mshahara wa Waziri lakini nilikuwa nahitaji tu kupata ufanuzi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2018/2019 nilikuwa ninaangalia katika kipengele muhimu kabisa cha utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais, lakini nimeona kwamba hakuna mahali popote ambapo panaonesha dhahiri panapolezea namna ya utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais. Ninasema hivyo nikiwa na mfano maalum na nitatolea mfano kutoka katika Jimbo langu; kwamba katika mwaka 2015 wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya lami katika Mji Mdogo wa Katoro kilomita tano pamoja na kilomita Buseresere. Hata hivyo tangu tumeanza hizi bajeti hatujaona utekelezaji ukifanyika. Sasa nimeona nipate ufanuzi katika jambo hili ili wananchi pia waweze kuelewa hatua inayoendelea katika ahadi za Rais?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kifungu hiki kinashikwa na mambo ya sera tusizungumzie majimbo kwa sababu la sivyo kila mtu atataka kusimama azungumze kuhusu jimbo lake. Mheshimiwa Waziri kwa hoja yake ya utekelezaji wa jumla wa ahadi za Mheshimiwa Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa dada yangu Mheshimiwa Lolesia Bukwimba. Ahadi za Mheshimiwa Rais zote zinaratibiwa na chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu tumeweza kutekeleza ahadi mbalimbali ambazo tumeziratibu katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo naomba niwahakikishie, maeneo mengi sana ambayo ahadi za Mheshimiwa Rais alizoziahidi tumeendelea kuzitekeleza hasa ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ninafahamu maeneo hayo ahadi ipo na katika kipindi hiki cha miaka mitano mpaka ikifika 2020 imani yetu ni kwamba tutakwenda kuondoa ahadi moja baada ya nytingine. Kwa hiyo, katika suala la ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa ujumla wake tuseme kwamba Serikali tumeziratibu na ziko katika hatua mbalimbali ya utekelezaji, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge awe na subira tu katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasuku Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi pia naomba ufanuzi kuhusu suala zima la kuhamisha walimu kutoka shule za sekondari kwenda shule za msingi. Ninakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Waziri kwamba hawa wangeweza kupata *retrenchment* kwa sababu ya kuzidi kwao. Ninachotaka kuhoji ni utaratibu mzima uliotumika ambao haukuwa na maandalizi ya kutosha kiasi kwamba unaleta usumbufu kwa walimu wapatao 8,000 yaani walimu 8,000 si kitu kidogo. Watu wana familia, wana majukumu na *status* zao tu ambazo zimefika mahali hazithaminiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi kama lingekuwa limeandaliwa hawa walimu wangeandaliwa malipo yao. Kwa mfano, pale ambapo..., tena naomba *ni-quote* kwenye Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2003; "*Where disturbance allowance is payable, must be paid prior departure.*" Hawa watu walishaondoka, *disturbance allowance* wanayostahili hawakupata. Baada ya *disturbance allowance* wanaandaliwa usafiri kwenda kwenye vituo vyao; wakifika kwenye vituo vyao wakakosa nyumba ya Serikali wana-*deserve subsistence allowance*. Yote hayo hayakufanyika kabisa, ni asubuhi barua hiyo hapo, mwalimu anza kuondoka. Sasa tunashuhudia wanapodai hata haki zao wanaanza kupigwa mabomu, jamani hawa ni watumishi wa umma, hawana kosa lolote, wao hawakusababisha wazidi kule shule ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninatarajia kushika mshahara wa rafiki yangu Waziri Jafo kama sitapata maelezo mazuri, ikiwa ni pamoja na namna watakavyopata *training* ya kufundisha shule za msingi wakiwa wame-*undergo course* ya kufundisha *a secondary school*. Mafunzo hayo watayapataje?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwasababau tunaendelea na hili zoezi niwakumbushe ni suala moja mahususi si masuala yote yanayohusu jambo hilo. Kanuni zetu zinataka suala moja mahususi la kisera. Kwa hiyo, tukumbuke wakati nikiendelea kuita majina hapa. Mheshimiwa Waziri kuhusu hoja yake ya mwanzo hayo mengine nadhani ameongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA**

**NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa Mheshimiwa Bilago na nilifafanua kwa kina sana mwanzo nikija kwamba Mwalimu kama Bilago na yeye anafahamu sarakasi za mambo ya taaluma kule. Nilisema wazi kwamba kuna walimu ambao kimantiki walikuwa wanafundisha kipindi kimoja na wengine vipindi viwili kwa wiki nzima ambapo *minimum* vipindi vinatakiwa 24 kwa wiki, hilo ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo nikazungumza tena kwamba walimu tunaowahamisha kwa kiwango kikubwa sana ni walimu hawa wa lugha pamoja na masomo ya sanaa na nikasema tena kwamba ukiangalia kwa kiwango kikubwa katika shule zetu za msingi, walimu hawa wa lugha ya kiingereza ni imani yetu ni kwamba wakishuka katika shule za msingi *impact*yake itakuwa kubwa sana. Hata hivyo nikasema tumekiri kupokea mawazo ya Wabunge, kwamba suala la *induction course* tutalifanyia utaratibu ili walimu wetu hawa waweeze kuona jinsi gani wataingia vizuri katika maneо haya; jambo hili lazima tulipange vizuri, litakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuhusu suala la malipo kuna *case by case*, hilo lillojitokeza si maeneo yote ni uniform, kuna Halmashauri nyingine zimefanya vizuri sana. Ndiyo maana nimesema katika hii pesa ya *EP4R* ambapo tumetoa bilioni 40; 20% ya hiyo ambayo ni bilioni nane inakusudiwa kwa ajili ya mtawanyo wa walimu na nikasema tena kwamba Halmashauri nyingine zimefanya vizuri lakini halmashauri nyingine inaonekana kuna changamoto hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili si kwa Tanzania nzima, na nikasema kwamba tutachukua *case by case* zilizojitokeza katika baadhi ya Halmashauri kwa lengo la kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Bilago baada ya ufanuzi huu wote wa kina, imani yangu ni nini? Pale kwenye mapungufu tuta-address mapungufu kutokana na *specific case* iliyopo. Ni imani yangu kwamba walimu wale, na mimi naomba sana Waheshimiwa Wabunge, tuwatengeneze na sisi kisaikolojia sisi sote ni viongozi. Tujue kwamba hata katika nchi za wenzetu walimu hawa wengine *wana Ph.D*, *wana Masters* ndio wanafundisha *primary school*. Tunataka tuhakikishe tunapeleka elimu kubwa kwa vijana wetu. Kwa hiyo, nadhani ni jambo tu kwa haya matatizo madogo madogo kuyaweka vizuri na mwishowe tutapata mafanikio mapana sana katika eneo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago naona ameelewa.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado.

**MWENYEKITI:** Bado? Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Waziri hayatoi *commitment* hawa watu wako tayari *point "B"*, walitoka (a) wakaenda (b) hawajalipwa chochote. Kama walikosa nyumba maana yake *subsistence 14 days without accommodation* sijui wanalala nje, sijui wanafanya nini. Tujiulize wenyewe tungkuwa kama ndio tumehama sisi, tusiwafikirie waliohamza. Hawa watu wamesha-*move from point "A" to "B" without any coin* hakuna *payment* yoyote. Kwa hiyo *concern* yangu ilitakiwa Waziri atuambie wiki ijayo walimu hawa wawe wamelipwa ili waache kutembea tembea barabarani kudai mambo yao kama vile siyo watumishi wa umma katika Serikali yao.

16 APRILLI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitoe hoja ili Waheshimiwa Wabunge wanisaidie tujadili hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofii*)

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago inavyoonekana amefanya *lobbyingya* kutosha kabisa. Hoja imeungwa mkono na kambi moja.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tupeane nafasi, Mheshimiwa Masoud una hoja hapa utasimama tena baadaye, Mheshimiwa Marwa na wewe utaitwa. Kwa hiyo, wapewe nafasi Wabunge wenzenu ambao hawana nafasi ya kuzungumza baadaye. Kwa hiyo, wamebaki ambao hawazungumzi baadaye, Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa *Chief Whip*, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Bashungwa na Mbunge wa Geita, Mheshimiwa Constatine Kanyasu. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli jambo hili linaonekana kama vile limefanywa haraka sana. Hata kama Serikali walikuwa na nia nzuri, lakini kwa upande wa elimu tunakwenda kuididimiza, kwa sababu leo hii tunapoongea hao watumishi ambao wamepelekwa shule za msingi wengine wamehama kutoka shule za mbali kama kilomita 50 au 60. Mfano, kwenye jimbo langu bado Walimu wale wanahangaika hawajui nini cha kufanya mpaka leo hii hawajapata stahiki hata moja na wanashindwa kuhamisha familia zao kwenda kwenye kituo kipyaa ambacho wamepangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba Serikali wangetoa kauli kwamba kufikia tarehe fulani hawa

16 APRIL, 2018

wafanyakazi waliohamza wawe wamepata mafao yao. Tena basi uhamisho wenyewe kuna sehemu nyingine haukutekelezwa ipasavyo, watu wamehamishwa kwa hila kwa sababu tu alikuwa na ugomvi na Mwalimu Mkuu au pengine alikuwa na ugomvi na Afisa Elimu anahamishwa tu. Asubuhi hapa Mheshimiwa Waziri amesema vigezo ni kwanzza wale ambao walihudumu kwenye shule za msingi kabla, kigezo cha pili ni wale wa diploma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Lakini hawafuati vigezo. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii, naomba Serikali itoe kauli leo hii hii. *(Makofii)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pascal Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niungane na mwalimu Bilago, ni kweli Serikali haijaonesha *commitment* yoyote ile kwa wale Walimu waliotolewa sekondari kwenda shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa mfano mdogo katika Mkoa wa Songwe na bahati nzuri sana wakati nachangia nilijaribu kutoa mfano kidogo tu. Wilaya ya Mbozi walimu 117 wametolewa shule za sekondari kwenda shule za msingi wanadai zaidi shilingi milioni ya 300 hawajalipwa; Wilaya ya Ileje Walimu 103 wanadai zaidi ya shilingi milioni 300 hawajalipwa na Wilaya ya Rungwe kule kwako Walimu 87 wanadai zaidi ya shilingi milioni 200 hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba tunahitaji Serikali iweze kutoa *commitment* tuambiwe ni lini hao Walimu wanaenda kulipwa. Hicho ndiyo kikubwa zaidi ambacho nadhani Mheshimiwa Waziri hajatuambia.

16 APRIL, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumshusha Mwalimu kumtoa sekondari kwenda shule msingi kiukweli kabisa pamoa na kwamba tunaenda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe kaka yangu Mheshimiwa mwalimu Bilago asizue shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu jambo hili la Walimu toka shule za sekondari kwenda shule za msingi mimi binafsi nikizungumzia kwa upande wa Karagwe tulikutana na changamoto hii lakini baada ya kwenda Serikalini tayari kule Walimu wangu wameshahakikishiwa kwamba watapewa fedha hiyo. Kwa hiyo, jambo hili baada ya kulifuatilia Wizarani wameshajipanga kuhakikisha kwamba Walimu wanapata stahiki zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Bilago arudishe shilingi tupitishe bajeti ya Mheshimiwa Waziri ili Watanzania waweze kupata fedha hii kwa ajili ya kuwasaidia katika kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwelewa Mheshimiwa Waziri kwamba suala hili yako maeneo limefanyika vizuri na yako maeneo lina upungufu kidogo na nikafikiri Mwalimu Bilago atakuwa ameefanya kwamba inawezekana hiyo exceptioniko kwake. Nikichukulia mfano kwenye halmashauri

16 APRIL, 2018

yangu mimi tulikuwa na tatizo kama hilo, lakini baadaye walimu wote walilipwa na tatizo hilo halipo tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe kama kwake tatizo hilo lipo basi tuli-*address* kama tatizo la halmashauri yake ili Walimu waweze kupata haki yao. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Raphael Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba shule za msingi zinakuwa na Walimu wa kutosha na maelezo ya Waziri kwamba tatizo hilo linahusu baadhi ya halmashauri lakini dhamira ya Mheshimiwa Bilago ni *commitment* ya Serikali kwamba baadhi ya hizo halmashauri ambazo zina matatizo ni lini watu watalipwa stahiki zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndiyo eneo peke yake ambalo Serikali ilitakiwa itoe *commitment* kwamba ni lini Serikali italipa hao Walimu ambao wana matatizo na wanahitaji kulipwa stahiki zao? Nadhani ni jambo jepesi ambapo Serikali ingefanya wala hakuna mgogoro kati ya Mheshimiwa Bilago na Serikali. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri tu atoe hii *commitment* ni lini hawa Walimu watalipwa hizo fedha zao ili wawe na *comfort* na waondokane na matatizo yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MILINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hata mimi nimemwelewa Mheshimiwa Bilago lakini pia nimemwelewa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Bilago suala hili limemwingia sana kwa sababu yeye ni Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwangu suala la malipo sio shida, shida kubwa iliyopo ni uelewa wa Walimu ambapo wengi wamechukulia kutolewa shule za sekondari kupelekwa shule za msingi kama *demotion*. Kwa hiyo,

16 APRILI, 2018

naiomba Serikali iharakishe kidogo malipo, japokuwa ameahidi na fedha zipo, ili Walimu wasione kama ile ni *demotion* wachukulie kama *transferya* kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Bilago aachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili hii hela iliyotengwa aweze kwenda kusimamia vizuri ili walimu wakapate stahiki zao. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niseme kwamba siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Bilago na nimwombe Mwalimu mwenzangu kaka yangu aachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri tupitishe fedha zake ili matatizo ya wananchi wake kule Buyungu yakapatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja hii Mheshimiwa Waziri amekwishaeleza vizuri kwamba hizi ni *isolated cases* kwamba zoezi hili limefanyika vizuri kasoro maeneo fulani. Kwa hiyo, nimshauri tu Mheshimiwa Bilago badala ya kushika shilingi kama una maeneo mahususi na Waziri Mheshimiwa Jafo tunamwona mchapakazi, hakuna jambo linalofika mezani kwake likashindikana, ampelekee ili aweze kutatuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Walimu kwamba huu uhamishio siyo kuwashusha madaraka, ngazi zao za mishahara na vyeo vyao vimebakia kama vilivyo. Kwa hiyo, zoezi hili siyo *demotion*, naomba Mheshimiwa Bilago aachie shilingi ili tupitishe bajeti mambo yakafanyike Buyungu kwani maendeleo ya wananchi yanahitajika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja ni yule kule una maelezo kabla sijampa afunge hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA**

**NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu

16 APRIL, 2018

Mheshimiwa Bilago ameshaelewa na imani yangu ni kwamba lengo letu lile kama alivyozungumza Mheshimiwa Profesa Ndalichako na wajumbe wengine humu ndani ni lile kwa sababu tuna *case by case*. Naomba nirekodi kesi ambazo ziko baadhi ya maeneo tuzifanyie kazi kwa sababu maeneo mengine suala hili limeenda vizuri. Kwa hiyo, sehemu ambayo kuna matatizo basi tutayashughulikia kama maeneo fulani ambayo yana matatizo hayo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona Serikali inasitasita kutoa *commitment* hapa pana shida. Mimi ningekuwa Waziri ningeagiza Wakurugenzi wote wiki ijayo wawalipe Walimu hawa ili wawe na *comfort* na *peace of mind*. Hawana *peace of mind* kwa sababu hawajui leo wala kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri mwenye dhamana anashindwa kuji-*commit* wakati fedha zipo *issue* ni kuwalipa wale wenye kesi za kulipwa. Kwani kinachoshindikana hapa ni nini mpaka wasiambiwe kwamba ifikapo kipindi fulani wawe wamelipwa mbona mengine huwa wanatamka kabisa tarehe fulani jambo hili liwe limekamilika, hili linashindikanaje? *It will take centuries to be paid* kama hakuna *commitment* ya Serikali hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hakuna *commitment* inaonesha na ninyi mnajua siri iliyopo ndiyo maana hamtoi hiyo *commitment*. Kuna jambo mnalijua ila hamuwezi kulisema hapa hadharani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona tu kama linashindikana basi tuamue kwa kura. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago nina uhakika umefanya utafiti na kuona hoja hii kama inapita ama vipi. Waheshimiwa Wabunge nitawahoji kwa mujibu wa kanuni zetu.

16 APRILLI, 2018

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Waliokataa hoja hiyo wameshinda, kwa hivyo, hoja ya Mheshimiwa Bilago haijapita. Tunaendelea na Mheshimiwa Selemani Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nitajikita kwenye sera ya afya na hususani suala la kuhakikisha huduma za afya zinapatikana na sera nzuri ya Serikali yetu sasa hivi ya kuamua kujenga hospitali za wilaya katika halmashauri zote ambazo hazina hospitali za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufanuzi kwa sababu kuna baadhi ya maeneo ambayo naona mambo yanakwenda kinyume na sera hii kwa maana ya kwamba kuna halmashauri ambazo tayari zina hospitali ya wilaya kwa mfano Halmashauri ya Nzega DC inashauriwa kuiachia hospitali hiyo iende kwenye mamlaka nyingine Nzega TC na yenye ibaki bila hospitali. Sera ni kwamba halmashauri ambao hazina hospitali zipate hospitali na siyo kwamba halmashauri zenye hospitali, hospitali hizo ziondoke ziende halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kauli ya Wizara katika kutekeleza sera hii, kwa nini isitoe kauli ya jumla kwamba zile halmashauri ambazo tayari zina hospitali usifanyike ushawishi au ushauri wa kuzihamisha hospitali hizo kutoka mamlaka hiyo kwenda mamlaka nyingine wakati TAMISEMI haina uwezo wa kuzipa fedha hizi halmashauri ambazo zimeondokewa na hospitali. Kwa mfano, Halmashauri ya Nzega DC Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa TAMISEMI wote wawili kwa nyakati tofauti walifika Nzega na wakashauri Nzega DC tuiachie hospitali kupeleka Nzega TC lakini katika mgao wa bilioni moja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

16 APRIL, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa sana Mheshimiwa Selemani Zedi na ajenda yetu ni kwamba kila halmashauri tupate hospitali za wilaya kwa lengo la kupeleka huduma kwa wananchi. Eneo lake la Nzega DC na Nzega TC tunafahamu wazi kwamba kuna hospitali lakini iko katikati ya mji wa Halmashauri ya Nzega. Kwa hiyo, mpango na nia njema ya Serikali ni kwamba ni vyema tuhakikishe katika eneo ambalo wananchi wengine wako mbali twende tukapeleke hospitali ya wilaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu hekima ya Mheshimiwa Zedi anasema hospitali ile ilikuwa katika halmashauri ya wilaya sasa iko kwenye halmashauri ya mji, mpango wetu mkakati ni kwamba aseme tu *inshallah* Mungu abariki, tunatafuta fedha wakati wowote, hata jana nilikuwa na watu wangu wametoka Dubai kwa ajili ya kutafuta fedha (*resource mobilization*) kwa ajili ya hospitali za wilaya. Kuna *issue* ya Kaliua, Nzega na maeneo mbalimbali nia ni tupate fedha zingine za ziada tujenge hospitali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya kama tulivyofanya pale Korogwe Hospitali ya Halmashauri ya Korogwe iko katikati ya Mji wa Korogwe tunatafuta fedha tunaenda kujenga katika Halmashauri ya Korogwe Vijijiini tuwapelekee huduma wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zedi wala asihofu eneo hilo, aamini Serikali yake itapeleka huduma kwa wananchi kwa nguvu zote kwa kadri iwezekanavyo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zedi, naona umesimama tena.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *commitment* ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba atafanya kila linalowezekana ili Halmashauri ya Nzega DC ambayo inanyang'anywa hospitali kwamba sasa na yenyewe

16 APRILLI, 2018

itapatiwa fedha za kujenga hospitali *otherwise* bila *commitment* hiyo itakuwa *very unfair*. Kwa hiyo, kwa *commitment* hiyo nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kilio changu ni miundombinu kwa ajili ya watu wenye ulemavu na hasa watoto wa shule ambapo miundombinu katika shule mbalimbali hasa vyoo inasikitisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika vyoo vya shule za msingi hakuna vyoo kwa ajili ya watoto wenye ulemavu. Watoto hawa wenye ulemavu wanalazimika kuingia katika vyoo hivyo hivyo ambavyo wanatumia watoto wengine na wakati mwingine vyoo hivyo utakuta ni vichafu lakini watoto hawa wanalazimika kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuijilize tu hata katika maeneo mbalimbali ya wazi (*public areas*) ambazo utakwenda napo hakuna vyoo kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Hata wakati tunasafiri kwenye mabasi ambapo wana vituo maalum ambavyo wanasimama tuijilize wote ambaao wenzetu mmejaliwa na Mwenyezi Mungu mpo salama kwa hawa ambaao wana ulemavu wanaingia katika vyoo gani? Hili jambo linaumiza, linatumiza sisi watu wenye ulemavu, lakini pia linawaumiza wale wote wanaoelewa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na nina imani kubwa sana na Serikali yangu, lakini endapo majibu hayataniridhisha basi nitashika mshahara wa Waziri. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba

16 APRIL, 2018

kushukuru mchango mzuri wa dada yangu Mheshimiwa Amina Mollel na nikijua wazi kwamba Mheshimiwa Amina Mollel ni Mbunge ambaye dakika zake zote anapambana kuwatetea walemaru katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nishukuru mchango wake mkubwa kwa kazi anayoifanya kwa sababu amekuwa akinisumbua muda mrefu sana mpaka hata kule kwake tuliamua kama Serikali kufanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nduruma na juhudini inaendelea kwa kazi kubwa anayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba kutokana na michango mbalimbali miundombinu mingi tunayojenga sasa hivi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na hasa ukianzia kwenye shule zetu na majengo mengine tumetoa maelekezo maalum kwamba miundombinu ikijengwa izingatie watu wenye ulemavu. Watu wengine ni mashahidi, leo hii hata tukitembelea baadhi ya shule ambazo zina watoto wenye ulemavu, twende Mpwapwa Sekondari na Pugu Sekondari, zamani vijana wanatembea katika hali ya uchafu sana, lakini kwa sababu tumetoa maelekezo maalum sasa hivi kila tunapojenga miundombinu kama ni vyoo katika shule hizi tuhakikisha miundombinu ya watu wenye ulemavu inakuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilio kimesikika, najua miundombinu ilijojengwa mwanzo ilikuwa na changamoto hiyo, lakini kwa utaratibu wa sasa ni kwamba miundombinu yote tunazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, nimhakikishie dada yangu Mheshimiwa Amina Mollel kwamba tutaendelea kuyafanyia kazi kwa nguvu zote mambo haya na hata sehemu zingine tumefikia uamuzi wa kuwabadilisha wakandarasi warudie tena kazi kwa mfano nilivyofanya kule Muheza ni kwa sababu walishindwa kuzingatia mahitaji ya wenye ulemavu. Kwa hiyo, ni *commitment* yetu kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyika vizuri. Ahsante.

16 APRILI, 2018

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, naona ameshakubaliana, anasimama tena, Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri kwa sababu hata kama nikishika mshahara, kikubwa nachohitaji ni *commitment* ya Serikali. Mfano mzuri tu ni uliopo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naupongeza uongozi wa Bunge kwa sababu wamejali mahitaji hayo. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ametoa ahadi naomba *commitment* yake kuhakikisha kwamba basi angalau katika maeneo mengi hata tamko tu vyoo vinavyojengwa basi tuweze kuangalia mahitaji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine sisi watu wenye ulemavu tunaona ni afadhalii basi likisimama porini tunaona tuko salama zaidi kuliko kwenda kusimama katika maeneo hayo ambayo ni vyoo vinavyotumiwa na wenzetu wote. Kwa mfano, mtu mwenye ulemavu anayetambaa wakati mwingine utakuta nguo zake zimelowa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, sina haja ya kushika mshahara wake. Ninachoomba tu aniridhishe na tuone ni kwa jinsi gani tunajali kundi hili. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naona ameshasimama lakini kwa maelezo aliyokuwa ametoa mwanzo nadhani ameshatoa *commitment* ya TAMISEMI. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Nataka nimwongezee.

**MWENYEKITI:** Umwongezee *commitment?* (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Ndiyo.

16 APRIL, 2018

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishatoa maelezo haya lakini kwa sababu Mheshimiwa Amina Mollel ameenda mbali maana yake siyo katika ile miundombinu inayojengwa na Serikali peke yake ni hata katika maeneo mengine. Jambo kubwa ni kwamba niwaelekeze Wakuu wa Mikoa wote ambao miundombinu mbalimbali inajengwa katika maeneo yao katika taasisi zote wasimamie kuhakikisha mahitaji ya watu wenye ulemavu yanazingatiwa katika mikoa yao ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa tutaendelea na nitawahoji kuhusiana na kifungu hiki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 - *Finance and Accounts Unit* ..... Sh. 665,927,000/=  
Kif.1003 – *Policy and Planning Division* .....Sh. 908,339,927/=  
Kif.1004 - *Information, Communication and Technology Division*.....Sh.2,824,486,000/=  
Kif. 1005 – *Legal Services Division*.....Sh.558,227,000/=  
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit*.....Sh..352,996,000/=  
Kif. 1007 – *Government Comm. Unit* .....Sh.321,744,000/=  
Kif. 1008 – *Procurement Mgt. Unit* .....Sh.392,584,000/=  
Kif. 1009 – *Infrastructure Dev. Div.* .....Sh.2,481,924,653/=  
Kif. 2001 – *Regional Administration* .....Sh.550,364,728/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Local Government Division* ....Sh.15,359,901,565/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba ufanuzi kwenye

16 APRILI, 2018

kifungu kidogo 22001. Katika mwaka wa fedha tunaoumalizia walitenga shilingi milioni 12 lakini sasa hivi Wizara hii inaomba bilioni tano, kuna ongezeko kubwa sana la fedha kwenye kifungu hiki. Kwa nini kuna ongezeko hilo kubwa kwa kiwango hiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ametaja kifungu 2200, ukurasa wa 349. Mheshimiwa Mbunge anasema kuna ongezeko kubwa sana hapo la takriban shilingi bilioni tano tuseme. Ufanuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo limetokana na suala zima la maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi niko katika *subvote* 2002, *Local Government Division* lakini niko kwenye 22010, *travel – in - country* ambapo katika mwaka uliopita 2017/2018 kulikuwa na shilingi milioni 71 sasa kuna shilingi bilioni 4,082,990,000/=. Kwa mujibu wa randama maelezo yanasema fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kugharamia watumishi watakaosafiri ndani ya nchi kikazi na kuratibu maandalizi ya shughuli za uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kuna ongezeko la shilingi bilioni nne na milioni kumi na moja na mnasema kwamba mnaenda kugharamia watumishi watakaosafiri ndani ya nchi kuratibu maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inakuja kwa mujibu wa CAG anasema kwamba katika maeneo haya ndiyo ambapo ujisadi ni mkubwa na haoni dalili kwamba mnadhibiti fedha hizi. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo inaonesha kuna wizi, ubadhira na ujisadi katika maeneo ya uchaguzi Serikali za Mitaa unajipangaje kukomesha ujisadi huo na wizi na ubadhira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

16 APRIL, 2018

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hivi ni TAMISEMI ndiyo mmepeata asilimia 90 ya hati...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Ndiyo, ya hati safi.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenisaidia katika kujibu. Katika maeneo ambayo kumekuwa na *improvement* kubwa sana ni pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI, udhibiti umekuwa wa kiwango cha hali ya juu. Pia nimwambie Mheshimiwa mjumbe ujisadi hautokani na bajeti, ujisadi unatokana na *expenditure*. Pale unapoenda kutumia ndipo ambapo unaweza ukasema hiki sio sahihi, kwa hiyo vifungu viko vizuri.

(*Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadilliko yoyote*)

Kif. 2003 – Sector Coordination Division .....Sh.771,901,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *subvote* 2003, kifungu kidogo 21121, *personal allowance in-kind*. Mwaka 2016/2017 ilitengwa Sh.9,903,919 tumeona pia imeendelea kutengwa 2017/2018, lakini hapa inaonesha kwamba imepungua. Sasa tunataka kufahamu kwa nini imepunguzwa kiasi hiki kwamba hakuna tena hizo *persons in-kind* au watu waliokuwa wanafadhalika wamendolewa pale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cecil Mwambe nimemwelewa. Ni kwamba eneo hilo

16 APRILI, 2018

litashughulikiwa na eneo la utawala (*administration*). Kwa hiyo, hilo jambo litafanyika lakini kwa kutegemea sehemu ya utawala, kwa hiyo, hakuna shaka yoyote.

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnapohojiwa ni lazima mjibu kwa sababu tunapata kumbukumbu kwamba mlifikali ama mlikataa.

Kif. 2004 – *Basic Education Coordination Division* .....Sh.11,811,158,735/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nipate ufanuzi kwenye kifungu hicho 2004. Mwaka 2016/2017 subvote 22008, *Training – Domestic* iliwekwa shilingi sifuri na 2017/2018 pia ilikuwa sifuri lakini mwaka huu imewekwa shilingi milioni 12. Hapa tumezungumza suala la kufanya mafunzo na tunavyojuua sisi mafunzo kwa Walimu kule yanaanza ngazi ya Wizara watu wanapewa *training then wanashuka kule chini shule za sekondari na shule za msingi kuwafanya wale wengine induction*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kiwango hiki kilichowekwa naomba nipate ufanuzi kama kweli kinakidhi kufanya *training* pale Wizarani na baadaye kushuka kule shule za msingi na sekondari ili Walimu wetu ambao wamehamishwa kutoka shule za sekondari kwenda shule za msingi waweze kufanyiwa *training*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

16 APRIL, 2018

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu limekuwa likisisitiza kwamba ni vizuri tukajihakikishia ubora wa elimu lakini ubora wa elimu ni pamoa na kuwafundisha hawa ambao wanaenda kusimamia. Kwa hiyo, eneo hili limewekewa mkazo ili tuhakikishe kwamba wanapata elimu na mafunzo ya kutosha ili kwenda kuhakikisha hiki anachokisema Mheshimiwa kinakuwa katika hali nzuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nahitaji kupata ufanuzi katika *subvote* 26311, *extra-budgetary accounts and funds cash* ambayo mwaka uliopita ilitengewa shilingi bilioni 11 na sasa inaombewa shillingi bilioni 10, kuna upungufu. Naflkiri kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya elimu bure kama nitakuwa sijakosea na kama ndivyo, naomba nipate ufanuzi kama mwaka uliopita kulikuwa na *deficit* kubwa kwa fedha za walanzi, maji, umeme na tumekuwa tukiomba ule waraka urekebishwe ili hizi fedha ziwe *accommodated*. Ni kwa nini fedha hizi zimepungua na ni kwa kiasi gani yale ambayo tumekuwa tukisema katika Waraka wa Elimu bure yamewekwa katika fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu huu pia umetokana na baadhi ya watumishi ambao wanastaifu lakini pia kama hilo halitoshi hili zoezi zima la uhakiki wa vyeti kuna baadhi ya watumishi ambao wamepungua ndiyo maana unaona fungu hili fedha zimepungua.

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

16 APRILLI, 2018

Kif. 2005 – *Urban Development Division*.....Sh.790,505,392/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2006 – *Inspectorate and Finance Tracking Unit* .....Sh. 423,508,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nimepata mashaka hapa kwenye 2006 kwenye *travel-in-country*. Mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni 40, lakini mwaka huu imekwenda shilingi 146. Sasa ongezeko hili ni kubwa sana na haya mambo ya *inspection and finance tracking* ni mambo ya kawaida ambayo yanafanyika kila mwaka tulitegemea yawe na *consistency* fulani hivi na siyo ya *ku-shoot* kiasi hiki. Kwa hiyo, naomba kupata maelezo kwa nini ime-shoot kwa kiasi kikubwa hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri umepaona hapo? Ukurasa wa 350, Mheshimiwa Naibu Waziri ufanuzi.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko kubwa hili msingi wake ni pale nilipoanza kuelezea juu ya suala zima la kwenda kufanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na sisi tumekuwa mashuhuda watu wamekuwa wakisema kwamba ni vizuri watu wetu wakapewa elimu ya uraia. Kwa hiyo ita-entail maafisa wengi kusafiri kwa ajili ya kwenda kutoa elimu hiyo, ndio maana fungu hilo limeongezeka.

(*Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2007 – *Health, Social, Welfare and Nutrition Services* .....Sh.376,320,000/=

Kif.3001 – *Mngnt Serv. Improvement Unit*.....Sh.501,455,000/=

16 APRIL, 2018

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiiliko yoyote*)

## Fungu 2 – Tume ya Utumishi wa Walimu

Kif. 1001 – *Administration and HR Mngt.....Sh.2,370,315,342/=*

(*Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiiliko yoyote*)

Kif. 2001 – *Recruitment and Dev. Division....Sh.1,586,168,146/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko hapo kwenye *subvote* 2001, *item* 22014 ambapo *hospitality supplies and services* kwa mwaka uliopita kulikuwa kuna sifuri sasa kuna Sh.101,615,000/= na maelezo mara nyingi inakuwa kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya takrima, vitafunwa, mambo matamu matamu ya chakula na yale ya mfanyakazi bora. Mtuambie mnataka kula nini mwaka huu? Ongezeko la shilingi milioni 100, mnataka kula vitamu gani mwaka huu? Je, mna mfanyakazi gani bora mtakayempa fedha hii zaidi? Hebu tuwekeni wazi tufahamu maana hamsomeki. Naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hicho ana-*compare* na bajeti ya mwaka jana na tufahamu hii ni Tume ya Walimu na Tume hii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ilikuwa haijaanza kuweka matawi yake kule. Kwa hiyo, hii maana yake ni mgawanyo wa halmashauri zote 185 katika maeneo yetu maana hata hivyo bajeti hii bado imebana sana kutokana na uhalsia ulivyo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiiliko yoyote*)

16 APRIL, 2018

Kif. 2002 – *Teachers Service Commission – District.....Sh. 8,558,776,512/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nipate ufanuzi *subvote 21114 ambayo inasema personal allowances (discretionary) – optional* ambayo mwaka jana na mwaka juzi ilikuwa shilingi sifuri kabisa na mwaka huu ni shilingi milioni 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni kifungu kile cha *Teachers Service Commission* katika ngazi ya wilaya (*district level*) kwa maana ya kwamba tunahitaji viwe vinakaa vikao vya mara kwa mara kwa sababu Walimu wana matatizo ya mara kwa mara ili kuweza kupitisha madaraja ya Walimu lakini pesa zilizotengwa hapa shilingi millioni 23 naona ni pesa ndogo sana. Kwa hiyo, naomba nipate ufanuzi kwamba kiwango hiki cha pesa kama kweli kinakidhi haja kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOANA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachosema Mheshimiwa Maftaha, mwaka jana tulikuwa tuna sifuri mwaka huu tumetenga shilingi milioni 23. Tunajua japo haitoshi lakini kutokana na ukomo wa bajeti hapo ndiyo tulipofikia angalau tuwe na kitu cha kuanzia hivi sasa. Kwa hiyo, tulitamani sana hata iwe shilingi milioni 80 lakini kutokana na ukomo wa bajeti tunaanza na hiyo kwa kadiri tunavyokwenda basi bajeti hii itakuwa inaongezeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba nipate ufanuzi katika

16 APRIL, 2018

kifungu kidogo cha 22014, *hospitality, supplies and services*. Mwaka uliopita tulitenga shilingi milioni moja na sasa hivi Wizara inaomba shilingi milioni 200. Kuna ongezeko kubwa sana kwenye kasma hiyo, kwa hiyo, tunaomba ufanuzi ongezeko hili ni la nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo ofisi zetu zilikuwa bado hazija-*function* katika halmashauri zetu kule wilayani, lakini kwa mwaka huu wa fedha sasa tunategemea ofisi hizi zitasikiliza matatizo mengi sana kuhusu walimu. Kwa sababu watateuliwa wale Makatibu katika wilaya ndiyo maana unaona kifungu hiki sasa hivi kinaenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli katika mwaka wa fedha uliopita hali yao ilikuwa mbaya sana. Kwa hiyo, huu ni uhalisia jinsi gani wataweza kufanya kazi katika maeneo ya halmashauri zote 184 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hukusimama mwanzo, kwa hivyo, tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 104 tunaingia kwenye utaratibu wa kuitisha mafungu yote kwa pamoja, Katibu.

## **MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MIKOA**

### **Fungu 36 - Mkoa wa Katavi**

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Mngt.....</i>	Sh.2,127,701,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Account.....</i>	Sh.52,450,000/=
Kif. 1003 – <i>Internal Audit Unit.....</i>	Sh.62,260,000/=

Kif. 1004 – <i>Procurement Management</i> .....	Sh.13,872,000/=
Kif. 1005 – <i>DAS – Mpanda</i> .....	Sh.200,408,000/=
Kif. 1006 – <i>DAS – Mlele</i> .....	Sh.154,869,000/=
Kif. 1007 – <i>DAS – Tanganyika</i> .....	Sh.142,611,000/=
Kif. 1014 – <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh.20,393,000/=
Kif. 1015 – <i>Information and Communication Tech. Unit</i> .....	Sh.9,015,000/=
Kif. 2001 – <i>Planning and Coordination</i> .....	Sh.97,888,000/=
Kif. 2002 – <i>Economic and Productive Sector</i> .....	Sh.66,318,000/=
Kif. 2003 – <i>Infrastructure Sector</i> .....	Sh.30,225,000/=
Kif. 2005 – <i>Local Gov. Management Services</i> .....	Sh.98,920,000/=
Kif. 2006 – <i>Education Sector</i> .....	Sh.148,333,000/=
Kif. 2007 – <i>Water Services</i> .....	Sh.18,950,000/=
Kif. 3001 – <i>Regional Hospital</i> .....	Sh.354,322,000/=
Kif. 8075 – <i>Transfers to LGAS – Primary Education</i> .....	Sh.22,166,833,000/=
Kif. 8076 – <i>Transfers to LGAS – Secondary Education</i> .....	Sh. 9,381,280,000/=
Kif. 8077 – <i>Transfers to LGAS – Land Dev. &amp; Urban Planning</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8078 – <i>Transfers to LGAS – Public Health Services</i> .....	Sh. 8,163,967,000/=
Kif. 8079 – <i>Transfers to LGAS – Preventive Services</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8080 – <i>Transfers to LGAS – Health Centres</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8081 – <i>Transfers to LGAS – Dispensaries</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8082 – <i>Transfers to LGAS – Works</i> .....	Sh.798,331,000/=
Kif. 8083 – <i>Transfers to LGAS – Rural Water Supply</i> .....	Sh.518,944,000/=
Kif. 8084 – <i>Transfers to LGAS – Natural Resources</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8085 – <i>Transfers to LGAS – Community Dev Gender&amp;Children</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8086 – <i>Transfers to LGAS-Agriculture</i> ...	Sh.2,210,348,000/=
Kif. 8087 – <i>Transfers to LGAS – Livestock Operations</i> ....	Sh.0/=
Kif. 8088 – <i>Transfers to LGAS – Water Supply</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8090 – <i>Transfers to LGAS – Internal Audit Unit</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8091 – <i>Transfers to LGAS – Administration &amp;General</i> .....	Sh.13,547,335,000/=

16 APRIL, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunapotumia utaratibu huu twende haraka kidogo, kwa hiyo, tuwe tunaenda na Katibu anavyoenda.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 47- Mkoa wa Simiyu

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Mngnt.....</i>	Sh.641,520,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Account Unit .....</i>	Sh. 166,536,000/=
Kif. 1003 – <i>Internal Audit Unit.....</i>	Sh.86,300,000/=
Kif. 1004 – <i>Procurement Management Unit....</i>	Sh.29,920,000/=
Kif. 1005 – <i>DAS – Baria.....</i>	Sh.328,236,000/=
Kif. 1006 – <i>DAS – Maswa.....</i>	Sh.334,661,000/=
Kif. 1007 – <i>DAS – Meatu.....</i>	Sh.304,267,000/=
Kif. 1008 – <i>DAS – Busega.....</i>	Sh.271,167,000/=
Kif. 1009 – <i>DAS – Itilima.....</i>	Sh.296,947,000/=
Kif. 1014 – <i>Legal Service Unit.....</i>	Sh.68,060,000/=
Kif. 1015 – <i>Information and Communication Tech. Unit.....</i>	Sh.36,400,000/=
Kif. 2001 – <i>Planning and Coordination.....</i>	Sh.249,836,000/=
Kif. 2002 – <i>Economic and Productive Sector.....</i>	Sh.270,368,000/=
Kif. 2003 – <i>Infrastructure Sector.....</i>	Sh.212,004,000/=
Kif. 2004 – <i>Social Sector.....</i>	Sh.163,000,000/=
Kif. 2005 – <i>Local Government Management Services.....</i>	Sh.128,600,000/=
Kif. 2006 – <i>Education Sector.....</i>	Sh.390,599,000/=
Kif. 2007 – <i>Water Sector.....</i>	Sh.100,380,000/=
Kif. 3001 – <i>Regional Hospital.....</i>	Sh.1,248,890,000/=
Kif. 8075 – <i>Transfers to LGAS – Primary Education.....</i>	Sh.61,061,538,000/=
Kif. 8076 – <i>Transfers to LGAS – Secondary Education.....</i>	Sh.23,971,193,000/=
Kif. 8078 – <i>Transfers to LGAS – Public Health Services.....</i>	Sh.5,126,342,000/=
Kif. 8079 – <i>Transfers to LGAS – Preventive Services.....</i>	Sh.2,287,759,000/=
Kif. 8080 – <i>Transfers to LGAS – Health</i>	

16 APRILLI, 2018

<i>Centre</i> .....	Sh.4,096,114,000/=
Kif. 8081 – <i>Transfers to LGAS – Dispensaries</i> .....	Sh.4,225,373,000/=
Kif. 8082 – <i>Transfers to LGAS – Works</i> .....	Sh.1,102,774,000/=
Kif. 8083 – <i>Transfers to LGAS – Rural Water Supply</i> .....	Sh.868,996,000/=
Kif. 8086 – <i>Transfers to LGAS-Agriculture</i> ...	Sh.3,135,309,000/=
Kif. 8087 – <i>Transfers to LGAS – Livestock Operations</i> .....	Sh.2,334,826,000/=
Kif. 8091 – <i>Transfers to LGAS – Administration &amp; General</i> .....	Sh.19,588,800,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### Fungu 54 - Mkoa wa Njombe

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Mngnt</i> ...Sh.1,020,092,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Account Unit</i> .....Sh.151,977,000/=
Kif. 1003 – <i>Internal Audit Unit</i> .....Sh.67,124,000/=
Kif. 1004 – <i>Procurement Management Unit</i> ...Sh.48,506,000/=
Kif. 1005 – <i>DAS – Njombe</i> .....Sh.331,330,200/=
Kif. 1006 – <i>DAS – Makete</i> .....Sh.326,877,200/=
Kif. 1007 – <i>DAS -Ludewa</i> .....Sh.369,937,400/=
Kif. 1008 – <i>DAS – Wanging’ombe</i> .....Sh.273,599,000/=
Kif. 1014 – <i>Legal Service Unit</i> .....Sh.48,644,000/=
Kif. 1015 – <i>Information and Communication Tech. Unit</i> .....Sh.45,107,000/=
Kif. 2001 – <i>Planning and Coordination</i> .....Sh.137,902,000/=
Kif. 2002 – <i>Economic and Productive Sector</i> .....Sh.208,987,000/=
Kif. 2003 – <i>Infrastructure Sector</i> .....Sh.129,850,000/=
Kif. 2004 – <i>Social Sector</i> .....Sh.114,699,000/=
Kif. 2005 – <i>Local Government Management Services</i> .....Sh.94,266,000/=
Kif. 2006 – <i>Education Sector</i> .....Sh.376,023,000/=
Kif. 2007 – <i>Water Services</i> .....Sh.76,287,000/=
Kif. 3001 – <i>Regional Hospital</i> .....Sh.1,054,483,200/=
Kif. 8075 – <i>Transfers to LGAS – Primary Education</i> .....Sh.42,830,692,000/=

16 APRIL, 2018

Kif. 8076 – <i>Transfers to LGAS – Secondary Education</i> .....	Sh.30,907,510,050/=
Kif. 8077 – <i>Transfers to LGAS – Land Dev. &amp; Urban Planning</i> .....	Sh.64,094,000/=
Kif. 8078 – <i>Transfers to LGAS – Public Health Services</i> .....	Sh.4,491,038,000/=
Kif. 8079 – <i>Transfers to LGAS – Preventive Services</i> .....	Sh.2,408,674,000/=
Kif. 8080 – <i>Transfers to LGAS – Health Centres</i> .....	Sh.3,896,990,000/=
Kif. 8081 – <i>Transfers to LGAS – Dispensaries</i> .....	Sh.8,099,041,000/=
Kif. 8082 – <i>Transfers to LGAS – Works</i> .....	Sh.1,395,267,000/=
Kif. 8083 – <i>Transfers to LGAS – Rural Water Supply</i> .....	Sh.916,665,000/=
Kif. 8084 – <i>Transfers to LGAS – Natural Resources</i> .....	Sh.24,341,000/=
Kif. 8085 – <i>Transfers to LGAS – Comm Dev Gender&amp;Children</i> .....	Sh.34,289,000/=
Kif. 8086 – <i>Transfers to LGAS–Agriculture</i> ...	Sh.1,742,569,000/=
Kif. 8087 – <i>Transfers to LGAS – Livestock Operations</i> .....	Sh.1,813,884,000/=
Kif. 8088 – <i>Transfers to LGAS – Water Supply</i> .....	Sh.0/=
Kif. 8089 – <i>Transfers to LGAS – Planning, Trade&amp;Economy</i> .....	Sh.32,824,000/=
Kif. 8090 – <i>Transfers to LGAS – Internal Audit Unit</i> .....	Sh.32,823,000/=
Kif. 8091 – <i>Transfers to LGAS – Administration&amp;General</i> ....	Sh.16,397,956,950/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiiliko yoyote)

### Fungu 63 - Mkoa wa Geita

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i> .....	Sh.850,514,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Account Unit</i> .....	Sh.172,134,000/=
Kif. 1003 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.48,466,000/=
Kif. 1004 – <i>Procurement Management</i>	

<i>Unit.....</i>	Sh.103,131,000/=
Kif. 1005 – <i>DAS -Geita</i> .....	Sh.300,019,000/=
Kif. 1006 – <i>DAS - Bukombe</i> .....	Sh.310,915,200/=
Kif. 1007 – <i>DAS - Chato</i> .....	Sh.304,716,000/=
Kif. 1008 – <i>DAS - Nyang'wale</i> .....	Sh.332,905,000/=
Kif. 1009 – <i>DAS - Mbogwe</i> .....	Sh.301,109,000/=
Kif. 1014 – <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh.35,002,000/=
Kif. 1015 – <i>Information and communication</i>	
<i>Tech. Unit</i> .....	Sh.72,361,000/=
Kif. 2001 – <i>Management Support</i> .....	Sh.193,542,000/=
Kif. 2002 – <i>Economic and Development</i>	
<i>Support</i> .....	Sh.289,384,000/=
Kif. 2003 – <i>Infrastructure Section</i> .....	Sh.155,250,000/=
Kif. 2004 – <i>Social Sector</i> .....	Sh.132,739,000/=
Kif. 2005 – <i>Local Government Management</i>	
<i>Service</i> .....	Sh.196,344,000/=
Kif. 2006 – <i>Education Sector</i> .....	Sh.510,364,000/=
Kif. 2007 – <i>Water Sector</i> .....	Sh.102,813,000/=
Kif. 3001 – <i>Regional Hospital</i> .....	Sh.1,096,972,283/=
Kif. 8075 – <i>Transfers to LGAS – Primary</i>	
<i>Education</i> .....	Sh.73,397,137,712/=
Kif. 8076 – <i>Transfers to LGAS – Secondary</i>	
<i>Education</i> .....	Sh.36,034,235,507/=
Kif. 8077 – <i>Transfers to LGAS – Land Dev.</i>	
<i>&amp; Urban Planning</i> .....	Sh.116,280,000/=
Kif. 8078 – <i>Transfers to LGAS – Public Health</i>	
<i>Services</i> .....	Sh.7,431,500,943/=
Kif. 8079 – <i>Transfers to LGAS – Preventive</i>	
<i>Services</i> .....	Sh.1,948,604,344/=
Kif. 8080 – <i>Transfers to LGAS – Health</i>	
<i>Centres</i> .....	Sh.5,268,987,906/=
Kif. 8081 – <i>Transfers to LGAS-</i>	
<i>Dispensaries</i> .....	Sh.5,240,419,911/=
Kif. 8082 – <i>Transfers to LGAS – Works</i> .....	Sh.921,652,887/=
Kif. 8083 – <i>Transfers to LGAS – Rural Water</i>	
<i>Supply</i> .....	Sh.679,696,684/=
Kif. 8084 – <i>Transfers to LGAS – Natural</i>	
<i>Resources</i> .....	Sh.196,000,000/=
Kif. 8085 – <i>Transfers to LGAS – Comm Dev</i>	
<i>Gender&amp;Children</i> .....	Sh.331,996,516/=

16 APRIL, 2018

Kif. 8086 – <i>Transfers to LGAS-Agriculture</i> ...Sh.2,727,122,691/=
Kif. 8087 – <i>Transfers to LGAS – Livestock Operations</i> .....Sh.1,684,465,141/=
Kif. 8089 – <i>Transfers to LGAS – Planning, Trade&amp;Economy</i> .....Sh.996,702,900/=
Kif. 8090 – <i>Transfers to LGAS – Internal Audit Unit</i> .....Sh.122,800,000/=
Kif. 8091 – <i>Transfers to LGAS – Administration&amp;General</i> ....Sh.21,097,303,375/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiiliko yoyote)*

### **Fungu 70 - Mkoa wa Arusha**

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i> .....Sh.1,608,647,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....Sh.150,164,000/=
Kif. 1003 – <i>Internal Audit Unit</i> .....Sh.72,126,000/=
Kif. 1004 – <i>Procurement Management Unit</i> .Sh.110,996,000/=
Kif. 1005 – <i>DAS – Arusha</i> .....Sh.279,334,000/=
Kif. 1006 – <i>DAS – Ngorongoro</i> .....Sh.267,323,000/=
Kif. 1007 – <i>DAS – Karatu</i> .....Sh.346,506,400/=
Kif. 1008 – <i>DAS – Arumeru</i> .....Sh.298,255,000/=
Kif. 1009 – <i>DAS – Monduli</i> .....Sh.392,945,400/=
Kif. 1010 – <i>DAS – Longido</i> .....Sh.286,780,200/=
Kif. 1014 – <i>Legal Service Unit</i> .....Sh.6,367,000/=
Kif. 1015 – <i>Information and Communication Tech. Unit</i> .....Sh.13,324,000/=
Kif. 2001 – <i>Planning and Coordination</i> .....Sh.208,775,000/=
Kif. 2002 – <i>Economic and Productive Sector</i> .....Sh.345,357,000/=
Kif. 2003 – <i>Infrastructure Sector</i> .....Sh.195,612,000/=
Kif. 2005 – <i>Local Govt. Management Services</i> .....Sh.191,480,000/=
Kif. 2006 – <i>Education Sector</i> .....Sh.420,998,000/=
Kif. 2007 – <i>Water Sector</i> .....Sh.27,020,000/=
Kif. 3001 – <i>Regional Hospital</i> .....Sh.6,530,644,000/=
Kif. 8075 – <i>Transfers to LGAS – Primary Education</i> .....Sh.74,990,056,000/=

16 APRIL, 2018

Kif. 8076 – <i>Transfers to LGAS – Secondary Education</i> .....	Sh.56,265,948,000/=
Kif. 8078 – <i>Transfers to LGAS – Public Health Services</i> .....	Sh.7,058,414,000/=
Kif. 8079 – <i>Transfers to LGAS – Preventive Services</i> .....	Sh.4,749,579,000/=
Kif. 8080 – <i>Transfers to LGAS – Health Centres</i> .....	Sh.8,414,252,000/=
Kif. 8081 – <i>Transfers to LGAS – Dispensaries</i> .....	Sh.6,216,588,000/=
Kif. 8082 – <i>Transfers to LGAS – Works</i> .....	Sh.1,655,737,000/=
Kif. 8083 – <i>Transfers to LGAS – Rural Water Supply</i> .....	Sh.1,105,603,000/=
Kif. 8086 – <i>Transfers to LGAS–Agriculture</i> ...Sh.4,214,062,000/=	
Kif. 8087 – <i>Transfers to LGAS – Livestock Operations</i> .....	Sh.3,847,239,000/=
Kif. 8088 – <i>Transfers to LGAS – Water Supply</i> .....	Sh.8,042,000/=
Kif. 8091 – <i>Transfers to LGAS – Administration &amp;General</i> .....Sh.32,194,512,000/=	

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 71 - Mkao wa Pwani**

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Ruth Mollel mtoa hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za nchi zinasema ukisha-forge/ukishaghushi inatosha wewe kukufikisha Mahakamani, kosa la jinai. Serikali hiyo hiyo kwa sababu ni Serikali sikiu ikasema hatuwapeleki Mahakamani tunawasamehe na msamaha huo umetangazwa na Serikali kwamba wale watu wamesamehewa. Sasa akishakuwa mtu

ametenda kosa na ukamsamehe, nilidhani kwamba ni muda wa kupongezana Serikali hii ina huruma kwa sababu kwa mujibu wa sheria za nchi huwezi ukaendelea na ajira ya mtu ambaye hana sifa kwa cheo kile. Wameachishwa kwa sababu hawapaswi kuwepo pale, waliwepo pale kwa sababu ya kughushi, unapowabakiza na kuwapa mafao maana yake ni kwamba hata maana yenyewe ya mafao inapotea. Mafao ile wazungu wanaita *award*, unamu-*award* mtu kwa maana ameheshimu mkataba, mmeefanya naye kazi vizuri, dhamira ya *fact* kwamba yule mtu amefanya kazi kwa mkataba feki ambao ni *illegal* hivi ku-*award* unaanzia wapi. Unamu-*award* mtu ambaye ameingia pale kimakosa. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba Serikali hii ni sikivu ilitakiwa wapelekwe Mahakamani, Serikali imeona kwamba itoe msamaha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watumishi wamekuwa wanakatwa kodi, hawa watumishi wamefanya kazi miaka mingi katika Serikali, hawa watumishi wamekuwa wanakatwa Hifadhi ya Jamii. Mimi na hakika kabisa hii Serikali sikivu kuwatoa hao tunaita *with a human face. A human face* ya kuangalia siyo tu wale watumishi lakini watu wengine wote wanaowategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili lazima na Serikali nayo ikubali kwamba imehusika kwa namna moja au nyingine kwa sababu ya kutokuwa na mfumo thabiti wa kuhakiki na kuhakikisha vyeti feki havitembe katika Utumishi wa Umma, kwa hiyo, naomba hili jambo lijadiliwe liweze kupata michango ya watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja Ilitolewa lamuliwe*)

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa

Abdallah Mtalea na Mheshimiwa James. Uwiano uko mwingi kweli hapa nakumbushwa hadi *gender*, wengine si mlisimama kuunga mkono hoja. Tutulie basi tuwasikilize wenzetu. Ahsante sana, tutaanza na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nilitaka nipate *clarity* kwa sababu naona liko tatizo la *clarity* hapa. Kuna watu walijiriwa *before 2004* hawa walijiriwa wakiwa darasa la saba, wako Wakunga, Wenye viti wa Vijiji, madereva pale kada ndogo ndogo wauguzi walijiriwa *clearly* wakiwa ni darasa la saba. Baada ya mwaka 2004 ukaja waraka kwamba sasa lazima watu wawewe ku-*upgrade* wawe na cheti cha *form four*. So mimi nawaongelea hawa *pre-2004*. Wale walioajiriwa baada ya mwaka 2004 masharti yanajulikana ilikuwa lazima uwe *form four* ama usome umalize, sasa hawa wa *pre-2004* ambao kwa kweli wameajiriwa muda mrefu na ile kazi wamefanya mtu kama ni dereva hivi *form four* inaongoza nini kuwa dereva? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *so issue* yangu ni hawa wa *pre-2004* naomba Waziri atupe *clarity* ya hawa watu walioajiriwa *before 2004* na walijiriwa kwa sifa za kuwa darasa la saba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Serukamba hiyo naona ni hoja mpya, kwa sababu hoja ya mtoha hoja ni tofauti na hiyo unayoizungumzia wewe, kwa maana hiyo nitaita mtu mwingine hapo baadae kwenye nafasi yako. Mheshimiwa Abdallah Mtalea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ruth Mollel na hii ni kwa sababu mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mtu kuajiriwa akiwa na vyeti *fake* linasababishwa na mfumo mbovu wa ajira, kwa sababu kuajiri ni *process* yaani mtu anapita kwenye mchakato wa kumfanyia *screening* mpaka taasisi ijiridhishe

kwamba huyu mtu yuko safi. Taasisi kwa maana ya Serikali ilikuwa na mifumo mibovu ambayo watu wenyewe vyeti *fake walipita* na wale watu wakafanya kazi na kwenye kufanya kazi mtu hafanyi kazi peke yake anafanya kazi akiwa anasimamiwa, wanafanyiwa *performance appraisal*, wanaonekana wanafaa, wanalipwa mishahara, wanapandishwa vyeo, leo kama tumeiboresha mifumo yetu na tumegundua kuna watu waliingia vibaya hatuwezi kuwafukuza namna hiyo, ni lazima tuangalie namna gani tunawapa angalau ka-*gratuity* ili waondoke nacho kwa sababu na ninyi mmewatumia. Huwezi ukaukataa ukweli kwamba hawa watu hamjawatumia, hawa watu tumewatumia tena walikuwa wafanyakazi waadilifu kweli kweli kuliko wenyewe vyeti sahihi. (*Makofii*)

Sasa leo tusitumie kichaka hiki cha kukosa fedha za kuwalipa watu tukaondoka na haki za watu, hebu tuwe binadamu kidogo jamani. Tuwaangalie hawa Watanzania ambao walilitumikia Taifa hili kwa nguvu zao zote japo hawakuwa na vyeti. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa James Millya.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya elimu yetu ni kwamba lazima tutambue *certificates* tu, lakini mara nyingi mtu anaingia kazini na anajifunza akiwa kazini, lakini *system* za Serikali hii haiwezi kumtambua wakati anaendelea kutumikia hiyo ajira yake. Ni muda muafaka na ukijaribu ukiangalia inawezekana ninyi mlipata sifa kwa sababu ya watumishi hawa wenyewe familia, wenyewe watu wanaowategemea, lakini kwa sasa mnaanza kuwa-*dump* tu kama vile kile kitu ambacho sitaki kikitaja hapa kwa sababu ya watoto.

Lakini niseme hivi watu hawa wametumia muda mwingi kutumikia Serikali, wamejifunza na wana uwezo wa hali ya juu na inawezekana hata siku moja hawajapewa *warning letter* kwamba ninyi hamuwezi kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, nafikiri ni vyema Serikali na ninyi muwe kama wazazi, mkirii kwamba mmefanya makosa kuwaajiri kwanza

na vyeti *fake*, lakini baadae ninyi mnataka kuwaachia mzigopeke yao. Ninyi ni wakati sahihi na ninyi mkiri makosa kama Serikali kwamba tuliwaajiri, lakini watu hawa wamekuwa wabobezi inawezekana. Kumbukeni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Serikali kwa sababu kwanza Waziri alitoa tamko hapa Bungeni mapema wiki iliyopita na tamko lile liliweka *clarity* juu ya nani ambaye anahusika na mpango huu wa Serikali na nani hahuksiki. Pia naunga mkono hoja yake kwa wale ambaao walikuwa wame-forge vyeti kwa sababu sikubaliani na utaratibu wa kuendekeza watu ambaao wanaghushi vyeti wakae kwenye ofisi za umma kwa sababu hata kama ingekuwa ni ofisi yangu binafsi ni jambo ambalo nisingelikubali. Naamini mtu yejote yule *conscious* hawezi kukubali kulipa mishahara wakati akitambua kabisa kwamba cheti cha mtumishi aliyemuajiri ni cheti cha kughushi kwa maana hiyo ana ujuzi hafifu na ujuzi wenywewe siyo *based* kwenye *acredentials* alizoziwasilisha wakati akiajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ninaunga mkono hoja ya Serikali kwamba ni jambo lisiloyumkinika kwa mtu msomi tena aliyewahi kuwa mwajiri kupigia chepuo kwamba watu ambaao walighushi vyeti waruhusiwe kubaki katika mfumo rasmi wa Serikali. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naomba tu nitoe mfano mdogo labda na Mheshimiwa Waziri ataliangalia hili kwa jicho lingine jinsi ambavyo huu waraka unavyoleta mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UDOM*nafikiri ilianza 2007 na kuna baadhi ya wafanyakazi wamekosa ajira zao zaidi ya 40 ambao wana cheti cha darasa la saba na ni madereva, sasa hawa wana-base wapi kwa sababu wamekosa ajira na mafao yao na walijiriwa kihalali na walipata hii ajira baada ya huu waraka kutoka. Naomba Waziri aliangalie hilo na aone kwamba hii *situation* inaleta mkanganyiko kiasi gani, ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja ya Mheshimiwa Ruth Mollel ambaye tunamuheshimu sana, kwanza ningeomba kama inawezekana Wabunge wote uruhusu tusimame kwa dakika moja kuwakumbuka Watanzania wenzetu ambao walikufa kutokana na kuhudumiwa pengine na walikuwa wame-forge vyeti wakidhani ni madaktari na wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mleta hoja mwenyewe alikuwa Katibu Mkuu - Utumishi na haya mambo aliyabariki na aliyatengeneza yeye, lakini kana kwamba haitoshi anakuja Bungeni kuwatetea watu kama hao tena. Hili sio gereza, nchi sio gereza ambako wafungwa wanasmehewa halafu wanapewa nauli ya kurudi majumbani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu anaposema tuwe na *human face*, *human face* ndio ambayo Mheshimiwa Rais ameionesha kwamba ninyi mmejipatia ulaji kwa miaka mingi, lakini sasa nendeni nyumbani sitawapeleka mahakamani. Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Ruth Mollel, ili kuficha aibu ambayo imetengenezwa na mifumo mibovu ambayo yeye alikuwa ni Katibu Mkuu, hoja hii aikatae hapa hapa na atoe kauli yake vinginevyo itamvuruga na kumuaibisha mbele ya jamii... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nipende tu kuungana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ukiangalia katika Kanuni za Adhabu Sura ya 16 suala hili ni kosa la jinai, lakini vilevile ukiangalia hata mkataba wenyewe wa ajira ambao unakuwa *referred to tangu mwanzo hata kama mkataba uliingiwa ni null and void ab initio*. Kwa hiyo, yaani hatuwezi kabisa kuhalalisha suala hili kwa kusema tu kwamba mtu alikuwa ameingia mkataba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea hata katika mfano, mfano kulikuwa kuna wizi huwezi ukasema eti kwa sababu mtu alikuwa akikuibia eti umsamehe kwa sababu alikuwa alikuwa akiendelea kuchukua fedha zako. Kwa hiyo, nipende tu kusema kwamba suala hili liko wazi kabisa *amnesty* iliyotolewa na Mheshimiwa Rais nadhani inatosha na nipende tu kukubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala hili. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia watu wanazungumza nilikuwa Katibu Mkuu kweli na mimi ningekuwa Katibu Mkuu leo, mimi ningemshauri Rais. Nisingemshauri jinsi ambavyo ninyi mmemshauri, mimi ningemshauri vinginevyo kwa sababu kuna aina nydingi ya kum-penalize mtu, sio lazima umfukuze kazi, unaweza kum-demote, unaweza kumkata mshahara, kuna vitu vingi ambavyo unaweza kufanya bila kwenda kwenye hiyo ex..., ndio maana ninazungumza suala la *human face*. Kwa hiyo, mimi ningekuwa Katibu Mkuu ningemshauri Rais vinginevyo, kwa hiyo ninyi hamkumshauri Rais inavyopasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaona vibaya sana kwa jinsi watu wamekatwa kodi, wamefanya hivi na wengine wameajiriwa kwa kile kigezo cha darasa la saba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tupige kura, tujue moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji mwenye shilingi yake kabaki nayo, kwa hiyo, nitawahoji, wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Ruth Molle!

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi nipo kwenye mshahara wake Waziri wa Utumishi wa Umma, Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika na Msaidizi wake Angella Jasmine Kairuki, hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake na katika michango yetu tulioionyesha sisi mambo mengi makubwa na mazito ambayo yanakwenda ndivyo sivyo watu wanaoteswa, kupigwa na kukamatwa Mheshimiwa Waziri akasema hayo hayako kwangu. Akasema nanukuu Waziri wa Utawala na Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika anasema hivi; "kwamba kazi yake kubwa vijana anaowaongoza Wizara inayosimamia Idara ya Usalama wa Taifa ni kukusanya habari na kuishauri Serikali sio wajibu wao, haitakuwa kazi idara hiyo kufuatilia wahalifu" Nanukuu maneno ya Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inakuja pale ambapo vijana wanatenda ndivyo sivyo, sisi tumesema kwamba kuna aina ya baadhi ya watumishi wako usiwakatalie kwamba wanatenda vitendo kinyume na sheria. Tumetoa maelezo mbalimbali tukasema Mheshimiwa Zitto alisema yule Kangoye Diwani, tumesema Alphonse Mawazo na tumewataja wengi, kuna Hananasif juzi Daniel tumesema wengi kabisa na vijana sita wa kule Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba nikuambie kwamba utuambie uhakika gani, ututhibitishie, utupe *commitment* yako kwamba endapo vijana wako sasa watagundulika au tutawagundua wanakwenda kinyume na taratibu na sheria hizo utawafanya nini? Tuna namba za gari na mimi nitakupa kwa faragha hizo namba za gari ambazo zimetumika kuchukua vijana sita kule Pemba, wamepigwa kwenye nyayo, nyaya wako taabani kwamba sisi tutakupa namba za gari ambazo zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* yako je, pindi ikigundulika kwamba ni vijana wako utafanya nini, vinginevyo shilingi yako na jirani yako itaondoka, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shilingi kama sitapata majibu mazuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kabla hujasimama, ili kuweka kumbukumbu sawa, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Angella Kairuki ni Waziri wa Madini, sio Naibu Waziri wa Utumishi.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba ni Waziri Mstaifu wa Utawala Bora, ni jirani yake yule ni Wizara aliyongoza kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufananuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi katika kuwasilisha hoja yangu nilieleza nini kazi za Usalama wa Taifa. Nilisema Usalama wa Taifa kazi yake kukusanya habari na kuishauri Serikali, anapotokezea mtu ameiba, mtu ameua ni *police case*, madhara yote yanayofanyika sio kazi ya Idara ya Usalama kukamata watu na nilisoma kifungu asubuhi pale kwamba *TISS* imetiliwa mkazo katika sheria ile kwamba kwa namna yoyote ile haitokuwa kazi yake kukamata mhalifu katika *ku-enforce* sheria, sio kazi yao, kazi yao kutafuta habari na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu yangu Masoud hayo unayoyasema kama kuna watu wametendewa sivyo, kuna mahali kwanza wanaweza kwenda mahakamani lakini hata kama wakienda mahakamani, watakaoshughulika na hiyo kesi hawatokuwa *TISS* kwa sababu sio kazi yao kukamata wahalifu na kuwashitaki, kazi yao ni kutafuta habari na kuishauri Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nilichomueleza Waziri wa Utawala Bora ni kwamba sisi baada ya matukio ya kule Kisiwani Pemba kuna namba za gari ambazo zipo na nikamueleza Mheshimiwa kutokana na hali hii kwamba matatizo haya yanaonekana na kama ukienda *ZRB* namba hizo utagundua ni watu wa aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja ili jambo hili mbali ya kumpa hizo namba kwa faragha, sositaji hizo namba za gari kwa jinsi nilivyo na jinsi idara yake anasema ni faragha, nitakupa namba hizo ambapo utaona mwenyewe ukipiga simu tu kwa Kamanda wa Polisi Kaskazini Pemba utapata habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ili jambo hili likomeshwe, naomba nitoe hoja ili jambo hili tuweze kulifuatilia kwa makini ili jambo hili iwe ni fundisho kwa watu wengine, nashukuru sana. Naomba kutoa hoja.

*(Hoja Iilitolewa lamuliwe)*

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Tizeba, Mheshimiwa Angella Kairuki, Mheshimiwa Mtulia, Mheshimiwa Mwakasaka, Mheshimiwa Julius Kalanga, Mheshimiwa Lucy Magereli na Mheshimiwa Rukia. Haya Mheshimiwa Julius Kalanga!

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi, lakini ukiangalia majibu ya Serikali na hoja zinazotolewa na Wabunge kwamba kwa mujibu wa sheria *TISS* hawaruhusiwi ku-enforce law kama anavyosema. Lakini katika mazingira ya kawaida zipo taarifa kwamba wanahusika na Serikali haijawahi kutoa kauli kuhusu mambo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliwahi kutokea kwamba Mbunge mwenzetu mmoja wakati huo akiwa Serikalini, Mheshimiwa Nape alitishiwa bastola hadharani na polisi wakasema huyu sio mtumishi wetu na kama polisi sio mtumishi wao japo *OCD* alikuwepo wakati ule mpaka leo huyo mtu hajakamatwa. Hivi angekuwa ni raia wa kawaida kweli asingekamatwa mpaka sasa hivi? Mnataka kutuambia polisi wetu hawana intelijenisia ya kukamata wahalifu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hilo, hata wakati wa Mkutano wa CCM akina Bashe walikamatwa na taarifa zikasema ni Usalama wa Taifa waliwakamata, lakini hakuna kauli ya Serikali iliyokanusha hiyo. Kwa mazingira gani mnatuaminisha kwamba hawahusiki? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kunipa nafasi niweze kuongelea jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Serikali isikwepe majukumu yake kwa sababu Kisiwa kile cha Pemba ni kidogo, gari zilizokwenda kuwachukua hawa zinajulikana na namba zipo na kwa kweli kile kisiwa chenyewe hasa gari ikionekana inajulikana hii inatoka sehemu gani. Kwa nini Serikali ilishaambiwa namba zipo tutawapa, wameshindwa kuwafuatilia, ina maana ni *direct* kuwa Serikali inahusika na kukamatwa watu hawa. Watu wamekamatwa wamepelekwa huko, wamefungwa wakionekana katika mazingira kama yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamuomba Mheshimiwa Waziri jambo hili usilikwepe tukupe namba zile watu wafuatiliwe na wajulikane walikamatwa na nani na kwa kisa gani. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele imeshagonga. Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. ABDALLAH S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi napingana na hii hoja, kwanza niseme tu vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi vizuri sana. Lakini unapotoa malalamiko, *hear says* Serikali imeshasema kwamba haihusiki, kama mna ushahidi na uhusika muende mahakamani, muende polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anazungumzia suala la CCM...

**WABUNGE FULANI:** Buuuuuu!

**MHE. ABDALLAH S. A. MTULIA:** Ukirusha jiwe gizani ukisikia yalaa maana yake limempata. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Bidhaa.

**MHE. ABDALLAH S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usalama ni suala nyeti sana, sio suala la kuja na uvumi, namba ya gari tutahakikisha viyi hiyo namba ya gari huja-note, una gari unayoipenda wewe yaani utatuhakikishiaje kwamba hii namba ya gari...

**MBUNGE FULANI:** Unapenda wanaume wenzako balaa.

**MHE. ABDALLAH S. A. MTULIA:** Ni kweli ilikuwepo kwenye tukio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii haina msingi kwa kweli, naungana na maeleo ya Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge niwaombe na humu Bungeni kuna wageni mnawaona wapo...

**MBUNGE FULANI:** Wajue!

**MWENYEKITI:** Hapana, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo kwa sababu kama ikanza zomea humu ndani kuna upande ambao wapo wengi wakiamua kuzomea sijui kama tutasikilizana humu ndani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kila mtu ujitalidi kwa sababu wewe ukipewa fursa ya kuzungumza unasilizwa, sikiliza na wewe wenzako, ni utaratibu wa kawaida na uzuri wengi wanaopiga hizo kelele wanatoka chama chenye jina zuri kabisa linalotambua demokrasia. Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi. Naunga mkono maelezo ya Mheshimiwa Mkuchika kama alivyoongea kuhusu mipaka ya kazi; kila idara ina mipaka yake ya kazi. Wametajwa polisi hapa, lakini niende kwa mtoa hoja Mheshimiwa Masoud.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la namba za gari hata hapa ninaweza nikaandika namba za gari zozote nikaweka, lakini kuna watu wanavaa nguo za vyama, ninaweza nikavaa nguo ya chama fulani wakati mimi ni chama fulani, ni kitu watu wanafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuache vyombo ambavyo vinahusika ili viweze kufanya hiyo kazi. Hili suala la watu kupatiwa madhara wote hatulipendi na halitokei upande mmoja tu, leo Mheshimiwa wa Nyang'hwale ameongelea wale akina mama ambao waliuwawa kule. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo sisi tunatakiwa kuishauri na kuisaidia Serikali kwamba hapa kuna tatizo fulani. Tumeona

jambo fulani ambalo tuna ushahidi nalo, wapo polisi ambao wanashughulikia masuala haya, lakini tukienda kwamba eti kulikuwa na namba za gari basi tuzichukulie hizo, je, zile za bandia inakuwaje? Kwa hiyo, tufuate sheria inasema nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunadhulika na suala la usalama, hakuna ambaye haitaji usalama, tusiwe na *double standard* kwa sababu ni wanasiasa, wote tunadhulika. Kwa hiyo, sio mwana CHADEMA peke yake au mwana CCM peke yake ambaye anapatikana na matatizo haya ambayo yanatokea. Kwa hiyo, tusifanye ushabiki wa kisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Serikali, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kumuunga mkono Mheshimiwa Masoud, liko tatizo kwenye Taifa hili; msifumbe macho wala msidhani ya kwamba ni suala la kawaida sana...

**WABUNGE FULANI:** Buuuuuu!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

(*Hapa vipaza sauti villzimwa kwa muda*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnanilazimisha kusimama lakini naomba tusikilizane, nadhani tumeshakubaliana hii habari ya kuzomeana haipo kwa sababu hakuna upande ambao hauwezi kuzomea, imeshaisha hiyo. Mheshimiwa Magereli. (*Makofi*)

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza ya kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Masoud na kwamba kama Taifa kuna jambo la kujadili hapa, kuna hoja ya kusikilizwa, kuna hoja ya kufanyiwa maamuzi. Mheshimiwa Kepteni Mkuchika bahati nzuri tumehudumu pamoja kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama. Suala hapa si

kutetea *TISS* wala kuishutumu *TISS* na ninadhani hatulazimiki kuzungumza habari ya *TISS* hapa, tunajadili suala la usalama wa Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mlidhani awali orodha hii ndefu ya watu wanaouliwa, wanaopotea, wanaotishwa, na mimi ni mmoja wao kati ya watu waliotishwa na hata namba za simu, ukiachilia *plate number* kama mtabadili basi mimi ninazo namba za simu za watu wanaotisha na kuteka watu na kuwapoteza ambapo hata na mimi walijaribu kunitisha.

Kwa hiyo, suala hapa sio *TISS*, suala hapa ni usalama wa Watanzania, suala la usalama wa Watanzania liko katika hali tete, hili tusifikiri ni la fulani ama fulani, hali si shwari. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Tizeba.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linalojadiliwa ni kubwa sana na ili tu kuliweka sawa jambo analozungumza Mheshimiwa Masoud, nitajitolea mfano mimi mwenyewe. Mwaka 2002 nilikuwa natoka Benako nakwenda Karagwe majira ya saa 11.00, ametokea mtu barabarani amevaa *uniform* za polisi akatusimamisha na sisi tukatii tukasimama, tumetii timesimama ametoa bunduki, njooni hapa tukaanza kukaguliwa mifukoni, katuchukulia pesa zetu zote. Tulifanya jambo hilo kwa kuamini kwamba yule ni afisa wa polisi kavaa *uniform* zake halali, kila kitu na tukatii sheria tukaishia katika kuporwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hili jambo lina hizo sura mbili, sura za udanganyifu na wakati mwingine sura ya kweli, niseme tu kwamba Serikali hairuhusu maafisa wake kuvuka mipaka ya kazi zao, na akibainika anafanya hivyo anachukuliwa sheria. Iko mifano mingi, akina Zombe walipelekwa mahakamani, walikuwa Maafisa wa Polisi wa Serikali. Zombe alituhumiwa kwa kufanya makosa, alikamatwa, akashtakiwa pamoja na wenzake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vyema raia, viongozi, yejote, anapokutana na kadhia au hali ya namna hiyo ajiridhishe tu kwamba anachokiona ndicho chenyewe. Na njia nzuri Waheshimiwa Wabunge ni kuripoti palepale polisi *and then later uwa-accuse* polisi kwa kutofanyia kazi ulichowaripotia. Lakini kusema tu kwamba alivaa *uniform* au nilliona gari inafanana sidhani kama inatosha kutufanya sisi tubadilishe au tukubali kwamba sasa mipaka ya vyombo vyetu inakiukwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakubaliana na maoni ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angella Kairuki.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na hoja au maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Ameeleza vizuri kuhusiana na kifungu cha 5 cha Sheria ya Usalama wa Taifa, mgawanyo uko wazi, Usalama wa Taifa ni Usalama wa Taifa, polisi ni usalama wa raia. Lakini vilevile ni bahati mbaya tu kwamba chombo hiki hakiwezi kwenda hadharani kuweza kujitetea kwa hiyo, *tusi-take advantage* kuhusiana na upenyo huo kwamba hawawezi kwenda hadharani kujitetea wenyewe kuanza kuwalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani badala ya kuwalamu, badala ya kuwashutumu, badala ya kuja na tuhuma ambazo hazina hata uthibitisho, tuwaunge mkono, tuwatie moyo. Wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa ajili ya kutulinda sisi wote hapa, ni kwa sababu tu mambo mengi unakuta wanayazuia, lakini tunakua hatupewi taarifa ndiyo maana inawezekana tunakichukulia chombo hiki kwa wepesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana suala hili limekuwa likielezwa kwa muda mrefu. Kwenye Kamati kama alivyoeleza Mheshimiwa Magereli, limekuwa likielezwa, lakini bado unashangaa suala hili linaendelea *ku-feature*. Nadhani ifike wakati sasa lifike mwisho, tuwape heshima yao, tuwatie moyo ili waweze kufanya kazi kwa uzuri zaidi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud, naona umeridhika!

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ndio Mbunge mkongwe kuliko wote humu ndani ya Bunge hili aliye kwenye Kamati ile kwa muda mrefu, hakuna asiyejua, kwa hiyo hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba nimemshauri Waziri, Mheshimiwa Kepteni Mkuchika, kwamba sisi tumpe nambari za gari yeye baadae atafuatilia. Na hii imekuja baada ya Kamanda wa Polisi Kaskazini Pemba sisi kupiga ripoti, Kamanda wa Kusini Pemba kupiga ripoti, baadaye Kamishna wa Polisi Zanzibar, Kamishna wa Operesheni Tanzania nzima, Waziri, Mheshimiwa Kepteni Mkuchika nimecaa naye, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, nimecaa naye na Waziri Mkuu binafsi nimekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana nikasema kuna mambo ya faragha nitakupa namba ufuatilie, najielewa, najijua. Haya mambo ni mengi, makubwa na mazito na tukasema lazima haya mambo yakomeshwe. Kwa hiyo kipi kimewekwa hadharani Mheshimiwa Dkt. Tizeba? Hakuna mambo kama ya kufanana fanana, nasema tutakupa mambo kwa faragha ufuatilie kwa faragha uone. Lakini nataka jambo hili likome, kama tukimwaga kila kitu hapa itakuwa si vizuri.

Kwa hiyo, ni Mjumbe pekee wa Kamati ambaye nimecaa miaka mingi kwenye shughuli hii na wewe Mheshimiwa unafahamu. Kwa hiyo, haya mambo mkae Serikali mjue tu kwamba kuna watu kama wanatenda ndivyo sivyo, kinyume na sheria wakomeshwe, ni hilo langu mimi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masoud kwa kurudisha shilingi. Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa inahusiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ni kuhusiana na tozo. Mwaka jana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo, TAMISEMI ilishapita.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya muda ule haukuniita, kwa hiyo, nitaomba nafasi wakati mwingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza napenda nimshukuru Waziri, Mzee wangu Mheshimiwa Mkuchika, kwa kutoa ufanuzi wa vifungu vya Sheria Namba 15 ya mwaka 1996, Sheria ya Usalama wa Taifa, kwamba hawaruhusiwi kukamata, hawaruhusiwi kupekuapekua watu, kufuatiliafuatilia watu. Lakini Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba Maafisa Usalama wa Taifa sasa hivi wanakamata na wanapekuapekua watu na kuna ushahidi unaotosha kuonesha jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilieleza kuhusiana na kisa cha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, Ndugu Simon Kanguye ambaye miezi tisa sasa haonekani. Ndugu Kanguye amekamatwa na *DSO*wa Wilaya ya Kibondo, amefuatwa Ofisi ya Chama cha Mapinduzi ya Wilaya, kapelekwa Ofisi ya Mkurugenzi, amesaini nyaraka za Serikali. Katoka pale *DSO* wa Wilaya ya Kibondo amemkamata. Wana-CCM wenzake wakaenda polisi, *OCD* wa Kibondo akasema sina mamlaka tena na huyu *DSO*. Jambo hili limeripotiwa polisi dakika chache baada ya Bwana Kanguye kukamatwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali ya kawaida tu, na hasa ninyi wana-CCM ambao huyu ni Diwani wenu, ni

Mwenyekiti wenu, ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama chenu ya Mkoa na chama chenu kinasema kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake; tupeni maiti ya Kanguye tukamzike kwa heshima zetu za Mkoa wa Kigoma. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijampa Mheshimiwa Waziri kujibu hoja, nilishawakumbusha hapo mwanzo, nakumbusha tena kwa sababu tunaendelea na hili zoezi. Kwenye kifungu kama hiki unaleta jambo mahususi linalohusu sera, sio jambo la mtu mmoja, kama ambavyo wengine niliwakatalia waliozungumzia hoja za majimbo yao. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshukuru ndugu yangu, Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa swali lake. Naomba kusema hivi, mimi ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, sio Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwa maelezo yangu asubuhi nilieleza kwenye mgawanyo wa kazi kama huyu bwana ameuawa, kama ameumizwa, *it is a police case*, ni kesi ya polisi, mnaihamishiaje Usalama wa Taifa? (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninachotaka kusema, mwenzangu ameyaeleza kwa undani kwa jinsi anavyofahamu, na mimi nina *version* yangu ambayo nimeifanya kwa kuheshimu. Mheshimiwa Zitto mimi namheshimu, tuko vyama mbalimbali lakini kichwa yake nzuri, vyama mbalimbali alinieleza suala hili nikaona linatoka kwa Mheshimiwa Zitto Kabwe, kiongozi wa chama, nimelifuatilia na upande mwingine unahitilafiana na wewe, sasa hapa si mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kusema niliyojua baada ya kufuatilia haya, alikwenda kuombwa na Mkurugenzi twende ofisini kuna *documents* za kusaini. Mheshimiwa Zitto hapa *version* aliyonayo ye ye alikwenda kuchukuliwa na *DSO*. Haya sasa ingekuwa mahakamani si kila upande ungetoa mashahidi? Sasa hapa si mahakamani, hapa sisi tunapiga sera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba suala hili liliripotiwa polisi kwa taarifa nilizonazo, na kwa mujibu wa mgawanyo wa kazi ndani ya Serikali, anayepeleza kesi ni polisi, nipeni shilingi yangu hiyo Mheshimiwa Zitto Kabwe. Hapa si suala la Idara ya Usalama, *this is a police case*, mahali popote pale mtu ameuawa, amepigwa ni kesi ya polisi. Kama wa Idara ya Usalama watahusika wataitwa polisi waende wakatoe ushahidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, naomba ukae.

Waheshimiwa Wajumbe, mtakumbuka, kwa sababu Kiti huwa kinapokea malalamiko mengi sana; nilimkalisha Mheshimiwa Sakaya, nimemkalisha Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kwa sababu ya kuzungumzia hoja ambayo iko kwenye majimbo yao na ye ye amezungumza jambo ambalo halihusu sera, linahusu mtu mahususi. Kwa hiyo tutaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* ..... Sh. 356,529,333/=  
Kif. 1003 – *Government Comm. Unit*..... Sh. 262,960,000/=  
Kif. 1004 – *Procurement Management Unit*...Sh.263,334,000/=  
Kif. 1005 – *Internal Audit Unit*..... Sh. 259,835,000/=  
Kif. 1006 – *Planning Division* ..... Sh. 374,298,000/=  
Kif. 1007 – *Info. & Comm. Tech. Unit*..... Sh. 226,427,000/=  
Kif. 2001 – *Policy and Development Div*..... Sh. 560, 884,905/=  
Kif. 2002 – *Management Services Division*... Sh. 661,591,000/=  
Kif. 2003 – *Establishment Division* ..... Sh. 673, 065,667/=  
Kif. 2004 – *Ethic Promotion Division* .....Sh. 390,306,000/=  
Kif. 2005 – *Human Capital Mgt Division*.....Sh.1,123,507,000/=  
Kif. 2006 – *Performance Contracting*..... Sh. 457,166,000/=  
Kif. 3001 – *HR Development Div*. .....Sh. 5,906,776,000/=

**MWENYEKITI:** Nawakumbusha tena, maana hata watu wa Serikali mmenyamaza kimya kifungu kinaafikiwa?

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3004 – *Diversity Management Unit* ..... Sh. 239,932,000/=  
Kif. 4002 – *Mgt. Info. System Division*.....Sh. 7,192,928,416/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 4 – Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu**

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*..... Sh.1,163,242,375/=  
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ..... Sh.165,947,312/=  
Kif.1003 - *Planning, Monitoring & Evaluation*  
    *Unit* .....Sh.171,717,000/=  
Kif. 1004 – *Info. & Comm. Tech. Unit* ..... Sh.104,154,000/=  
Kif. 1005 – *Legal Services Unit* ..... Sh.10,500,000/=  
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* ..... Sh.101,734,202/=  
Kif. 1007 – *Government Comm. Unit* ..... Sh. 7,690,000/=  
Kif. 1008 – *Procurement Mgt. Unit*.....Sh. 82,564,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 4001 – *Archive Management Division* .... Sh. 294,425,692/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sungura.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye kifungu cha 4001, *sub-vote 21114 - personnel allowances (Discretionary) optional*. Ukiangalia mwaka uliopita kulikuwa kuna sifuri, lakini mwaka huu imewekwa shilingi 600,000 tu. Tukiangalia Idara hii ya *Archives Management Vision* ni idara ambayo ndiyo inatunza kumbukumbu za Taifa. Sasa kuweka kwa watu ambao wanatunza kumbukumbu za Taifa lakini pia kumbukumbu muhimu kwa mujibu wa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawekaje *personnel allowances (Discretionary) optional*ya shilingi 600,000 na kazi hii inayofanyika ni kubwa. Ningeaomba ufanuzi kutoka kwa

Mheshimiwa Waziri kwa nini eneo hili ambalo ni muhimu sana, eneo ambalo linategemewa, kwa nini limewekewa pesa ndogo kiasi hiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hutumika kulipia posho mbalimbali za kiutumishi ikiwemo posho za vibarua. Kifungu hiki ni kipyä hakikuwemo kwenye mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa hiyo mwaka huu kwa kuona umuhimu wake tumeona tuweke kifungu hicho.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 4002 – *Records Management Division* ... Sh. 449,214,559/=  
Kif. 4003 – *Records Center Division*..... Sh. 294,913,186/=  
Kif. 4004 – *The Founders of the Nation Center Division* .....Sh.123,529,674/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 9 – Bodi ya Mishahara na Maslahi**

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*..... Sh.501,554,800/=  
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* ..... Sh.133,256,000/=  
Kif. 1003 – *Planning Unit* ..... Sh.103,903,000/=  
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* ..... Sh.19,500,000/=  
Kif. 1005 – *Legal Services* ..... Sh.144,440,000/=  
Kif. 1006 – *I Comm. Technology* ..... Sh.61,519,642/=  
Kif. 2001 – *Productivity and Research Unit*....Sh.572, 696,358/=  
Kif. 2002 – *Remunaration Unit* .....Sh.115,565,200/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 20 – Ofisi ya Rais Ikuu**

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt..... Sh.22,644,912,748/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 30 –Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif. 1001 -*Administration And HR Mgt..... Sh. 396,005,310,000/=*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts..... Sh. 499,264,000/=*

Kif. 1003 - *Policy and Planning ..... Sh.486,768,000/=*

Kif. 1004 - *Internal Audit Unit .....Sh. 290,828,000/=*

Kif. 1005 –*Info. & Comm. Tech. Unit..... Sh. 244,166, 000/=*

Kif. 1006 –*Procurement Management Unit Sh. 274,360, 000/=*

Kif. 2001 –*Cabinet Secretariat .....Sh. 1,679,728,000/=*

Kif. 2002 – *Government Communication ... Sh. 370,970,000/=*

Kif. 2003 – *Good Governance .....Sh. 476,975,000/=*

Kif. 2004 –*Public Service Appeal .....Sh. 469,944,000/=*

Kif. 2005 – *Public Sector Reform*

*Coordination Unit.....Sh. 359,967,000/=*

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili**

Kif. 1001 - *Admin. and HRM .....Sh.1,998,533,496/=*

Kif. 1002 – *Finance and Account ..... Sh. 406,370,400/=*

Kif. 1003 – *Planning, Monitoring &  
Evaluation Unit.....Sh. 226,681,500/=*

Kif. 1004 – *Government Comm. Unit ..... Sh.136,585,700/=*

Kif. 1005 – *Procurement & Mgt Unit .....Sh.103,749,200/=*

Kif. 1006 – *Internal Audit .....Sh.163,620,000/=*

Kif. 1007 – *Info. and Comm. Tech. Unit .....Sh.182,528,400/=*

Kif. 1008 – *Legal Service Unit .....Sh.245,000,000/=*

Kif. 2001 – *Public Service Leaders Division ....Sh. 806,798,796/=*

Kif. 2002 – *Political Leaders Division ..... Sh. 557,352,000/=*

Kif. 2003 – *Zonal Offices.....0/=*

Kif. 2004 – *Zonal Office- Northern Zone .....Sh. 412,650,892/=*

Kif. 2005 – Zonal Office- Southern Zone .....Sh. 380,955,700/=  
Kif. 2006 – Zonal Office-Central Zone ..... Sh. 394,121,000/=  
Kif. 2007 – Zonal Office-Eastern .....Sh. 304,897,100/=  
Kif. 2008 – Zonal Office-Southern Highlands....Sh.394,325,200/=  
Kif. 2009 – Zonal Office-Lake Zone .....Sh. 423,250,656/=  
Kif. 2010 – Zonal Office-Western Zone ..... Sh. 324,453,960/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**Fungu 67 - Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira Katika  
Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 – Administration And HRM..... Sh. 952,314,000/=  
Kif. 1002 – Finance and Account .....Sh.150,781,000/=  
Kif. 1003 – Planning, Monitoring &  
Evaluation .....Sh. 58,153,105/=  
Kif. 1004 – Government Comm. Unit..... Sh. 59, 525,895/=  
Kif. 1005 – Legal Service Unit .....Sh. 67,262,000/=  
Kif. 1006 – Procurement Management Unit .. Sh. 72,540,000/=  
Kif. 1007 – Mgt. Information System Unit.....Sh.140,380,000/=  
Kif. 1008 – Internal Audit Unit .....Sh. 108,100,505/=  
Kif. 2001 – Recruitment Mgt Division ..... Sh. 578,690,000/=  
Kif. 2002 – Quality Control .....Sh.185,932,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**Fungu 94-Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001- Administration & H R M.....Sh. 2,162,172,561/=  
Kif. 1002 –Finance and Accounts Unit ..... Sh. 203,736,330/=  
Kif. 1003 – Planning, Monitoring &  
Evaluation Unit.....Sh.512,894,000/=  
Kif. 1004 – Internal Audit Unit .....Sh. 75,580,000/=  
Kif. 1005 – Procurement Management Unit....Sh. 37,972,000/=  
Kif. 1006 – Legal Service Unit .....Sh. 52,380,000/=  
Kif. 1007 – Government Com. Unit.....Sh.109,361,109/=  
Kif. 1008 – Info. Comm.Tech.Unit ..... Sh. 91,692,000/=  
Kif. 2001 – Civil Service.....Sh. 426, 809,000/=

Kif. 2002 – *Local Government Service* ..... Sh. 402,471,000/=  
Kif. 2005 – *Health's Service*..... Sh. 331, 211,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **MPANGO WA MAENDELEO**

#### **Fungu 4 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka**

Kif. 1001- *Administration and HRM*.....Sh. 0/=  
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation*.....Sh. 5,178,872,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif. 1003 – *Police And Planning* .....Sh.175,055,489,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 – *Administration & HRM*..... Sh. 3,000,000,000/=  
Kif. 1006 – *Planning Division*.....Sh. 0/=  
Kif. 2002 – *Policy Devpt. Division*.....Sh. 0/=  
Kif. 2004 – *Ethic Promotion Division*.....Sh. 0/=  
Kif. 2005 – *Human Capital Management Division*.....Sh.0/=  
Kif. 2006 – *Perfomance Contracting*.....Sh.0/=  
Kif. 4002 – *Mgt. Info. System Division*.....Sh. 7,939,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili**

Kif. 1001 – *Administration and HR M*.....Sh. 2,107,800,000/=

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ..... Sh.42,100,000/=  
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation*.....Sh. 252,533,992/=  
Kif. 1004 - *Government Communication*..... Sh. 58,099,600/=  
Kif. 1007 – *I and Com. Technology Unit* .....Sh.180,000,000/=  
Kif. 1008 –*Legal Service Unit* .....Sh. 213,330,000/=  
Kif. 2001 – *Public Service Leaders Division*.....Sh. 50,700,000/=  
Kif. 2002 – *Political Leaders Division* .....Sh. 647,661,748/=  
Kif. 2003 – *Zonal Offices*.....Sh. 0/=  
Kif. 2004 – *Zonal Office-Northern Zone* .....Sh.13,322,000/=  
Kif. 2005 – *Zonal-Southern Zone* .....Sh.114,447,165/=  
Kif. 2006 – *Zonal Office- Central Zonal* .....Sh.114,447,165/=  
Kif. 2007 – *Zonal Office- Eastern Zone* .....Sh.114,447,165/=  
Kif. 2008 – *Zonal Office-Southern Highland*....Sh.114,447,165/=  
Kif. 2009 – *Zonal Office-Lake Zone* ..... Sh.13,322,000/=  
Kif. 2010 – *Zonal Office- Western Zone*.....Sh.13,322,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 67 - Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma**

Kif. 1007 – *Mgt. Info. Systems Unit* ..... Sh. 750, 000,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

(*Bunge Linarudia*)

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Mtoa Hoja taarifa!

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3)(a) na (b) ya Kanuni

za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake naomba sasa taarifa ya Kamati ya matumizi ikubaliwe na Bunge, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja IIitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora inayohusu Makadilio ya Mapato na Matumizi. (*Makof*)

*(Hoja IIiamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana.

Pongezi nyingi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, lakini pia watumishi unaofanya nao kazi niwapongeze kwa kuleta makadirio haya ambayo Bunge limeyapitisha leo na mimi nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyofanya ya kumshauri Mheshimiwa Waziri kwenye maeneo mbalimbali katika kipindi cha Kamati na hatimaye kutuletea hiyo taarifa hapa ambayo leo Bunge limeweza kuidhinisha makadilio hayo ya mapato na matumizi. Kwa hiyo, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri. (*Makof*)

Hata hivyo, pia nichukue fursa hii kumtakia Mheshimiwa Waziri pamoja na watumishi anaofanya nao kazi kila la kheri kwenye utekelezaji sasa wa bajeti hii ambayo imeidhinisha na Bunge siku ya leo. Tunaamini kwamba yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge walikushauri katika kipindi cha Kamati na hata tulipokutana hapa kama Bunge zima tutayatilia maanani na utayafanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo,  
naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.40 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumanne,  
Tarehe 17 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi*)